ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nne – Tarehe 25 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 107

Muendelezo wa Mradi wa *TASAF*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Haji Mkema Haji) - Aliuliza:-

Tunaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia miradi ya *TASAF* hapa Zanzibar. Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo kwa kuitumia miradi hiyo katika mpango wa MKUZA.

(a) Mhe. Waziri, baada ya kumalizika kwa mafanikio Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mradi wa *TASAF*. Je, serikali ina mpango wa kuendelea na mradi huo katika Awamu ya Tatu.

(b) Kama iko Awamu ya Tatu, utekelezaji wake utaanza lini.

(c) Katika mradi huo wa *TASAF* Kamati ya Uongozi ya *TASAF* Pemba imefanya ziara Tanzania Bara mara mbili kwa kujifunza kwa wenzao, kwa nini Kamati ya Uongozi ya *TASAF* Unguja haijafanya ziara kama hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 107 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, *TASAF* awamu ya kwanza imemalizika na *TASAF* awamu ya pili inaendelea ambapo inatarajiwa kumalizika mwaka 2012 baada ya kupata muda wa nyongeza.

b) Mhe. Spika, *TASAF* awamu ya tatu itakuwepo na serikali zinaendelea na mazungumzo pamoja na maandalizi

ikishirikiana na Washirika wa Maendeleo. Taarifa rasmi ya utekelezaji itatolewa wakati maandalizi yatakapomalizika.

c) Mhe. Spika, ziara za kubadilishana uzoefu baina ya Kamati za *TASAF* Unguja, Tanzania Bara na Pemba zimefanyika kama zifuatazo:

1. Mwaka 2008 Wajumbe kutoka Kamati ya Uongozi, Masheha, Kamati za Usimamizi wa Miradi na Viongozi kutoka Afisi ya Waziri Kiongozi Unguja walitembelea Miradi ya *TASAF* maeneo ya Iringa na Moshi.

2. Mwaka 2009 Wajumbe wengine kama hao walitembelea miradi ya *TASAF* Pemba.

Mhe. Spika, ziara kama hizo kwa Kamati ya Uongozi na Kamati nyengine za *TASAF* tunategemea kuzipanga kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wananchi kwa kutumia miradi ya TASAF wameonesha ari na mafanikio makubwa katika nchi yetu Unguja na Pemba, lakini pia katika ziara hizo huwa ni changamoto kwa kutembelea na kubadilishana mawazo.

Je, Mhe. Waziri, atalieleza nini Baraza hili kwa manufaa ya wananchi

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kwamba miradi ya TASAF imeweza kutoa changamoto na ari kubwa kwa wananchi wetu katika maeneo mbali mbali ili waweze kujipatia miradi ambayo wanaona wao wenyewe inaweza kuwapunguzia umasikini.

Mhe. Spika, faida iliyopatikana katika ziara hizo kwanza wamekwenda kujionea ni namna gani wenzetu walivyojitahidi kupiga hatua za maendeleo kwa kushirikiana katika miradi hiyo ya TASAF. Vile vile, unapotembelea eneo jengine kutoka eneo ambao ulilokuwepo, wewe mwenyewe basi huwa umeshajifunza mambo mengine mapya. Pengine usimamizi mzuri wa miradi, pia na aina ya ile miradi ambayo imeweza kuibuliwa.Vile vile, jambo jengine ni kuwa kamati zetu hizi wameweza kujifunza namna ya Zanzibar ilivyojitahidi kupiga hatua kubwa sana juu ya miradi hii ukilinganisha na miradi kutoka upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, miradi ya Zanzibar ukiangalia miradi wenyewe na thamani yake kwa kweli inaonesha kwamba wananchi wa Zanzibar wanajitahidi sana na ni wasimamizi wazuri wa fedha kwa ajili ya matumizi kutokana na miradi hiyo. Kwa hivyo, kuna mambo mengi wamejifunza zaidi ya hayo, lakini kubwa zaidi ni kuweza kulinganisha jinsi wao wanavyojitahidi na wenzao kwa upande wa pili.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi siku ya leo kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b):

a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba miradi ya TASAF imeleta mafanikio makubwa kwa upande wa wananchi hapa Zanzibar. Je, wizara yake kama ni wizara inayoshughulikiwa shughuli zote za serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti katika miradi ya TASAF ili wananchi waweze kufaidika zaidi.

b) Kwa kuwa miradi ya TASAF kifedha ni chini ya asilimia 4 inayopatikana kwa Tanzania nzima inayokuja Zanzibar na amethibitisha kwamba hapa Zanzibar imeonesha mfano mzuri katika miradi hii. Je, wizara yake ingefanya nini kupigania kukinyanyua kiwango hiki kama vile ilivyofanya Wizara ya Kilimo kunyanyua mtaji wa bahari kuu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa upande wetu wizara baada ya kufanya tathmini ndio tumeweza kujenga hoja ya kuweza kuongezewa nyongeza ya hili fungu. Mhe. Spika, suala hili kwa sababu miradi ya TASAF sio miradi ambayo inamalizika, miradi hii ni endelevu ndio maana fedha hizi tunazopewa ni kwamba tunajitahidi kuzigawanya katika maeneo mbali mbali kadri lile fungu lilivyokuja.

Pia, tunawashukuru washirika wetu wa maendeleo baada ya kumalizika TASAF ya kwanza na kuona kwamba tumeweza kusimamia vizuri matumizi kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya wananchi, ndio maana tulipojenga hoja wakatukubalia kuendelea na TASAF II. Hii TASAF II vile vile baada ya kuona kwamba tumeendelea vizuri ndio maana tumepata muda wa nyongeza. Kwa hivyo, suala la kuongeza bajeti hii itategemea ni namna gani ya ile miradi tunavyoiendesha, lakini vile vile ni baada ya kurejesha maelezo juu ya ile miradi ndio tunategemea kuwa tunaweza tukafanikiwa kuongeza hilo fungu.

Mhe. Spika, ni kwamba kila kitu kina vigezo vyake katika masuala ya uvuvi wa bahari kuu *nature* ya Zanzibar ni visiwa na ukiangalia mazingira ya visiwa katika suala la uvuvi basi ni suala ambalo linatakiwa kupewa kipaumbele na ndio maana tulipojenga hoja tukaweza kufanikiwa vizuri.

Mhe. Spika, katika miradi ya TASAF kama nilivyosema kwamba hii asilimia 4 ambayo tunaipata bado sio ndogo kwa sababu ukilinganisha kwa hapa Zanzibar na Tanzania Bara ni kwamba Zanzibar sasa hivi utakuta kuna majimbo tayari ina miradi karibu minne wengine mpaka miradi minane ndani ya jimbo moja. Kwa hivyo, ukilinganisha na kule Tanzania Bara na majimbo yao unaweza ukalikuta jimbo pengine lina miradi minne, lakini ule ukaribu unaowafikia wananchi basi kwa Zanzibar inakuwa ni mara kumi zaidi kuliko Tanzania Bara.

Kwa sababu kama unavyofahamu Mhe. Spika, eneo la Zanzibar inawezekana majimbo 12 ya Zanzibar ni sawa sawa na jimbo moja kwa ukubwa kwa Tanzania Bara. Kwa hivyo, kwa upande wa miradi ya TASAF hii asilimia sio ndogo kwa sababu sasa hivi kila jimbo utakalokwenda basi utakuta alama ya mradi wa TASAF ambayo wananchi wameweza kufaidika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, baadhi ya shehia waliibua miradi lakini miradi hiyo iliingiliana na miradi mikubwa ya kitaifa na ikafutwa. Je, haoni iko haja wananchi wa maeneo hayo wakapata fursa ya kuibua miradi mengine wakati bado matatizo yamo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakubaliana sana na wazo la Mhe. Mwakilishi kwa sababu kweli kuna baadhi ya shehia waliweza kuibua miradi lakini baadae kwa kuwa kulikuwa kuna miradi mikubwa ya kitaifa ilikuwa inategemewa kufanyika katika maeneo yale miradi ile ikafutwa. Mhe. Spika, katika shehia hizo hata na mimi mwenyewe muhusika pia ilinikumbuka kadhia hiyo na nilipata tabu sana kwa wananchi wangu kwamba kwa nini tumeshaibua mradi wa ujenzi wa barabara lakini baadae tukaambiwa kwamba sasa hivi *feeder road* kuna taratibu maalum zitashughulikiwa.

Kwa hivyo, mradi ule ukafutwa vile vile na katika shehia nyengine ambazo zimo ndani ya Jimbo la Mfenesini. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi nakuhakikishia kwamba nitakaa na mradi wa TASAF kwa Unguja na Pemba ili kuweza kuangalia ile miradi ambayo iliaghirishwa ili wananchi wale waweze kuibua miradi mengine. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo linatekelezeka na hii itakuwa ni njia moja ya kuweza kuwapa moyo wananchi wetu kwa yale mambo ambayo wameyaibua kuweza kuyashughulikia.

Nam. 16

Kufufua Vinu vya Umeme Pemba

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Naipongeza Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa jitihada yake kubwa juu ya kupatikana umeme wa uhakika huko Pemba, na kuondoa tatizo la kihistoria la umeme wa vinu ambao haukuwa wa uhakika.

Mhe. Waziri, pamoja na matatizo yake vinu hivyo vimesaidia kuzalisha umeme kipindi kirefu. Wizara yako ina mikakati gani juu ya kuviimarisha vinu hivyo ili kuvihifadhi kwa ajili ya matumizi ya dharura.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imetenga katika bajeti yake jumla ya shs. milioni 453 kwa ajili ya kuviimarisha vinu hivyo.

Mhe. Spika, wizara yangu itaendelea kutafuta njia ya kuongeza vinu vya kuzalisha umeme Pemba ili Kisiwa cha Pemba kijitegemee.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kulijibu kiurahisi hili jibu, lakini kimtazamo swali hili ni gumu na zito tunakokwenda hasa tukichukulia mfano huu uliojitokeza hapa kwetu Unguja.

Kwa kuwa mikakati hii imepangwa vizuri kuhakikisha kwamba vinu vyetu vilivyokuwepo Pemba vinaendelezwa na vinaimarishwa. Je, kwa upande wa Unguja pamoja na kadhia hii ambayo inalingana wanaweka mkakati gani wa kutafuta fedha zaidi ili kuhakikisha kwamba pindi ukikatika umeme unatoka Bara kuwe na jenereta la akiba kwa ajili ya huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kadhia ambayo tumekuwa nayo mwaka mmoja uliopita na hii ya sasa hivi tumejifunza vya kutosha. Kwanza nataka nilithibitishie Baraza lako kwamba jenereta ambazo ziko Pemba hazitaondolewa zitaendelea kutunzwa na kufanyiwa matengenezo makubwa ili wakati wowote tatizo litakapotokea Pemba isipate

tatizo kama tulilolipata hapa. Kwa hapa kwetu kwa sasa hivi tunajitayarisha angalau kutafuta jenereta la akiba lenye *mega walt 25*.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba tunavyosikia kutokana na wale mafundi wanaoshughulikia zile jenereta kule Pemba wanatwambia zile jenereta ni za zamani sana na hata hicho kiwanda kilichotengeneza jenereta zile hakipo tena, na sasa hivi kipuri likitokea tatizo inabidi watoe oda ya kuchongea.

Je, haoni kuna haja ya kutafuta jenereta ambazo vifaa vyake vinapatikana kuliko kung'ang'ania yale mabovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwanza nataka kuweka wazi juu ya jambo hili kwamba jenereta zile pamoja na ukongwe wake ni moja ya majenereta yaliyokuwa bora na madhubuti. Ni kweli jenereta zile sasa hivi zimeshapitwa na wakati, lakini katika kipindi cha miaka 10 ijayo bado kampuni ile itaendelea kutengeneza vipuri kwa ajili ya nchi mbali mbali ambazo zinamiliki viwanda vile. Ushauri wako uliousema sasa hivi tujiandae ni kwamba kuna jenereta la kileo kabisa ambazo vipuri vyake vitakuwa vinapatikana huu tunauchukua na tutaufanyia kazi. Lakini hizi ambazo tunazo sasa hivi bado kwa ubora wake ni lazima tuendelee kuzituza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwanza naipongeza serikali kwa jitihada yake ya kutaka kuwaondoshea tatizo la umeme wananchi wa kisiwa cha Pemba. Ni kwamba kwa nia nzuri tayari waya wa umeme kutoka Tanga mpaka Pemba umeshawekwa, lakini kuna baadhi ya vifaa ambavyo vilikuwa bado havijafika ili kuwaondoshea wananchi hilo tatizo la umeme.

Je, vifaa vile tayari vimeshafika ili kuwandoshea wananchi tatizo hilo la umeme na kama havijafika. Je, hawaoni kwamba serikali umeme ule kuanza kuwashwa mwezi wa pili itakuwa imefeli.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, vifaa kwa ajili ya kumalizia kazi hiyo vimeshafika na kazi hiyo inaendelea na Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi juu ya wananchi wa Pemba kwani tunakotoka ni mbali na tunakokwenda tunapaona hapa tujiandae na cherekochereko. Nimesikia wananchi wa Pemba wanajiandaa sherehe kubwa zaidi za kumtafutia zawadi Balozi wa Norway, hilo nimelisikia na sio vibaya hii inaonesha namna ya furaha walionayo wananchi wa Pemba kuona vipi serikali imeweza kulishughulikia tatizo hilo la umeme. Kwa hivyo, tupo karibu kufika safari yetu.

Nam. 8

Ujenzi wa "*Jet*" Kwenye Mahoteli

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Katika maendeleo ya Biashara ya Utalii Zanzibar, umezuka mtindo wa Wawekezaji wa Hoteli kujenga "*JET*" kwenye fukwe zilimo hoteli zao ili kuvutia biashara. Ipo shaka ya kuwa *JET* hizo hujengwa bila ya utafiti wa kina juu ya athari za kimazingira zinazoweza kutokea (*Environmental Impact Essessment*).

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inazingatia vigezo gani kuruhusu ujenzi huo wa *JET*.

(b) Mhe. Waziri, huoni kuwa ujenzi wa *JET* unaleta athari za kimazingira na sifa ya fukwe zetu ambazo bado zinasifika kwa uzuri wake.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mchakato wa kuruhusu ujenzi wa aina yoyote kwa miradi inayoidhinishwa na *ZIPA* kwa kawaida unashirikisha wadau husika wote (*Interested Party*) wakiwemo wasimamizi wa sheria na wataalamu wa mazingira. Mhe. Spika, kwa upande wa suala la utafiti wa athari za Kimazingira, Idara ya Mazingira ambayo ndiyo yenye dhamana ya kulinda na kusimamia mazingira endelevu kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya 1996, ndio inayotoa muongozo na ushauri ambao hutumika kuwa ni kigezo cha kuruhusu au kutoruhusu ujenzi wowote ikiwemo ujenzi wa "*Jetty*" za mahoteli ya kitalii yanayoidhinishwa na *ZIPA*.

(b) Mhe. Spika, ushauri na miongozo inayotolewa na Idara ya Mazingira tunaizingatia na kuyatekeleza ili kukinga athari za kimazingira zisitoke wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi wa mahoteli na miradi mingine inayoidhinishwa na *ZIPA* au taasisi nyengine yoyote inayosimamiwa na wizara hii. Endapo athari za uharibifu wa mazingira zitajitokeza wizara yangu inafuata kikamilifu maelekezo ya wataalamu wa mazingira ili kudhibiti uharibifu zaidi na kuepuka madhara.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa kuwa imetajwa *jetty* hapa ambayo inatoka kutoka nchi kavu mpaka baharini na kwa sababu wale wanaolinda mazingira ya bahari na wao ni sehemu ya ulindaji wa mazingira. Je, maeneo haya yanapotokezea wahusika hawa nao wanashirikishwa kikamilifu au kunakuwa na *study* ambazo hazikukamilika.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ilikuwa ni mtindo kabla ya matokeo ya Nungwi kwamba Idara ya Mazingira ikishakutoa kibali basi *jetty* inajengwa na hakukuwa na ushirikishwaji wa wananchi wenyewe. Baada ya zogo lilitokea Nungwi, sasa hivi tumebadilisha mwelekeo, sasa hivi kamati zote zilizopo katika eneo husika linalojengwa hoteli zitashirikishwa katika ujenzi wa aina hii.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu mama ya Mhe. Waziri, alisema kwamba kuna maelekezo kamili yanachukuliwa kutoka *ZIPA* kuhusiana na suala zima la ujenzi wa *jetty* pamoja na uharibifu wa mazingira. Je, nilikuwa nataka kujua katika ujenzi wote ambao umeshafanyika mpaka hii leo kumeshatokezea uharibifu huo na kama umetokezea je, kuna kitu chochote ambacho kinatakiwa kulipwa kutokana na maharibiko hayo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa kweli hadi sasa wizara yangu haijapata taarifa ya uharibifu wowote wa mazingira.Kwa hiyo, hakuna kima chochote ambacho kimewekwa kwa aliyeharibu mazingira kulipa. Inawezekana labda kuna uharibifu wa kimazingira kuendana na mwenendo wa upepo kwa sababu wakati *jetty* zinajengwa lazima zitakuwa zina-influence mwenendo wa upepo na hata mwenendo wa mawimbi pale ambapo jetty inajengwa.

Huu ni utafiti wa kitaalamu sana ambao sidhani kama umefanyika katika *jetty* zote zilizojengwa kutokana na ukosefu wa utaalamu. Kwa hivyo, kwa ufupi tu niseme kwamba athari za kimazingira bado hazijaripotiwa na hakuna kima ambacho kimewekwa kulipwa.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Katika miradi ya mahoteli. Je, hii jetty inatiwa kabisa malipo yake katika mradi ama inalipwa mbali. Vile vile, nchi nyingi duniani watalii wanakuja Zanzibar kwa kupenda fukwe zetu, lakini imebainika kwamba *jetty* hizo zinaathiri fukwe. Je, na hilo limezingatiwa.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, wawekezaji wanapowasilisha mradi wanawasilisha mradi kamili ingawa baadhi ya wawekezaji huwa wanagawa kwa *phase, phase one* atajenga mpaka kiwango

fulani, *phase two* anamalizia *phase three*. Kwa hivyo, huwa wanawasilisha mradi kamili. Kama nilivyojibu mwanzo hatujapata taarifa ya uharibifu wa mazingira ya fukwe kutokana na ujenzi wa *jetty.K*wa hivyo, wizara yangu bado kama nilivyosema hatuna taarifa hizo.

Nam. 58

Uanzishwaji wa Hifadhi ya Wanyama (*Zoo*) Welezo

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika maeneo ya Welezo nje kidogo ya Mji wa Zanzibar, yupo Mwekezaji aliyeamua kujenga hifadhi ya wanyama wa aina mbali mbali (*zoo*) inayojulikana kwa jina la *Zanzibar Park.*

(a) Je, Mhe. Waziri, Mwekezaji huyu aliyejenga *Zanzibar Park* ni mzalendo au mgeni.

(b) Miongoni mwa wanyama waliopo pale inasemekana ni makobe ambao wanatoka katika kisiwa cha changuu walioko chini ya uangalizi wa vijana wa Mji Mkongwe waitwao *Beach Boys* ambao wamekodishwa kwa dola 400. Je, hilo ni kweli.

(c) Inasemekana ndani ya siku nne za sikukuu ya Eid-El-Fitri iliyopita Mwekezaji huyo aliingiza zaidi ya milioni 17 kwa kupokea wageni kwenye *Park* hiyo. Je, jambo hilo ni kweli. Kama ni kweli serikali ilipata kodi ya kiasi gain.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Muekezaji aliyejenga *Zanzibar Park* ni Mzalendo kwa mujibu wa usajili uliofanywa.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu iliwahi kufunga Mkataba na Mwekezaji wa *Zanzibar Park* wa kumkodisha Makobe Kumi (10) kutoka changuu, hata hivyo mkataba huo haukutekelezwa kwani ulivunjwa rasmi tarehe 16/9/2009 baada ya kupata maelekezo kutoka Kamati ya Baraza lako tukufu ya kufuatilia Hesabu za Serikali. Hivyo, sio kweli kuwa Makobe waliopo *Zanzibar Park* ni kutoka katika Kisiwa cha Changuu.

(c) Mhe. Spika, nasikitika kulieleza Baraza lako tukufu kuwa Wizara yangu haina taarifa juu ya ukusanyaji wa Mapato ya T.shs. 17 milioni pamoja na kima cha kodi kilichopatikana, Kwani hiyo ni kazi ya *ZRB* kupitia Wizara ya Fedha. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri na nimpongeze kwa kufuata maagizo ya Kamati ya *PAC* ambapo nami nilikuwa mmoja wao, lakini naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mwanzo wa mkataba uliyovunjika ulihusisha wizara na mwekezaji ingawa walezi wa makobe wale vijana wa *beach boys* walifanya fujo kidogo. Ningetaka nijue kwa sasa uhusiano wa wizara yake na vijana wa *beach boys* ukoje juu ya makobe wale wa Changuu.

Lakini pili, kwa kuwa malipo ya Wazanzibari wanaoingia pale kuangalia mbuga ile ya wanyama ni shilingi 6,000 kwa mgeni na shilingi 3,000 kwa Wazanzibari. Je, wizara yake sasa itachukua juhudi gani kumshawishi mwekezaji ili malipo yale ya Wazanzibari kuondoshwa ili na wao kufaidi uwekezaji ule wa *Zanzibar Park.*

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, uhusiano wa wizara na *Beach Boys* ingawa hakusema wa wapi, kwa sababu *Beach Boys* wameenea Unguja na Pemba, lakini nadhani amekusudia wale vijana wa Malindi pale. Mhe. Spika, wizara yangu ilichukua hatua ya kuuita uongozi wa Mji Mkongwe na kuzungumza nao. Kwani kitendo walichokifanya vijana wale hakikufurahisha wizara yangu kwani ilikuwa ni kitendo cha kihuni.

Mhe. spika, kuhusu malipo wizara yangu haiwezi kuamua kuondosha malipo yale, kwa sababu ni idadi ndogo ya Wazanzibari wanaokwenda, lakini wengi ni wageni. Hata kama ni Wazanzibari wanaokwenda, basi ni lazima walipe kwa sababu makobe wale ambao idadi yao ni kama 130 wanahitaji huduma na hasa huduma ya chakula. Kama hawakulipishwa wanaokwenda kutizama ina maana mradi ule hautakuwa endelevu, itabidi mwekezaji atoe pesa yake kutunza makobe wale kitu ambacho kwa tabia ya wawekezaji huwa wanataka zaidi kufanya faida kuliko kuendeleza mradi na hasa ambao sio wake ni mradi wa serikali.

Nam. 27

Wanaofanya Kazi katika Mazingira Hatari

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Haji Mkema Haji) – Aliuliza:-

Wafanyakazi wengi wanafanyia kazi katika mazingira ya hatari. Kwa mfano wafanyakazi wa mashamba ya mipira, kwenye viwanda vya kokoto na wanaochanganya lami.

Mhe. Waziri, wizara yako ina utaratibu gani wa kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi ambayo ni ya hatari ili kuona kama hatua za usalama kazini zinazingatiwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Nam. 27 la Mhe. Haji Mkema Haji.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa wafanyakazi wa mashamba ya mpira, kwenye viwanda vya kokoto na wanaochanganya lami wanafanya kazi katika mazingira ya hatari. Katika kukabiliana na mazingira hayo ya hatari wizara yangu inafanya ukaguzi mbali mbali za usalama na afya katika maeneo hayo na mengineyo, ili kuepusha ajali na hatari zinazotokana na mazingira hayo.

Kwa kipindi cha mwezi Julai – Disemba mwaka jana, jumla ya taasisi 81 zilikaguliwa.Halikadhalika sehemu tulizozikagua ni pamoja na viwanda vya kokoto vya Tunguu na Jendele na wachanganyaji wa lami katika ujenzi wa Uwanja wa Ndege Unguja. Aidha, kwa Pemba ni Kiwanda cha Makonyo, Matrekta na Mpira cha Maziwani Pemba.

Wizara inawaelekeza waajiri wa taasisi hizo kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, afya na usalama kazini Nam. 8 ya mwaka 2005 na hadi sasa hatujapokea kesi kubwa za kiafya za taasisi hizo, lakini hata hivyo tunashauri kuzidisha kinga.

Mhe. Spika, wizara yangu inaendeleaje kushirikiana na *ZIPA* ili kuhakikisha kwamba miradi yote inayowekezwa nchini, inaweka kinga katika masuala ya usalama na afya na pamoja na sisi kuendelea kukagua miradi hiyo ili kuepusha ajali sambamba na kutoa elimu. Ahsante.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wizara yake imefanya ukaguzi katika sehemu mbali mbali nyingi sana alizotutajia, kuna mapungufu yoyote yaliyoonekana katika kaguzi hizo. Kama kuna mapungufu yaliyojitokeza, ni hatua zipi zilizochukuliwa kuondosha mapungufu hayo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, mapungufu yanayojitokeza mara nyingi ni vifaa vya kulinda wafanyakazi na vifaa vya usalama kama vile vya kuzima moto sehemu nyengine inakuwa havipo na kadhalika.Zile kasoro ambazo zimeonekana watendaji wetu wanaandikia na kuwaeleza kwamba hapa pamekosekana na hiki na hiki.Kwa hivyo, wazingatie na kurekebisha.

Nam. 18

Vifaa vya Usalama Kazini kwa Wapika Lami

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri, unafahamu kuwa wafanyakazi wa *UUB* sehemu ya kibele hawana vifaa vya kujikinga na madhara wakati wa kazi ya upikaji lami kama vile, helmeti, maski, na wala hawapewi maziwa.

(b) Kwa kuwa mikataba ya kazi ya kimataifa inasisitiza kuwepo kwa mazingira mazuri ya usalama kazini. Je, Wizara yako ina mkakati gani ili kunusuru afya za watendaji wake hao.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kuwa Wafanyakazi wa Idara ya *UUB* hasa wa Kibele wanapatiwa vifaa vya kujikinga na madhara kila pale hali ya fedha inaporuhusu. Vifaa vyote alivyovitaja pamoja na viatu na *"boiler suits"* wanapatiwa karibu kila mwaka. Aidha, wizara yangu inakiri kuwa hadi sasa wafanyakazi wa Kibele hawakupatiwa maziwa ingawa wizara bado iko katika mchakato wa kujiandaa kuwapatia maziwa au posho la kukidhi haja hiyo. Wizara yangu ina utaratibu ambao umeandaliwa wa kuwawezesha wafanyakazi wote wa wizara wanaostahiki kupata posho wakiwemo wa Kibele.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kupata nafasi hii ndogo ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu wafanyakazi hao wanafanya kazi katika mazingira hatarishi kwa afya zao.

Je, ni kila baada ya muda gani wafanyakazi hao hasa wale wapishi wa lami huwa wanapimwa afya zao ili kujulikana kama wameathirika na moshi wa lami au hawajaathirika, tena wote wa Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria za kazi makazini au usalama wa kazi makazini kama Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto alivyokuja kujibu hapa Idara hii ya Usalama wa Wafanyakazi Makazini inatakiwa wao sio waambiwe na idara wanayoifanyia kazi isipokuwa wajipangie kwenda kuangalia afya za wafanyakazi. Isipokuwa sisi kama wahusika wa Wizara ya Mawasiliano tuna utaratibu wa wafanyakazi wetu wote ambao wana matatizo hayo kuwapeleka hospitali kupimwa. Lakini kwa mujibu wa sheria ya kazi kuna Idara maalum ya usalama kazini ambayo inastahiki kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu lake alikiri kwamba wafanyakazi hao wanapewa zile *gears*, yaani viatu, mabuti makubwa na ovarol. Je, wakionekana kwamba hawana huwa wameviuza au vimepitiwa na muda.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, Idara yetu sisi ya *UUB* kwa Unguja peke yake tuna wafanyakazi karibu 599 na kwa Pemba 425. Kibele wako 35, KIbele mara ya mwisho kupewa vifaa hivi ni mwezi wa Oktoba mwaka uliopita na Pemba wafanyakazi zaidi ya 300 walipewa mwezi wa Januari mwaka huu vifaa hivyo.

Sasa Mhe. Rashid Seif Suleiman na Waheshimiwa wengine ukiona mfanyakazi wa *UUB* hakuvaa vifaa hivyo, basi ujue huyo pengine kavifua au kafanya nini. Hata mimi mwenyewe nikikutana nao huwa nawauliza zile nguo na viatu tulivyowapeni bado havijakauka? Kwa sababu kwa mujibu wa kutunza ghala au utunzaji wa mali ya serikali hata kikichanika kinatakiwa kirejeshwe kiwekwe katika ghala ili apewe kipya, huwezi ukasema tu kwamba kimechanika au kupotea huko huko, kuna taratibu za kiserikali ambazo zinastahiki kufuatwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba suala la kuwapatia maziwa wafanyakazi liko

kwenye mchakato. Mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri, hivi hata suala la kuwapatia maziwa linahitaji mchakato.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, hata maziwa yanahitaji mchakato kwa sababu maziwa ni fedha na fedha lazima kuwe na utaratibu maalum. Kwa sababu sisi bahati nzuri wizara yetu kama ilivyo ya miundo mbinu, kwa asilimia kubwa wafanyakazi wengi wa wizara yetu wanahitaji kupata posho maalum kwa sababu kazi zao ni ngumu. Sasa huwezi kwenda kuwachukua wafanyakazi 35 ukawapa hiki na wengine 1500 ukawaachia hiki. Kwa hivyo, sisi kwa kushirikiana na utumishi tunaandaa taratibu ambazo zitawapa posho nzuri ili wafanyakazi wetu waendelee kuipenda Wizara ya Mawasiliano na kuacha kukimbilia sehemu nyengine ambako kuna maslahi mazuri.

Nam. 30

Uwekaji wa Televisheni Wilayani

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza:-

Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ilianzisha utaratibu wa kuweka TV (*Screen*) kubwa kwenye Makao Makuu za kila Wilaya, Unguja na Pemba. Aidha, mradi huo pia ulipangiwa kuendelezwa sehemu zote za mikusanyiko ya watu wengi, kwa kuwekwa TV za aina hizo.

(a) Zile TV ambazo wizara ilizigawa kwa kila wilaya ziko wapi.

(b) Ile TV iliyokuwa imewekwa Malindi *"Show Room"* nayo iko wapi.

(c) Je, ule mpango wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo wa kutoa elimu kwa njia ya Televisheni kwa wale wasio na uwezo utafikiwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwepo hapa wazima wa afya kwa siku hii ya leo.

Sasa Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, *TV set* zilizopelekwa katika Afisi ya Mkuu wa Wilaya ziliondoshwa katika mamlaka ya Idara ya Televisheni Zanzibar na kukabidhiwa katika mamlaka ya Mkuu wa Wilaya husika moja kwa moja. Hivyo, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Idara ya Televisheni Zanzibar ilijitoa kabisa katika jukumu hilo la kubaki na televisheni hizo na sasa jukumu tulilokuwanalo ni la kurusha matangazo yake hewani tu.

(b) Mhe. Spika, *TV Set* iliyokuwa imewekwa Malindi ipo katika *Store* ya Idara ya Televisheni Zanzibar hapo *Karume House* na *TV Sets* nyengine kama hizo ambazo hivi sasa zimeshapitwa na wakati nyengine ni mbovu na hazifanyi kazi. Hivi karibuni katika mradi mpya wa kuhama kuanza kutoka kwenye *analogy* kwenda *digital*, utaratibu mzuri utafanywa wa kuziondosha televisheni hizo hapo *store*.

(c) Mhe. Spika, kutoa elimu kwa njia televisheni ndio lililokuwa lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea kuanzishwa kwa Televisheni Zanzibar. Hadi sasa lengo hilo bado lipo na linaendelezwa kwa kuoneshwa vipindi mbali mbali vya elimu ya afya, kilimo, sheria, wanawake, watoto, dini, mazingira na elimu yenyewe.

Pia, gari zetu za sinema nazo zimepangiwa kutoa taaluma za namna hiyo sehemu mbali mbali hususan vijijini kote hapa Unguja na Pemba. Hivi sasa kazi hiyo inaendelea kufanyika.

Mhe. Spika, elimu hiyo hutolewa katika mifumo mbali mbali ikiwemo pamoja na mijadala, michezo ya kuigiza, madarasa na hufukia wale wote wasiokuwa na uwezo kupitia gazi hizo tulizokuwanazo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, naomba ruhusa ya kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, *TV Sets* nilizozungumzia katika swali mama zilielezwa Wajumbe hapa ni kuwasaidia wananchi kupata taaluma mbali mbali pamoja na kujua matokeo ya kila siku ya shughuli za kimaendeleo. Lakini kwa bahati mbaya ndio zimeondoshwa ghafla na kuwekwa *store*. Je, huko *store* zitawasaidia vipi wananchi.

La pili kwa nini wananchi wasipewe taarifa kuwa televisheni hizo zinaondoshwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nadhani nilipojibu mara ya kwanza sikufahamika vizuri, nilisema televisheni

hizo zimewekwa *store* kwa sababu ni mbovu, zimeshapitwa na wakati na ni mbovu sio kama zimewekwa *store*, sasa zitaleta faida gani.

Pili, nimejibu pia katika swali la awali kwamba elimu huwafikia wote waliokuweko hata huko vijijini wale wasiokuwa na uwezo kutokana na gari mbili mpya ambazo zilipokelewa mwaka jana kutoka Shirika la *UNESCO* ambalo lenye majukumu pia ya kufikisha elimu kwa jamii. Sasa jukumu hilo tunafanya sisi pamoja na shirika hilo la Umoja wa Mataifa kufikisha elimu kokote kunakohusika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika viwanja vingi vya kimataifa hivi sasa duniani huwekwa televisheni kama hizo. Je, katika matengenezo ya kiwanja chetu cha Amani na hilo limekumbukwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba zile *display boards* pamoja na *score boards* za viwanja mbali mbali vya kimataifa ulimwenguni huwa na uwezo wa kuonesha mambo kama hayo.

Juzi usiku Mhe. Spika, tulifanya majaribio Uwanja wa Amani na nadhani watu wanaokaa karibu na maeneo ya Magogoni, Amani yenyewe na Sebleni watakuwa wameziona taa zile zilizowashwa usiku na tuliwasha taa hizo kwa kutumia jenereta kubwa ambalo limeletwa pale kwa madhumuni hayo hayo kwamba zikizimika taa mchezo uweze kuendelea, pasikatike mchezo wowote pale. Kwa hivyo, taa hizo ziliwashwa na zilipowashwa taa hizo na *score board* nayo pia iliwashwa pamoja na *display* .

Sasa tulichokiona ni kwamba ile *display board* pamoja na *score board* yetu tuliyokuwanayo ni digital, (ya mfumo wa kisasa) na ina uwezo wa kuonesha picha zinazokwenda pamoja na labda kama kushangilia kama kuonesha goli na vitu vingine. Kwa hivyo, inayo uwezo huo na tunaamini vyombo vyetu vyengine tutakavyokuwanavyo tukiweza kuunganisha na *score board* lile basi hizo picha zitaweza kuonekana. Ahsante.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kitu chochote cha jamii lazima kiwe na utaratibu maalumu. Naomba nijue. Je, TV hizi zilizopelekwa kwa ajili ya jamii hapo kabla hazijapelekwa kwa Mkuu wa Wilaya zilikuwa na utaratibu gani.

Pili, je, zilipopelekwa kwa Mkuu wa Wilaya alikabidhiwa na utaratibu huo.

Tatu, TV zile zikiharibika, nani atakayewajibika kuzitengeneza.

Nne, je, wizara ina mpango wa kutafuta TV nyengine mpya kumuongezea Mkuu wa Wilaya ili akaziweka katika sehemu mbalimbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, itaeleweka kwamba katika sheria ya Tawala za Mikoa pamoja na wilaya zale kuna Afisa kutoka kila wizara anakuwa *appointed* katika tawala hizo. Sasa katika wilaya pamoja na mikoa yote tuna maafisa wetu watatu kutoka katika wizara yetu, kuna afisa wa habari, afisa wa utamaduni na afisa wa michezo na hao sasa hivi wako chini ya mamlaka ya Mkuu wa Wilaya moja kwa moja, lakini ingawa ni watu wa wizara yetu na wao ndio wanaosimamia masuala yote hayo yanayohusiana na wizara yetu.

Sasa zile TV zilipokabidhiwa katika mamlaka za Wakuu wa Wilaya au Tawala za Mikoa, basi zilikabidhiwa kwa maandishi moja kwa moja na jukumu hilo likawa limebebwa moja kwa moja na wilaya husika pamoja na bajeti zake. Kwa hivyo, hilo jukumu sisi tulijivua na tuliondokana nalo na ndio maana sasa hivi bajeti yetu inazingatia kurusha matangazo hewani haizingatii tena kwenda kwenye jamii kupeleka TV na mambo mengineyo.

Isipokuwa kwenye hayo magari mawili yaliyoletwa mapya ya aina ya *Land Cruiser*, magari hayo huwa yanaonesha sio TV ni moja kwa moja kwa *display* kubwa, yaani kunakuwa na *screen* kubwa ambalo huwekwa pamoja na *projector* na lile gari lina jenereta lake na kila kitu chake pamoja na bajeti yake. Jukumu lile bado liko wizarani kwetu na ndio maana magari hayo tunayasimamia ili kufika maeneo ambayo hakuna umeme hilo la kwanza. Lakini pia na maeneo ambayo hakuna *TV reception* inayopatikana, yaani hawawezi kupokea matangazo ya TV.

Hivi sasa kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tayari umeme karibu umeshafika mote na sehemu zile ambazo ni kijijini kabisa basi sasa hivi wanazo televisheni kutokana na bei zake. Nilieleza juzi kwamba bei za televisheni sasa hivi zimekuwa nafuu na zipo kote mpaka kule Micheweni kwenye Redio yetu ya Jamii, tumeziona televisheni kadhaa mbuzi wanakolazwa juu kwenye ghorofa. Sasa hilo tayari limeshatatuliwa na utaratibu wa kisheria umefuatwa katika makabidhiano hayo ya jukumu la kutengeneza zitakapoharibika basi hilo linabakia kule kule wilayani Mhe. Spika.

Nam. 53

Ugawaji wa Kompyuta Skulini

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Katika Kikao cha Bajeti cha mwaka 2007/2008, Mhe. Waziri alipokuwa akitoa majumuisho ya Hotuba yake ya Bajeti, alitoa ahadi ya kuzipatia kompyuta skuli mbali mbali zikiwemo skuli za sekondari za Mwambe na Kiwani. Aidha, alikwenda mbali zaidi kwa kuwataka walimu kujifunza matumizi ya kompyuta pamoja na kutengeneza vyumba maalum kwa lengo la kuweka vifaa hivyo.

(a) Je, Mhe. Waziri bado unaikumbuka ahadi yako hiyo.

(b) Ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utafanyika.

(c) Iwapo nia ya kutoa mafunzo ya kompyuta kwa walimu bado ipo kwa nini visitumike vituo vya walimu (*TC*) kwa kutoa mafunzo hayo tena bure.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 53 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wakati Mhe. Waziri alipofanya majumuisho ya Hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2007/2008 alitoa ahadi ya kuzipatia kompyuta skuli mbali mbali zikiwemo Skuli za Sekondari za Mwambe na Kiwani. Pia, aliagiza skuli kutengeneza nyumba maalumu kwa ajili ya matumizi ya kompyuta na kuwahimiza walimu kujifunza matumizi ya vifaa hivyo vya kompyuta.

a) Ahadi hiyo Mhe. Waziri bado anaikumbuka.

b) Utekelezaji wa ahadi hiyo unaendelea hatua kwa hatua. Hadi hivi sasa skuli zilizopatiwa kompyuta ni pamoja na Skuli ya Sekondari ya Fukuchani, Kiembesamaki, Skuli ya Sekondari ya Biashara kwa upande wa Unguja na Skuli za Sekondari za Uweleni na Utaani kwa upande wa Pemba. Wizara itaendelea kuzipatia skuli nyengine kompyuta na vifaa hivyo kwa kadri ya uwezo wetu utakavyoruhusu.

c) Vituo vyote vya walimu hivi sasa vinatumika kuendeshea mafunzo ya kompyuta kwa walimu katika maeneo yao bila ya malipo yoyote. Hata hivyo, wizara iliandaa mafunzo makubwa juu ya matumizi ya kompyuta katika kilichokuwa Chuo cha Ufundi cha Karume kwa upande wa Unguja na *Adulti Education Centre*, Chake Chake Pemba.

Mhe. Spika, jumla ya Walimu Wakuu 25, walimu wa kawaida 50, Maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Mikoa watano (5), Maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Wilaya 10 na Wakuu 9 wa Vituo vya Walimu kwa ajili ya kuandaa wakufunzi watakaoendesha mafunzo ya kompyuta kupitia vituo vya walimu. Pia, Wakaguzi wa elimu wote walipatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa uadilifu wako, naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba vituo vyote vya walimu zipo kompyuta na mafunzo yanatolewa bure.

(a) Ningependa kujua kituo cha walimu Mzingani Pemba kina kompyuta ngapi na walimu wangapi hadi sasa wamefundishwa.

(b) Kwa kuwa ahadi ile iliongezwa zaidi kupaliliwa mbele ya macho ya wananchi, mbele ya Mhe. Rais alipokwenda kufungua jengo na kuagizwa walimu kwa kushirikiana na Mwakilishi wao kutengeneza chumba cha kuweka kompyuta na kwa kuwa vyumba viko katika Jimbo la Kiwani ni lini Waziri atanambia kompyuta angalau moja katika skuli yangu itapelekwa, ukizingatia hoja ile ilikuwa ni hoja ya mwakilishi mbele ya Baraza na Mhe. Waziri alisema mara tu baada ya bajeti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kipengele (a) kuhusu kituo cha walimu Mizingani kwamba kina kompyuta ngapi na walimu wangapi wamefundishwa hadi hivi sasa, sina takwimu sahihi hivi sasa lakini tutawasiliana na nitampatia takwimu hizo.

Mhe. Spika, jibu (b) nadhani nilijibu katika jibu langu mama kwamba, utekelezaji wa agizo hilo unaendelea hatua kwa hatua na pale tu mara uwezo utakapopatikana basi kompyuta hizo zitapelekwa kama tulivyofanya katika vituo vyengine.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kompyuta sasa imekuwa ni kama maji ya kunywa kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Je, ni lini wizara yake watatia katika mtaala wao somo la kompyuta kwa wanafunzi wa *primary* na *secondary* kama vile zinavyofanya skuli binafsi, ili watoto wetu nao waliyoko katika skuli za serikali wasione jambo hili ni geni watakapokumbana nalo katika maisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kwamba sasa hivi kompyuta imekuwa ni mazoea kwa wananchi wengi hapa visiwani na wengi wanatamani kuwa na kompyuta hizo na kujifunza mafunzo hayo ya kompyuta. Hata hivyo, napenda nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu inalifikiria wazo hilo na mara pale ambapo itafanya mchanganuo na kuweza kuona kwamba iko haja sasa hivi kufanya hivyo, basi itafanya hivyo kama alivyoomba.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Je, Mhe. Waziri anayo habari kuwa kuna skuli ambazo zimepata kompyuta bila ya kupewa na wizara.

(b) Kama anayo habari, skuli hizi amezisaidiaje kupata walimu wa kuwafundisha wanafunzi kuzitumia kompyuta hizi.

(c) Kuna mwalimu wa kigeni ambaye anajituma sana na huwa anakwenda katika skuli mbali mbali kufundisha matumizi ya kompyuta. Je, anaonaje Mhe. Waziri akamfanyia maarifa mwalimu huyu wa Skuli ya Uweleni akaweza kumpatia usafiri angalau wa chombo cha miguu miwili akawa anafikia kule anakokwenda akifundisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ninayo habari kwamba zipo skuli ambazo zimepata kompyuta bila ya kupewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hivi karibuni tu Mhe. Waziri wa Elimu alikuwa anakabidhi kompyuta katika Skuli ya Jang'ombe.

Lakini mimi mwenyewe binafsi nimeshuhudia Skuli ya Kiwengwa ikipewa kompyuta na *Vodacom* pamoja na skuli nyengine mbali mbali ambazo zimebahatika kupewa kompyuta.

Mhe. Spika, kuhusu kuwapatia walimu nadhani katika jibu langu mama nilisema kwamba kuna mafunzo maalumu ambayo tumeyafanya na tunaendelea kuyafanya kupitia vituo vyetu vya walimu, ili kuwasaidia walimu hao kwenda kuwasaidia kufundisha katika skuli zao. Lakini kuhusu mwalimu wa kigeni ambaye anafundisha Skuli ya Uweleni kupatiwa kipando japo cha miguu miwili, basi wizara itafikiria hivyo na italichukulia suala hilo kwa uzito unaofaa.

Nam. 34

Ukosefu wa Wafanyakazi Siku za Mapumziko Sehemu ya *CT Scan*

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Mashine ya uchunguzi wa maradhi *(CT Scan)* ni muhimu kwa utoaji wa huduma ya uhakika ya afya. Lakini huduma hiyo bado haijatumika ipasavyo kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja, wafanyakazi wake hukosekana kwenye kituo hicho katika baadhi ya siku hasa Sikukuu na siku za mapumziko.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa nini wafanyakazi wa sehemu hiyo wanakosekana katika siku hizo.

(b) Kwa nini usiwekwe utaratibu mzuri wa kuwepo wafanyakazi siku zote kwenye kitengo hicho kama ilivyo kwa kitengo cha *X-ray.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa siku za mapumziko wafanyakazi wa Kitengo cha *CT Scan* cha Hospitali ya Mnazi Mmoja huwa hawapo kazini kama vile siku za kawaida.

Mhe. Spika, wakati wa siku za Sikukuu na siku za mapumziko huduma hizo za *CT Scan* hutolewa kwa wale wagonjwa wa dharura kwani wafanyakazi wa kitengo hicho huitwa wakati wowote na kutoa huduma inapohitajika.

Aidha, Wizara yangu inafanya jitihada za kuwasomesha wafanyakazi wengi zaidi kadri inavyowezekana ili kukidhi kikamilifu mahitaji ya huduma hiyo ya *CT Scan.*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, serikali kwa kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma muhimu imetumia fedha nyingi ili kuepusha fedha zetu zisiende nje na zibakie hapa kwa manufaa ya wananchi wake kupata huduma hii. Lakini Mhe. Naibu Waziri katika jibu mama amesema kwamba wafanyakazi huwa wako *standby* wakati wowote wa dharura inapotokea hasa siku za mapumziko na nyenginezo.

Je, kwa kuwa mgonjwa kapelekwa katika chombo hichi kafanyiwa uchunguzi hii leo na hufikia siku mbili, tatu au wiki, wengine hata wiki mbili wanasumbuka hawapati majibu. Hili wamelichukulia hatua gani ili adha hii iondoke kwa wagonjwa wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, suala la kuchelewa kwa majibu ya picha linatokezea kutokana na kuwa na mtaalam mmoja tu pale Hospitali ya Mnazi Mmoja anayechunguza picha zile. Lakini inategemea uzito wa kesi ya mgonjwa wenyewe ilivyo. Kama mgonjwa tatizo lake ni zito, mtaalam wetu yule anachukua jitihada pamoja na kushirikiana na madaktari kuhakikisha kwamba picha ile iliyopigwa iweze kupatikana kwa haraka sana.

Jengine picha zilizokuwa zina matatizo ya kawaida, basi daktari huwa anaziangalia kwa utaratibu wake lakini hatimaye zote zinaweza kupatiwa majibu mazuri.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hivi wizara yake ina wataalam wangapi wazalendo wanaoweza kusoma na kutafsiri picha za *CT Scan* zilizochukuliwa kutoka kwa mgonjwa. Ikiwa haina wataalam, wizara yake imechukua jitihada gani ya kuwasomesha vijana wetu ili kutokutegemea wataalam kutoka nje.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza lazima nimfahamishe kwamba kuna wataalam wa aina mbili pale, kuna wataalam wanaopiga zile *film* za *CT Scan*, hawa wazalendo ni wawili, ni Ndugu Khamis na Ndugu Ali Khamis. Hawa tumewasomesha South Africa na Nairobi, sio kila mtu anapiga *film* zile hapana.

La pili, kuna msomaji wa zile *film* za *CT Scan*, hapa tunae Daktari Bingwa anaitwa Dk. Wang, huyu ni Mchina. Mzalendo wakati wowote atamaliza *University of Nairobi*, huyu anaitwa Dk. Salum Ismail. Kwa hivyo, baada ya muda mfupi mambo haya yote yatakaa vizuri na sawa.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri kuhusiana na kadhia hii. Mhe. Spika, ni kweli inavyosemekana kwamba kuna kuchelewa na hii tafsiri huwa inakwenda kufanywa Dar es Salaam. Sasa sijui kama hili lina ukweli au halina.

Lakini kwa sababu mengine yamejibiwa jibiwa katika maswali yangu (a) na (b), sasa nilikuwa nataka kujua kuna mkakati gani wa makusudi wa kupata wataalam hawa wa kutosha. Kwa sababu kadri ya Waziri alivyonyanyuka anasema kuna mtu mmoja tu.Kwa hiyo, bado inaonekana tatizo litakuwa pale pale.

Je, kuna utaratibu gani na mkakati gani wa makusudi angalau tuwe na watu. Kwa sababu binadamu Mhe. Spika, akiwa peke yake ni binadamu anaweza kupata dharura yoyote ikiwemo hata ya ugonjwa, kifo na kadhalika. Atakapokuwa huyu hayupo ana dharura, utaratibu gani umepangwa wa kuweza kuwa na watu ambao tukajua tumekamilika badala ya kuwa tunapata matatizo kwa wagonjwa wetu na inatubidi kusafiri.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kama nilivyosema mtaalam *Radiologist* huwa hapatikani kwa muda mfupi miaka mitatu. Huyu kijana wetu tumempeleka Nairobi hivi sasa anasoma na karibu mwaka huu huu atamaliza na akirudi atamsaidia huyu Daktari Bingwa wa China, Dk. Wang. Kwa hivyo, huu ndio utaratibu na hatua tulizokwishachukua. Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi atustahamilie kwa muda mfupi tu itakuwa pale tuna wataalamu wawili wa kusoma hizi *film*. Kwa hivi sasa bado tunaendelea kumtumia mtaalamu kutoka China.

Mhe. Spika: Nimepata taarifa kwamba hili swali Nam. 114 (c) liliingia kwa makosa. Kwa hiyo, kama Mhe. Waziri hakulijibu isiwe ni tatizo. Nilipewa taarifa mapema na watendaji halikuwemo katika maswali yake Mhe. Mjumbe.

Nam. 114

Athari ya Kukosa Umeme kwa Ukusanyaji wa Mapato

Mhe.Muhyddin Moh'd Muhyddin(Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi)- Aliuliza:-

Vyanzo vingi vya mapato ya Serikali vinategemea kuwepo kwa umeme wa uhakika na katika kipindi hiki huduma hiyo imekosekana katika kisiwa cha Unguja tangu tarehe 10 Novemba, 2009.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni kwa kiasi gani makusanyo ya mapato ya Serikali yameathirika kutokana na tatizo hili la umeme kisiwani Unguja.

(b) Kwa kuwa Kisiwa cha Pemba karibuni kitakuwa na umeme wa uhakika kupitia waya wa baharini kutoka Tanga. Je, serikali ina matayarisho gani kuhakikisha kuwa shughuli za ukusanyaji kodi na ushuru katika Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba zinaanzishwa tena baada ya kufa kwa zaidi ya miaka 30 sasa.

(c) Mradi wa umeme wa baharini katika kisiwa cha Pemba umegharimu fedha kiasi gani kwa thamani ya shilingi na kwa muda wa miaka mingapi mradi huu unatarajiwa kurejesha fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 114 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako swali (c) baada ya mashauriano na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi jawabu ninalo nitalijibu na kama kuna nyongeza tutasaidiana pamoja.

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba vyanzo vingi vya mapato ya serikali vinategemea kuwepo kwa umeme wa uhakika pamoja na harakati za uchumi ambazo hutegemea kuwepo kwa umeme.

Kukosekana kwa umeme katika kisiwa cha Unguja tokea tarehe 10 Disemba, 2009 kumeathiri kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato ya serikali hasa katika Sekta ya Utalii kutokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa sababu ya kutumia umeme mbadala wa majenereta kwa muda mrefu. Halikadhalika, Sekta ya Mawasiliano imeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na wananchi wengi kushindwa kutumia simu zao. Kwa mfano makusanyo ya mauzo ya Kampuni ya *Zantel* kwa mwezi wa Disemba yalifikia 6.7 bilioni na kuweza kulipa ada ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* Tsh. 465 milioni, makadirio ya mauzo kwa kipindi cha mwezi wa Januari yanategemewa kushuka hadi Tsh. 3 bilioni kutoka Tsh. 6.7 bilioni ambapo yatashusha ukusanyaji wa kiwango cha *VAT*.

Shirika la Umeme *(ZECO)* limetoa kodi ya *VAT* Tsh. 72 milioni kwa mwezi wa Novemba, 2009 na Tsh. 69 milioni kwa mwezi wa Disemba, 2009. Hata hivyo, kwa mwezi wa Januari hakuna matarajio

ya ukusanyaji wa *VAT* kutokana na athari ya kutokuwepo kwa huduma ya umeme. Aidha, Sekta ya Uzalishaji imeathirika kutokana na kufungwa au kupunguza uzalishaji kwa baadhi ya viwanda ambapo kumeathiri ukusanyaji wa mapato ya serikali hasa ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na Ushuru wa Bidhaa *(Exercise Duty).*

Mhe. Spika, halikadhalika, kufungwa au kupunguza uzalishaji viwanda hivi pia kumesababisha baadhi ya wananchi kukosa kazi. Hivyo, kupunguza uwezo wao wa kununua *(Purchasing Power)* ambapo pia kumepelekea kupunguza kwa ukusanyaji wa mapato. Vile vile, sekta ya Ujenzi nayo imeathirika kwa kiasi kikubwa ambayo huchangia katika mapato ya serikali. Nafikiri sote ni mashahidi tunaweza kuona viwanda vingapi vya kufyatulia matofali vimelala kwa muda huu.

Hata hivyo, kwa sasa ni mapema mno kuweza kujua kiasi halisi cha makusanyo ya mapato ya serikali kitakachopungua kutokana na hali hiyo, ingawa makadirio ya mwanzo yanaonesha kwamba serikali itapoteza kiasi cha asilimia thalathini (30%) ya makusanyo ya mapato ilichokadiria kukikusanya katika kipindi chote kitakachokosekana huduma hii muhimu katika kisiwa cha Unguja.

(b) Mhe. Spika, kupatikana kwa umeme wa uhakika hivi karibuni katika kisiwa cha Pemba kutasaidia kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya serikali kutakakosababishwa na kuongezeka kwa Vitega Uchumi na Biashara mbali mbali katika Kisiwa hicho. Kutokana na hayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia taasisi zake za ukusanyaji wa mapato tayari zimeshajipanga vizuri kuhakikisha ya kwamba kodi halisi za serikali zinaendelea kukusanywa kwa faida ya nchi na wananchi wake kwa jumla.

Shughuli za ukusanyaji kodi na ushuru katika Kiwanja cha Ndege cha Karume, Pemba zimekuwa zikiendelea bila kusita pamoja na kuwepo idadi ndogo ya ndege zinazoanzia safari na zinazotua katika kisiwa hicho na hazijawahi kusitishwa.

Kwa mfano mwaka 2006/2007 makadirio ya makusanyo yalikuwa ni Tsh. 65 milioni ambapo Tsh. 83 milioni zilikusanywa sawa na asilimia 127 ya makadirio, mwaka 2007/2008 Ths. 86 milioni zilipangwa kukusanywa ambapo Tsh. 76.4 zilikusanywa sawa na asilimia 89 ya makadirio. Aidha mwaka 2008/2009, Tsh. 92 milioni zilipangwa kukusanywa ambapo Tsh. 81.4 milioni zilikusanywa sawa na asilimia 81.4 ya makadirio.

Mhe. Spika, nataka kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa makusanyo ya Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba sio kwamba yatakuja baada ya kuwepo umeme, tayari yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia taasisi za ukusanyaji wa mapato zitahakikisha ya kwamba wageni wote wanaoanzia safari zao katika kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba wanaendelea kulipa kodi na ada mbali mbali kwa mujibu wa sheria.

(c) Gharama za mradi wa kupeleka umeme Pemba zinatarajiwa kuwa shilingi 75 bilioni sawa na Norwagian Kronner 390 milioni. Mradi unatarajiwa kurejesha pesa hizo baada ya miaka 30.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo hufa kutokana na kutokufanyiwa tathmini mwanzo na kwa kuwa wananchi wa Pemba wameshakuwa na tegemeo la umeme wa uhakika. Je, Mhe. Waziri, umeme huu utachukua muda wa miaka mingapi kudumu kisiwani Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba nimhakikishie kwamba mradi wowote ni vyema ukafanyiwa tathmini na hasa tathmini ya matumizi na mapato, unatarajiwa kupata fedha ngapi na lini utaanza kujilipa. Mradi wowote kama hauna vigezo hivyo basi kwa kweli haukutimia na hata kama utaupeleka *ZIPA* basi utakataliwa, lazima viingie vitu kama hivyo.

Kwa muda unaotarajiwa kuishi huu umeme wetu ningeomba Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi anisaidie kujibu swali hilo.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kuna mambo mawili, kuna ubora wa miundombinu na maandalizi ya miundombinu yenyewe na makadirio ya matumizi kama alivyosema Mhe. Waziri, mapato na hatimaye makadirio ya matumizi ya mahitaji ya wananchi. Mkonge huu unaosafirisha umeme kutoka Tanga kuja Pemba umekadiriwa kuwa na maisha ya miaka 30. Ubora wa matumizi yake utaongeza miaka kadhaa juu ya hivyo, lakini tunategemea ndani ya hiyo miaka 30 na ziada kuwa na mikakati ya maandalizi mengine ya mahitaji. Hivi sasa tunatumia *megawatt* 4.5, uwezo wa waya huu ni *megawatt* 20.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba unatoa huduma asubuhi mpaka jioni hautoi huduma usiku. Huoni hiyo ni sababu moja ya kupunguza mapato.

Swali (b) kwa kuwa sasa hivi umeme wa uhakika kisiwani Pemba unakaribia kuanza kazi. Je, taa za kiwanja kile zitatengenezwa lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa *size* ya kiwanja cha ndege cha Pemba, ndege nyingi inazoruhusu kutua kwa sasa ni zile ndogo ndogo mpaka labda tuseme abiria 18, hivi vi-*charter* vidogo vidogo, *Coastal, Zanair*.

Siku moja niliwauliza hata Unguja hapa kwa nini hamtui usiku? Wenyewe wakanambia kiutaratibu wetu hata Dar es Salaam hatu-*operate* usiku kwa sababu hizi ndege zimetengenezwa wanasema *emergency*, hata kiwanja cha mpira ziwezekutua. Sasa wanaona ni *risk* kwenda usiku. Kwa hiyo, si kwa Pemba tu lakini hata Dar es Salaam, hata Unguja hazitembei kwa kweli usiku.

Lakini suala la umeme kwa kiwanja cha Pemba tayari hilo serikali inalifanyia kazi kwa wafadhili wetu hawa wa *Saudi Fund* kuna pesa ilibaki ya bakaa pale, tayari tumeshaiomba tunaifanyia kazi. Kwa hiyo, tunaamini matengenezo yajayo yatajumuisha *runaway* pamoja na jengo lile hasa kuzikarabati au kuziweka taa za umeme Pemba. Hilo tunalifanyia kazi kwa kupitia msaada kutoka *Saudi Fund*.

Nam. 33

Uharibifu wa Msitu wa Kiwengwa/Pongwe

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Msitu wa Kiwengwa/Pongwe umehifadhiwa ili kuyalinda mazingira. Kwa kuwa msitu wa Kiwengwa/Pongwe hivi sasa umeharibiwa vibaya na baadhi ya watu ambao huvamia msitu huo kutoka nje ya maeneo hayo.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako imeweka mkakati gani kunusuru msitu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu imechukua hatua ya kuimarisha ulinzi kwa kutumia wafanyakazi wa wizara pamoja na kushirikiana na Kamati za Uhifadhi, kusaidia wanajamii kuanzisha mashamba yao ya miti ili waweze kutumia kwa mahitaji yao mengine kwa kuuza na kujipatia kipato, kuelimisha jamii kwa shehia zote zinazozunguka msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa/Pongwe ili kuelewa taathira na umuhimu wa uhifadhi wa msitu huo hasa kwa vile ndio msitu pekee uliobaki katika upande wa Kaskazi wa Kisiwa cha Unguja. Wizara yangu imeshajiisha jamii inayozunguka msitu huo.

Hivyo, imeweza kuanzisha Kamati za Uhifadhi ili kuweza kusaidia Usimamizi na Uhifadhi wa msitu huo. Vile vile wizara imekuwa ikishajiisha na kuwasaidia wanajamii hao kubuni miradi mbadala ili kuondokana na utegemezi wa rasilimali zinazotokana na msitu wa Kiwengwa/Pongwe.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kitope kwa kazi yake kubwa mbali ya kuanzisha ile Kamati ya Mazingira, lakini pia na yeye mwenyewe kushiriki katika kuhakikisha kwamba msitu huu wa Kiwengwa unabakia katika hali yake ya kawaida.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe.Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, msitu huu wa Kiwengwa/Pongwe ni msitu ambao uhai wake ulikuwa ni msitu mzuri na unatisha kuingia katika sehemu za ndani, hasa ukizingatia kwamba ukiingia sehemu moja huwezi kutokea sehemu ya pili bila ya kuwa mwenyeji katika maeneo hayo kutokana na msitu ulivyoshikamana.

Lakini sasa hivi Mhe. Spika, nakuthibitishia tu kwamba hali halisi iliyojitokeza kwa mandhari ya nje utauona msitu ule uko vile vile, lakini ukiingia mita 20 toa 30 msitu ule umekuwa kama uwanja wa mpira.

Je, Mhe. Waziri, pamoja na hayo niliyoeleza na kuweka ulinzi ambao anasema uko imara. Atanieleza vipi wakati Kituo cha Misitu kipo Kituo cha Polisi Kiwengwa na njia za mikato ziko kilima cha Mchekeni ambapo wanapita pale kwa walinzi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na yeye juu ya maelezo ambayo ameyatoa kwamba msitu ule umekuwa kama uwanja wa mpira, ukiuona huku nje kweli unauona ni msitu, lakini ukiingia ndani nakubaliana na yeye sio kwamba ni uwanja wa mpira tu, lakini ni maeneo ambayo yamejengwa kama maeneo maalumu kwa ajili ya starehe.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kwa sababu huu msitu haukuzunguka eneo lile ambalo nilimtaja Mhe. Makame Mshimba Mbarouk peke yake, ni Shehia nyingi tu zikiwemo Matemwe na sehemu nyengine. Kwa hivyo, tunawaomba viongozi wote Waheshimiwa Wawakilishi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, tushirikiane ili tuweze kuhakikisha kwamba msitu wetu huu tunaulinda kwanza ukiwa ni rasilimali pekee. Lakini pia lengo lake kubwa serikali ni kuhakikisha kwamba unatoa tija au kusaidia uchumi wetu wa Zanzibar.

Lakini jengine pia la ziada, ni kama tulivyosema sisi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira sasa hivi tumefanya jitihada za ziada kuhakikisha kwamba wale waliouzunguka ule msitu tunawapatia masuala mengine ya mbadala ili waachane na kukata msitu ule kwa njia ya biashara.

Miongoni mwa mambo ambayo tumejiandaa na ambayo tumeshatumia jumla ya shilingi milioni 4.8 ni kuhakikisha kwamba tumeanzisha vilimo vya mboga mboga maeneo mbali mbali yakiwemo Bambi na sehemu nyengine. Lakini pia tumeanzisha kuku wa kienyeji katika maeneo mengine, pia tumeanzisha masuala ya kufuga nyuki, ili wale watu ambao wana kasi ya kwenda kuuvuna ule msitu kwa ajili ya kujipatia fedha waweze kufanya kazi nyengine na msitu wetu uweze kurejea.

Lakini jengine pia tumehakikisha kwamba tunapata mashamba ya watu binafsi ili waweze kutumia kwa ajili ya kupata kuni na mambo mengine.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tukiangalia hali halisi misitu yote imetoweka mbali ya hiyo ambayo imezungumzwa. Kule Hanyegwa Mchana tulikuwa na msitu mzuri tu hivi sasa haupo, hata hapo Jozani nao umebakia njiani tu ukiingia ndani hamna kitu.

Je, Mhe. Waziri, amelipokea vipi agizo lile la "Kata Mti Panda Mti" ili kuendeleza hii misitu yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nataka niseme kwamba sio nimelipokea vipi, isipokuwa niseme tumelipokea vipi. Mhe. Spika, kama nilivyorejea mwanzo, nasema suala la kukata miti na kupanda miti sana sisi tunahimiza upandaji wa miti, hatuhimizi ukataji wa miti kwa sababu miti inakatwa kwa dharura maalumu. Kwa mfano hatuwezi kuzuia pahala panataka kupita barabara au ujenzi wa skuli lazima miti itakatwa. Lakini huu ukataji wa miti kiholela nasema tulipokee sote Baraza zima na viongozi wengine walio nje, shehia na wananchi ili kuhakikisha kwamba tunapanda miti.

Mhe. Spika, wizara yangu imeweka Siku Maalumu ya Kitaifa ya Upandaji Miti hapa Zanzibar. Kwa sisi kama Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka mmoja tunazalisha zaidi ya miti laki tatu na kidogo kwa ajili ya kuwagaia wananchi bure ili kuendeleza upandaji wa miti hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, katika miezi mitatu au minne iliyopita misitu yetu mingi iliingia moto, utafiti tulioufanya waliokuwa wakienda kutafuta asali wanatumia moto, halafu wanashindwa kuuzima, moto unakwenda na hasara kubwa inapatikana. Kwa kuwa Zimamoto walitoa ushauri kwamba vichimbwe visima, ujengwe mnara ili kuweza kubaini moto haraka na kutengeneza njia ndogo ndogo. Kwa kuwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa imeshapeleka mapendekezo hayo katika wizara. Je? lini wizara itachukua hatua ya kuyafanya yale ili kunusuru athari isiwe kubwa, yaani Jozani karibu hekta 60 zimeungua hivi karibuni.

Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane na yeye kwa maelezo mazuri aliyoyatoa, lakini naomba niongezee moja. Mbali ya suala la uvunaji wa asali, pia kuna suala la uvutaji wa sigara ambao wako wengi katika maeneo kama hayo. Pia, nayo tunaigundua ni tatizo ambalo linaweza kujitokeza, mtu anaweza kuvuta sigara na baadae akakitupa kile kipisi cha sigara na moto ukashika na kuwaka.

Pia, kuna suala la tatu ambalo ndio kama tunavyosema mwizi mara nyingi hana zambi. Tunakuwa tunatia wasi wasi kuwa kuna watu wengine wanaitia moto misitu yetu kwa makusudi, yaani watu ambao sio waadilifu. Suala la kwamba tayari tumesaidiwa maelekezo na wenzetu hawa wa Zimamoto kuwa tuhakikishe kwamba tunafanya njia mbadala.

Njia ya kwanza ambayo kwetu sisi ni wajibu wetu wa kuhakikisha katika hiyo misitu yetu kuna kuwa na njia. Suala hili tangu zamani tunalifanya, tunaziita njia za moto, ili moto ukiingia katika kipande kimoja basi usiweze kwenda katika kipande cha pili. Lakini suala hili la kwamba wizara ni lini itatoa hizo fedha kwa ajili ya mambo mengine, suala hili naomba labda nimuachie Mhe. Waziri wangu anisaidie kidogo hapa kuwa ni lini tutaweza kuzipata hizo fedha na tutazitowa wapi?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mjumbe, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri.

Kwa ufupi ni kwamba suala hili ni kweli pendekezo hili limetolewa na wizara imelipokea na limo kulifanyia kazi, kwa sababu linahusika na gharama ambazo hazimo katika bajeti. Lakini wizara inafanya mipango ikiwezekana kuweza kuziomba fedha hizi, au ikiwezekana kutumia na mradi katika jumla ya miradi yetu kuweza kupata fedha zaidi za kutengeneza njia na ujenzi wa visima na minara.

HOJA ZA SERIKALI

Sera ya Nishati Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kupata nafasi ya kwanza katika kuchangia sera hii ya nishati. Kwanza namshukuru Allah kwa kutuweka hai na wazima na kwa kutupa nafuu ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, ni jambo lililokuwa halina mjadala kwamba sera ya nishati ni muhimu, na ina umuhimu wa aina yake. Mbali ya kwamba imeletwa katika Baraza kwa wakati huu, lakini imekuja katika wakati ambao jamii kubwa ya Wazanzibari ina dhiki kubwa kutokana na neno hilo nishati kukosekana.

Kwa hivyo, kila mmoja atakayelisikia atakuwa analijua umuhimu wake, kwa sababu jambo ukiwa unalipata si rahisi kulijua umuhimu wake mpaka siku ile utakapolikosa ndipo utakapolijua umuhimu wa lile jambo ambalo ulikuwa ukiendelea kulipata.

Pili, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuweza kwa muda mfupi kutengeneza sera ambayo imekwenda kwa undani kabisa karibu miaka mia ijayo labda. Lakini Mhe. Spika, ……

Mhe. Spika: Hivi Mhe. Waziri yuko wapi? Naibu Waziri pia na Kaimu sijui kama yupo? Tunataka kujua nani anachukua maelezo?. Kwa kawaida Waziri ndiye anayehusika au Kaimu Waziri. Halafu Waziri alikuwepo muda mfupi tu imekuaje mambo haya.

(waziri karudi)

Mhe. Waziri, tulitaka kuahirisha Baraza maana ulikuwa hupo mwenyewe. Una maelezo.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nikutake radhi, bahati mbaya niliingia msalani, kwa maana kujitayarisha kukaa kitako kwa hadi utakapoahirisha. Lakini kwa heshima kubwa nakutaka wewe radhi na Waheshimiwa Wajumbe, nilikuwa hapa, kumradhi sana.

Mhe. Spika: Tunamridhia. Mhe. Rashid Seif, sasa endelea.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, hasa kwa kumsamehe Mhe. Waziri wetu.

Mhe. Spika, nasema kwamba sera hii ina umuhimu wa aina yake sasa hivi kwa sababu jamii kubwa ya watu wameendelea kukosa nishati muhimu ya umeme. Sasa kwa sababu wamekosa ile thamani ya kile kitu inapoonekana. Kwa kuwa hii sera ni kubwa, mimi naomba nichukuwe vipengele viwili tu katika kuijadili hii sera, vipengele vyengine nitawaachia wenzangu waendelee navyo.

Mhe. Spika, katika mapitio yangu ya mjadala wa sera pahala pamoja niliona kwamba sera inatakiwa itowe vielelezo vya maelezo halisi au hali halisi ilivyo, ama mahitaji yanayohitajika au matatizo yaliopo. Hilo ndio jambo la mwanzo ambalo linatakiwa sera itowe. Kutokana na maelezo yaliyoelezwa katika kurasa mbali mbali za utangulizi wa hii sera, mimi nilidondoa mambo yafuatayo na baadae nitataja zipi zilizokuwa katika haya zimeshughulikiwa katika hii sera na yapi hayakushughulikiwa katika hii sera.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 9 wa utangulizi iliekwa asilimia ya matumizi ya nishati kwa Zanzibar. Mhe. Spika, mimi nilitoa mambo matatu, kuni asilimia 54, mkaa asilimia 25, kwa pamoja kuni na mkaa unatoa asilimia 79 ya matumizi ya nishati kwa Zanzibar. Hii si chochote bali ni miti. Kwa hivyo, tuangalie kuwa ikiwa Zanzibar inatumia asilimia 79 ya nishati yake kama ni kuni na mkaa, basi tuone ni kiasi gani miti inavyokwenda kwa ajili ya matumizi ya nishati. Umeme unatumia asilimia 4 tu ya nishati yote inayotumika Zanzibar

Mhe. Spika, mimi nimeli-*classify* kwamba hili ni tatizo kwanza la kimazingira na pili pana tatizo la ufanisi katika matumizi ya nishati. Sasa naomba nikiri kwamba kwa kiwango kikubwa sera imeweza kuelekeza matumizi ya nishati mbadala. Lakini ningependa kuchangia kitu kimoja, kwamba katika sera ingekuwa vizuri zaidi ingeeleza ni kwa kiasi gani na kwa muda gani tutaondokana na asilimia 79 ya kuiondoa miti yetu kuelekea katika nishati ya gesi au umeme. Kwa hivyo, ni baada ya miaka mingapi tutai- *revise* hii *trend* kuelekea kwamba sasa tunatumia asilimia 4 ya misitu yetu kwa nishati, lakini tunatumia asilimia 79 kwa umeme na gesi kwa ajili ya nishati. Hili ni jambo muhimu sana kulielekeza.

Mhe. Spika, baada ya hapo nakuja katika tatizo la pili. Katika ukurasa wa 9 na wa 10 wa sera, kuna sentensi hapa imeandikwa hivi.

Ukurasa wa 9 na 10

> " Mahitaji ya umeme Unguja na Pemba ni makubwa kuliko ugavi uliopo"

Sasa hili ni tatizo vile vile, kwamba umeme tuliokuwanao hautoshelezi mahitaji. Sasa tuangalie katika sera imetuelekeza vipi na tutafikia vipi katika suala hili la umeme kuweza kujitosheleza au kutosheleza mahitaji.

Mhe. Spika, kwa kiwango fulani sera imelizungumza suala hili, lakini tatizo lipo katika vifungu hivi vifuatavyo; Kweli tunaagiza waya wa *megawatt* 20 kutoka Tanga kwenda Pemba imeshafungwa sasa hivi, badala ya *megawatt* 4.5 ya umeme uliokuwa *maximum* kwa Pemba, sasa tutapata megawatt 20. Unguja kutoka megawatt 50 kuelekea 100, lakini Mhe. Spika, katika sera hii hii kwenye ukurasa wa 10 umeeleza hivi.

Kwa wastani watumiaji 80,000 wamesajiliwa na Shirika la Umeme hadi sasa, lakini sentensi hiyo haikulinganisha 80,000 hao kati ya wangapi. Kwa sababu tukitizama ikiwa watumiaji ni 80,000 ndani yake humo muna mahoteli, maskuli, mahospitali ya serikali na binafsi na mambo chungu nzima pamoja na hayo majumba ya watu binafsi. Kwa hivyo, tatizo hasa hatukulijua liko wapi?

Mhe. Spika, hapa nilipo ninayoripoti ya *House hold Budget Survey (HBS).* Katika kitabu hiki cha *House hold Budget Survey* kinaeleza hivi, na hii ilifanywa mwaka 2004/2005 "Asilimia za kaya zilizounganishwa umeme, Kaskazini A asilimia 4.1, Kaskazini B asilimia 7.9, Kati asilimia 6.5, Kusini asilimia 19.5, Magharibi asilimia 34.1, Mjini asilimia 67.6, Wete asilimia 11.9, Micheweni asilimia 2.4, Chake Chake asilimia 19.2, na Mkoani asilimia 6.2. Kwa ujumla ni asilimia 25. 2, kwa maana hiyo ni robo tu ya Wazanzibari ndio wanaotumia umeme uliounganishwa katika kipindi hicho. Sasa hili ni tatizo, ni lazima hii sera ingeelekeza tutafikia wapi kuongeza asilimia ya watu, iwe kila baada ya mwaka tunaongeza asilimia ya Wazanzibari kutumia umeme.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilivunjika moyo kidogo na baada ya maneno yaliomo katika sera, sikulifahamu labda hili neno. Katika ukurasa huu huu wa 10 nafikiri. Kinasema hivi sasa umeme ni fursa inayopatikana kwa watu wengi wa Unguja na Pemba. Sasa hivi tumefikia katika kiwango cha kuambiwa umeme ni lazima, lakini bado sisi kwetu ni fursa. Vile vile, *House hold Budget Survey* inasema ni asilimia 25, sentensi inasema ni watu wengi. Kwa hivyo, tumechukua ipi, pengine tumechukua asilimia ya mjini tu, ambayo imefikia

asilimia 67.6. Kwa hivyo, kidogo hapa tunataka kupate mwelekeo kidogo, sera inatupeleka wapi kwamba watu wetu waweze kupata umeme kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, binafsi yangu nilizungumza katika bajeti iliyopita kwamba tatizo moja ni bei ya kuunga umeme ni kubwa mno. Bei inawezekana ikawa haikupunguzwa kwa sababu bei inatokana na vifaa na vifaa vinanunuliwa na pengine serikali haina uwezo wa kuongeza tone katika uungaji umeme, lakini masharti. Kwa sababu mwananchi anayekwenda akaambiwa unaungiwa umeme kwa laki nne au laki tano alipe asilimia 66, si rahisi kwa mwananchi yule. Lakini tungemuanzia angalau asilimia 10 au 20 halafu baadae ndio akalipa ndani ya *bill* zake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi naomba jambo hili lizingatiwe sana, kutatua matatizo ya muda mfupi, kwa sababu mimi nakubaliana sana na sera hii kwamba imekwenda kuzingatia matatizo ya muda mrefu ya nishati. Ukisoma utaona hasa kuwa imezingatia matatizo ya muda mrefu ya nishati kwa Zanzibar. Lakini matatizo ya muda mfupi bado yapo kwamba wananchi wengi hawamudu kuunga umeme. Kwa hivyo, hata hizo njia ambazo tunazitaja sisi zitakuja kutuona kwamba tunao umeme mwingi na watu wetu bado hawana umeme majumbani. Kwa hivyo, mimi ningependa kwamba katika kipengele kilichotajwa cha ufanisi wa Shirika la Umeme. Kipo kipengele kwenye hoja ya 7 kinachosema, Ubora na maendeleo ya Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, hapa lingepewa jukumu maalum katika sera kuhakikisha kwamba Shirika la Umeme linaongeza kila mwaka asilimia ya watu wanaounga umeme kwa Zanzibar. Sasa wao watafanya njia zao, jukumu wamepewa katika sera kwamba Shirika la Umeme lihakikishe kwamba linaongeza wateja wake kila mwaka. Namna gani watafanya, hiyo ndio kazi yao ya mikakati. Lakini sera ielekeze kwamba Shirika la Umeme lihakikishe kwamba linaongeza wateja wake kila mwaka na ikifikia mwaka 2020 tuhakikishe asilimia 80 badala ya 25 kwamba watu wetu wa Zanzibar wanao umeme wa ndani. Kwa hivyo, mimi naomba hili lizingatiwe.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo lina muda mfupi na sera kidogo haikulizungumza kwa kina ni suala zima la uimarishaji wa Shirika la Umeme kimapato, bado ni shirika linaloendeshwa, wanasema kwa msaada sana kutoka NOREMCO na mengineyo na kuna matatizo ya udhibiti wa mapato. Kwa hivyo, sera ielekeze kwamba Shirika la Umeme liweze kujiendesha itakapofika tarehe fulani na kudhibiti mapato. Sasa wao watafanya nini, ndio mikakati inakuja hiyo au *work plan*. Lakini sera ielekeze, haiwezekani tuwe na Shirika la Umeme ambalo kila siku linasaidiwa wakati wananchi wanalipa, kutokana na kufungwa hizi mita za TUKUZA, ile mivujo ya malipo kutoka kwa wananchi

inazidi kupungua. Sasa hatujui masahihisho yaliyofanywa kwenye mashine huko, isijekuwa wananchi wanalipa lakini zinavujia katika michirizi mingine. Kwa hivyo, ni kazi ya shirika sasa kujiimarisha na kuweza kujitegemea, sera ielekeze hivyo.

Mhe. Spika, kwa nini nikaligusia Shirika la Umeme sana, kwa sababu kadri itakavyofanywa kushughulikia mambo ya umeme mbadala, mwisho kwa sababu tumeuchaguza kwamba ndio shirika *monopoly* mwisho utawakabidhi wao. Hata ukiwa na nishati ya upepo, nishati ya jua au nishati ya mawimbi *ultimately* ukishaishughulikia wewe utawakabidhi wao. Sasa ikiwa shirika hili halijiwezi watakabishiwa kitu gani. Kwa hivyo, lazima kuwe na *establishment* nzuri ya hili shirika, kwa sababu hii nishati tutakapoishughulikia mwisho itakwenda kwao, sasa kama hili shirika halijiwezi kudhibiti mapato yao hata tukiwakabidhi kitu gani kitakuwa hakiwasaidii wananchi.

Kwa hivyo, moja katika *primary goal* ya hii sera ya muda mfupi ni kuliimarisha Shirika la Umeme ili liweze kuwa na watendaji bora, liweze kuwa na ufanisi, liweze kuwa wazi katika shughuli za mapato. Wakati mwingi hapa tunaambiwa umeme haulipi, kuna *subsidy* zinazotolewa. Lakini tunauliza ni mahesabu gani yaliyofanywa hata kuwe kuna *subsidy* haulipi kwa njia gani. Njia moja ilijulikana kwamba yalikuwa yakivuja mapato watu hawalipi.

Sasa shirika walituambia hapa kwamba ifikapo 2012, TUKUZA itakuwa imeenea, sasa kutakuwa na njia gani tena ya kuwa mapato yavuje wakati wao wameshafunga mitambo yao. Isipokuwa ile mitambo itaingiliwa na mapato yatavuja kwa njia nyengine. Kwa hivyo, ni lazima shirika hili liweze kuimarishwa tokea hapa mwanzo ili liweze kuwa na watendaji wazuri, kwa sababu hata nishati mbadala ambayo kwa bahati nzuri nashukuru na ninaipongeza wizara kwa kuzungumza sana kuhusu nishati mbadala itakuwa haileti faida ikiwa shirika lenyewe linalokabidhiwa halina mwelekeo.

Mhe. Spika, baada ya kulizungumza hilo suala la umeme tegemezi ambalo ndio tatizo jengine tulilokuwa nalo, nashukuru pia limezungumzwa kwa uwazi. Isipokuwa sera wakati mwingi inahitaji fedha nyingi ili kuitekeleza. Hii sera ni kubwa na ninamshukuru Mhe. Waziri katika hotuba yake, alikuwa anagusia kuhusu mazungumzo yao na mashirika na nchi mbali mbali katika kuhakikisha kwamba wanapata *fund* ya kuweza kuisukuma hii sera, ni jambo muhimu, wakati tunakwenda na sera tusione kwamba sera hii hatuiwezi peke yetu, ni lazima tupate wasaidizi wa kutusukuma.

Mhe. Spika, tuje katika suala letu la uingizaji wa bidhaa za mafuta, hivi sasa hali tuliyonayo na mwelekeo wa baadae. Ilidhihirika wazi wazi jana hapa katika baadhi ya maswali kwamba suala hili lina maeneo mengi

yanayoshughulikia, wengine watoa leseni, wengine wanapima, wengine wanachukua mapato. Suala la *synchronization* ya uagiziaji na uingizaji wa mafuta ni suala muhimu sana kuondoa mianya hii inayojitokeza. Ubora wa mafuta umezungumzwa hapa, inatakiwa *responsible* kama hii ni wizara ya nishati inatakiwa ibebe jukumu lote. Kufuta leseni, kupima viwango, kupasisha na kufelisha kila kitu.

Kwa mfano ukenda kwenye afisi Mhe. Spika, unaweza ukamaliza shughuli zote lakini anayepokea pesa ni mtu mmoja tu, hilo sio tatizo, lakini zile *procedure* zimeshakwenda. Sasa duara lile la kupokea pesa sio tatizo. Kwa hivyo, kama ZRB ndio tunawaweka kuwa ndio kituo cha kupokea pesa, basi wasiwe na *over roll say* katika suala la nishati, kazi yao ni kuwa wameshapata ruhusa kwamba huyu kweli kaleta lita milioni moja, mafuta yao tumeshayatizama ni sawa sawa, yana kiwango kinachotakiwa. Kwa hivyo, tunawaleta kwenu kwa kulipa malipo. Lakini wizara ya nishati ni lazima ipewe *holybusiness* ya mafuta yanayoingia hapa, hakuna njia nyengine ya kumuweka huyu na kumuweka huyu. Kwa sababu wao ndio tutakaowauliza kwa nini mafuta hayajaja.

Mliona jana tulivyokuwa tukipata tabu, mara tunamuuliza Waziri wa Fedha na Uchumi, mara Waziri Maji, Ujenzi, Nishati na Mazingira anasema hivi na Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi anasema Mkurugenzi wa vipimo yupo. Lakini Mkurugenzi wa vipimo yupo wizara nyengine na mafuta yako wizara nyengine. Kwa kutumia sera hii lazima tuamuwe kwamba mafuta yanapoingizwa yawe chini ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Suala la kulipa *cash* au *check* ZRB ni suala moja dogo ambalo *procedure* yote imeshamaliza.

Mhe. Spika, imezungumzwa katika sera hii kwamba kuna sera nyingi ambazo ni *conjunction* na hii. Kwa hivyo, mimi ningeomba kwamba baada ya sera hii, wale ambao walitajwa kuwa sera zao haziku-*mention* na hazikutaja nishati wakawa *responsible*, yaani wakazipitia sera zao zikenda sambamba. Kwa mfano Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inayo misitu pamoja na mazingira. Lakini hizi kwa bahati nzuri mazingira yako kwenye wizara hii, sasa vitengo viwili hivi vya misitu na mazingira ikaangalia sera zake, je, zinalingana na Sera ya Nishati na wakenda sambamba na hawa?

Kwa sababu Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi akiamua kupandisha bei ya umeme hapandishi bei ya umeme tu, anamwambia na mwenye *cooker* usipikie *cooker* na badala yake akachukue kuni au makaa.

Sasa na yeye mtu wa mazingira pamoja na misitu atakapotunga sera yake, basi ataje mle kwamba wakati wa kupitishwa bei za umeme na wao washirikishwe, kwa ajili ya kuona kwamba *genuine* au si-*genuine*. Pengine Waziri amepungukiwa na fedha na kuona umeme upandishwe au jamaa wamevujisha

na shilingi milioni 200 zimepotea, anaona loo! Pengo hili tutalifanya nini sisi, isipokuwa ni kupandisha kidogo.

Lakini kupandishwa kwa bei ya umeme kumeathiri kiasi kikubwa kama vile wale wenye *cookers* hawapikii tena *cookers*. Kwa hivyo, umeme utashuka wakati huo huo na kuni zitateketea, makaa pamoja na miti kwa jumla. Kwa maana hiyo, sera ni vyema kwenda sambamba.

Suala jengine ambalo nataka nilizungumze ambalo limezungumzwa kwenye sera kuhusu muda mfupi, wakati na mrefu. Mhe. Spika, angalau ungekuwa *mentioned* tukapata. Kwa hiyo, *point* nitakayoitaja baadaye kujua muda mfupi ni upi, miaka mitano mpaka kumi, muda wakati ni upi? Miaka 20 mpaka 25, pamoja na ule muda mrefu ni upi?

Kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu moja katika kitu ambacho kimesisitizwa sana katika upangaji wa sera ni tathmini, kwa lugha ya kigeni tunasema *evaluation*. Mhe. Spika, katika kufanya tathmini ya sera lazima ujue huu muda mfupi tunaokusudia ni muda gani? Kwa hiyo, tunajua malengo yetu ya muda mfupi, je, yamefikiwa? Kwa maana hiyo, *atleast* kuwe na *mention* kwa muda mfupi iwe ni miaka mitano mpaka kumi au kumi mpaka kumi na tano, kwa muda mrefu ni miaka mingapi.

Kwa sababu nasikitika kidogo sera imekwenda sana *deep*, lakini kipengele cha tathmini kimewekwa mwisho na wala hakikupewa uzito unaostahiki. Mhe. Spika, kiko ukurasa wa 51 ambao ndio unaomalizia hii sera. Lakini sikuona kwamba kuweka mwisho labda ndiko kimedharauliwa ah!

Kwa sababu tathmini huja mwisho, ndio kikawekwa mwisho. Isipokuwa nilichoona kuwa hakikupewa uzito ni ile sentensi iliyoandikwa. Katika *paragraph* ya pili kifungu cha 15.0 kinachozungumzia usimamiaji na tathmini, naomba kunukuu Mhe. Spika.

> Ukurasa wa 51, *paragraph* ya pili, kifungu cha 15.0, kinasema hivi:
>
> > "Sera itapitiwa baada ya miaka mitano, iwapo haja ya kufanya hivyo"

Ah! Kweli sera hakuna haja ya kutathmini, yaani hakuna hata wakati mmoja ambapo hakuna haja ya kutathmini sera, ndio maana niliposema tuwe *very definite* katika vipindi vyetu, yaani muda mfupi tunakusudia muda gani,wakati ni muda gani. Kwa sababu kabla ya kufika vipindi vile lazima tufanye tathmini ya sera na wala haiwezekani kabisa sera kwenda.

Mhe. Spika, niliangalia kidogo katika *Policy Analysis* anasema baada ya *definition* tu na ku-*detail problem* lako, *establish evaluation criteria*, yaani hii ni sehemu ya pili. Kwa hivyo, hii imo katika *Internet Policy Analysis*, yaani uweke mikakati ya kufanya tathmini, kwa maana hiyo unaipanga kabisa kwenye sera na wala si kitu *alternative* ambacho unaweza kukichukua au huwezi, yaani ni lazima kufanya tathmini.

Kwa mfano lile tatizo nililolizungumza mwanzo kwamba Shirika la Umeme linawahudumia asilimia 25 tu ya Wazanzibari by 2005 kwa mujibu wa *House Hold Budget Survey*. Sasa kila mwaka pengine wanafanya tathmini. Je, kwa mwaka huu tumeongeza wangapi? Kwa hivyo, tathmini inafanywa kila baada ya kipindi na wala hatusubiri mpaka ule muda unapomalizika.

Mhe. Spika, tathmini ni eneo muhimu sana la sera na pengine hilo ndilo linalozikwaza sera zetu, yaani tunakuwa na wingi wa sera, lakini maendeleo pamoja na mabadiliko hayapatikani kwa sababu hatufanyi tathmini ya sera, tunaogopa.

Mwisho Mhe. Spika, naomba nichangie kidogo kuhusu nishati na maendeleo. Kwa kweli hakuna ambaye anapinga, lakini kuna hili la muda mfupi, sisi Zanzibar tunavyo viwanda kidogo na watu wa viwanda wanasema moja katika tatizo lao ni *expensive power*, yaani nishati ya umeme ni ghali sana kwa upande wa viwandani.

Kwa hivyo, sijui kwa maendeleo ya viwanda, suala hili tumeshalifanyia utafiti na kuliona kwamba kwa mwelekeo wa baadaye umeme wa viwandani tunaupangia vipi? Wenzetu wanafanya vipi? Hivi hakuna *package* maalumu kwa ajili ya watu viwandani? Kwa sababu wale watu wa viwanda kama tunavyosema wanazo faida tatu katika nchi.

Kwanza, wanakuhakikishia ule umeme wako watauchukua, kwani ni *high consumption unity*, wanatoa *tax* na suala la tatu wanaajiri, yaani hali ile ya kutoa ajiri viwandani, basi ni sehemu kubwa ya usaidizi katika nchi. Sasa na wao wanahitaji kupewa *package* maalumu na wala sio *tariff* ya kiwanda ndio iwe basi.

Lakini kama kiwanda kweli kinaajiri watu wengi na unakiona kinazalisha. Kwa hivyo, wanahitaji kupewa *package* maalumu na hii ilikuwa izungumzwe kwenye sera, kwamba katika maendeleo ya viwanda Shirika la Umeme litoe *package* maalumu kwa ajili ya viwanda.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono sera pamoja na hali yoyote tutakayokwenda nayo, lakini ni muhimu wenzetu kuiunga mkono, kwa ajili ya kupata maendeleo halisi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Zakiya Oma Juma: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika sera yetu hii muhimu, ambayo kwa kweli kila mmoja alikuwa na hamu kubwa ya kwamba iletwe katika Baraza hili.

Mhe. Spika, kabla ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutufikishia siku hii ya leo, kwa sababu ilikuwa ni siku ambayo tunaisubiri sana tena kwa hamu kubwa. *(Makofi)*

Vile vile, nichukue fursa hii adhim kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote, kwa kuwa wakweli pamoja kuwa waungwana na kuhakikisha kwamba sera hii imekamilika na kuweza kuiwasilisha barazani kama ambavyo Mhe. Waziri alitoa ahadi hiyo na leo imetimizwa.

Nikiendelea na dibaji hii ya shukurani sina budi kumshukuru Balozi wa Norway nchini Tanzania, kwa juhudi zake kubwa katika kufanikisha suala zima la sera na umeme katika nchi yetu pamoja na kutupatia fursa ya kuweza kupata semina ambayo tulipata maelekezo ya masuala mbali mbali yaliyofikishwa kwetu kupitia Baraza lako hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kwa ajili ya kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ujumla wao. Kutokana na mashirikiano, umoja pamoja na mshikamano tulioonesha na kufikia kufanikisha suala hili na hatimaye leo tupo hapa kwa ajili ya kujadili. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu nataka niingie kwenye sera yenyewe kwenye kipenge cha 4.1 kinachozungumzia kuhusu Lengo Kuu la Sera, Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kipengele cha 4.1 kinachosema hivi:

> "Lengo Kuu ni kufikia mahitaji ya nishati kwa watu wa Zanzibar kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi pamoja na kulinda mazingira"

Mhe. Spika, lengo linaeleweka na kufahamika vizuri sana, isipokuwa kuna kazi moja kubwa sana ili tuweze kulifikia hili lengo, basi wametangulia hapa Mhe. Rashid Seif Suleiman, kuzungumzia suala zima la hali ya matumizi ya miti. Kwa kweli yeye alisema *almost* iko 79 *percentage* tunatumia zaidi miti, jambo

ambalo linaangamiza au linaharibu mazingira, kwa sababu tunatumia kuni na makaa, pengine umeme ni asilimia 4.

Kwa hivyo, hili ndilo linalotaka kufanyiwa kazi kubwa tena ya kina na kama alivyomalizia Mhe. Mjumbe ni kwamba tathmini ya mara kwa mara ni muhimu sana kufanyika. Mhe. Spika, pamoja na ilivyoelezwa kwenye sera hii kwamba watafanya baada ya miaka mitano kama kuna haja.

Kwa kweli nadhani haja ipo na wala isiwe kwa miaka mitano, lakini iwe kwa mwaka ili kuona kwa kiasi gani, yaani watakapoipima itakuwa ni kazi ya kiasi gani, kwa sababu miongoni mwa malengo ni kuwaingiza zaidi watu kutumia nishati hizi, kwa ajili ya kuweka mazingira yetu vizuri na kuacha kutumia masuala ya kuni na makaa.

Mhe. Spika, haya ni mambo ambayo tumeyazoea kwa muda mrefu, haitakuwa rahisi tu kwamba kwa sababu kuna sera, basi aache kutumia makaa au kuni, kwa kuwa kuna umeme wa kutoka Tanga pamoja na ule mwengine ambao tunautarajia baadaye na huu ambao tuna hivi sasa ukawa unamvutia. Pengine unaweza kumvutia kinadharia, lakini kihalisia ikawa ni tatizo. Kwa hivyo, hii ni *challenge* ambayo kwa kweli wizara inahitaji kujipanga vya kutosha.

Nadhani tungesaidia namna ya kufanya, kwa sababu pamoja na kwamba sera imeeleza na ndivyo hali halisi ilivyo kwamba si Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi peke yake itakayohusika na hili. Lakini ni sekta tofauti kwa maneno ya sasa wanasema ni suala mtambuka ambalo sote kwa umoja wetu kupitia mashirika, wizara pamoja na taasisi mbali mbali tutakuwa na wajibu pamoja na jukumu la kuona kwamba tunalifanikisha hili. Isipokuwa mhusika mkuu zaidi itakuwa katika wizara yetu hii.

Mhe. Spika, nafikiri wizara ingeli-*influence* na taasisi nyengine zikiwemo na wizara nyengine pia, kuona katika hayo malengo tunayojipangia ya muda mrefu, mfupi na wakati, basi tungejiwekea muda ikiwa ni mfupi au wakati kuwa na kipindi cha mpito, kuona kwamba tunaongeza watumiaji wa umeme au vitu vyengine visivyokuwa vya kuni na makaa. *(Makofi)*

Hili ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha, lakini elimu peke yake Mhe. Spika haitoshi, lazima kuwe na vivutio vya kuona kwamba mtu atavutika kuacha kutumia kuni na makaa na kutumia umeme au gesi.

Mhe. Spika, kipindi hiki cha mpito kiwe kimeweka malengo yatakayomfanya mtu asione ule uzito wa kujiunga. Kwa mfano kama ilivyozungumzwa hapa kwamba bado gharama za kuunga umeme ni kubwa na wengi wangependa kuwa na umeme kwenye nyumba zao, lakini uwezoo ni mdogo na hawa ndio

watu wengi ambao wanashindwa kuunga umeme kwenye nyumba zao kutokana na gharama hizi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wizara ingeweka mkakati wa makusudi kwa kipindi fulani. Kwa mfano mimi nimeweka biashara yangu na kwa kutaka kufanya *competition* pamoja na kuvuta wateja, basi unaweka bei ambayo kila mtu ataacha kwenda kwengine na kuja kwako. Hivyo, hata kwa upande wa wizara ingeweka kitu kama hiki, badala ya kuchukulia kuna gharama kubwa ya mambo fulani, lakini tuone *target* yetu ni kitu gani.

Nadhani ni vyema tungeweka hiki kipindi cha mpito cha kuona kwamba watu wengi watavutika kuunga umeme na kuacha kutumia kuni na makaa, badala yake atumie jiko la gesi, kwa kuweka kile kiwango ambacho kwa asilimia kubwa itakuwa mtu ataweza, kutoka kwenye utaratibu ule wa zamani wa kutumia masuala ya kuni na makaa na kuingia kwenye utaratibu huu.

Mhe. Spika, tulikuwa na watu wa Kampuni ya Gesi *ORXY* hapa Barazani, walikuwa wakifanya *campaign* pamoja na kutoa elimu kwamba watu waache kutumia masuala ya makaa na watumie gesi ambayo haina matatizo na wala sizo zile gesi za kuripuka, kwa sababu hii ni *light gas*. Kwa kweli ni maneno mazuri yanavutia, lakini sasa ukirudi unashindwa, kwa sababu hilo jiko lenyewe kwanza linaanzia 90,000/-, pengine mtu huo mshahara wake hautimii. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nafikiri katika kufanya vivutio vya kuwaondosha watu katika utaratibu fulani na kuwaweka kwenye utaratibu mwengine ni suala zuri, lakini uzuri siku zote ni lazima uzurike. Kwa hivyo, kuna haja ya makusudi kabisa kuweka mkakati wa kuona katika kipindi fulani baadaye tutarudi kwenye utaratibu mwengine, lakini kwanza kuvuta wale wateja na kuweza kuunga umeme na kuacha kutumia makaa na kutumia gesi.

Hivyo, ni vyema kuweka utaratibu ambao utamfanya mtu aweze kumiliki jiko la gesi na kuweza kutumia gesi, ambayo kwa tathmini yake ataona kumbe zile shilingi 2,000/- ninazonunua makaa kila siku ni bora kununua jiko la gesi pamoja na mtungi wake, ambayo pengine itanichukua mwezi au miezi mitatu inategemea na kile kiwango ambacho atapenda kutumia kwa mujibu wa uwezo wake. Lakini kiwe katika viwango ambavyo kwa kweli ataona hiyo mantiki ya kuacha kutumia kuni na makaa na kutumia masuala ya umeme na gesi.

Kwa hivyo, napendekeza sana kwamba pamoja na taratibu ambazo zitapangwa pamoja na malengo haya ya muda mrefu na mfupi, lakini kiwepo kipindi cha mpito ambacho kitaweza kuwavuta wateja wengi kujiunga na kucha masuala ya kutumia kuni na makaa.

Vile vile, wakati kamati yetu ilipokuwa ikifanya ziara za kazi za kamati tulipokuwa Tanzania Bara Mhe. Spika. Kwa kweli tulikwenda kwenye Kampuni ya *ORXY* ambao wao ndio wanaosambaza gesi kwa asilimia kubwa katika nchi na wanatuuzia kwa bei ghali. Kwa kweli walikubali hilo, lakini pamoja na ughali suala zima la usafiri linachangia huo ughali.

Sasa kama ungepatikana utaratibu wao wa kuweka gesi yao hapa Zanzibar, basi usambazaji ndani ya visiwa vya Zanzibar ungekuwa na nafuu, pengine ingeshuka kiasi asilmia 50. Lakini gharama kubwa inakuja katika suala zima la usafiri.

Kwa hivyo, naomba kukumbusha kwa sababu tulizungumza hili wakati wa kamati, kwamba walikuwa wanaomba na hili litaingia katika hiyo namna ya mikakati ya kuwashajihisha waweze kutumia hizi nishati mbadala baada ya kuacha kuni na makaa, basi waweze kutumia gesi.

Mhe. Spika, ikiwa hiyo gesi inapatikana hapa, ingawa hivi sasa inapatikana hapa. Lakini kutoka Dar-es-Salaam na kuja hapa, ambapo inakuwa bei ni kubwa zaidi, kuliko kama ingekuwa shirika wenyewe wamepata pahala na kuweza kuileta mpaka ndani ya visiwa, halafu sisi kununua kwetu ni kutoka kwao hapa hapa, yaani wapate sehemu ya kufanyia biashara yao.

Nadhani hilo ni miongoni mwa yale mambo ambayo yanaweza kusaidia jinsi ya kupata wateja kwa wingi, ambapo itakuwa ni kuliimarisha zaidi shirika.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusiana na mafuta. Kwa kweli sote tunaona hali halisi na kama tunavyosema jambo huwezi kuona faidi na hasara yake mpaka inapokuwa kile kitu hakipo, yaani unakikosa. Kwa hivyo, niungane na wenzangu kwamba pamoja na yapo mashirika mbali mbali ambayo yaliyopewa haki ya kuweza kuagiza na kuuza bidhaa hii.

Lakini bado kuna haja kwa serikali nayo kumiliki hii rasilimali na kuweka matangi makubwa ya kuweza kuwa na hakiba, wakati inapotokea tatizo kama hili, basi serikali ikaweza kuhami wananchi wake.

Vile vile, niungane mkono na Mhe. Hamad Masoud Hamad kwamba tulimtembelea mwekezaji mmoja ambaye anafanya kazi nzuri pale Mangapwani.

Isitoshe kuwa ni mwekezaji na kwa sababu wizara baadaye linapotokea tatizo, wao ndio wanaoulizwa, basi wangeona kuna haja ya kuwa na hakiba ambayo watakuwa nayo wao kama serikali inapotokea matatizo yoyote kuhusiana na hii nishati ya mafuta na kadhalika, basi waweze kuihami hiyo hali. Kwa sababu

hivi sasa hali ni mbaya na huko mitaani ndio tunao uzoefu zaidi kutokana na kukosekana kwa mafuta.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu nishati mbadala. Kwa hivyo, kama nilivyotangulia kushukuru kuwa sasa Pemba inataka kuandika historia kutokana na tatizo lile la umeme ambalo kila siku ni kilio sasa tutapata umeme wa uhakika kwa muda usiopuungua miaka 30 na zaidi, itategemea na matumizi kama alivyozungumza Mhe. Waziri asubuhi.

Lakini nasema kama wengine wanavyosisitiza na kwamba wizara pia imeliona hilo suala, kwamba kuna haja pamoja ya kuwa na mikonga ya nyaya za umeme kutoka Tanga na mwengine tunaotarajia kuwepo hapa baadaye na huu uliopo.

Kwa kweli bado kuna haja ya lazima ya kuwa na majenereta ya hakiba, sio tu kuwa na majenereta ya hakiba pia, naunga mkono sana suala zima la kuwa na umeme mwengine wa hapa nyumbani, ambao unatokana na nishati kama vile ya upepo, jua na kadhalika, yaani kadri ya tathmini inavyokwenda na tunawapongeza sana wale wanaofanya hiyo shughuli kwa gharama zao kwa niaba yetu, basi hili liwe ni suala la kulivalia njuga.

Hivi sasa tunatarajia kuwa na umeme wa uhakika kule Pemba na baadaye hapa Zanzibar tukajiachia, kwa sababu hili ni tatizo ambalo nadhani ndilo lililotufikisha katika hali ambayo tunayo sasa. Kwa kuwa tuliona umeme wa kutoka Ras Kilomoni mpaka Fumba upo tena wa uhakika, basi tulijisahau na kujiacha.

Pengine tulikuwa na vijenereta vya hakiba na kwa sababu ya imani pamoja na huruma zetu tuliwapa wengine, lakini sisi wenyewe sasa imetokezea tunayo matatizo, basi tunashindwa kupata mtu wa kutulilia hali kwa machozi ya huruma.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba tunamshukuru sana Balozi wa Norway kupitia Shirika lao la *NORAD* kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutusaidia kwenye suala hili.

Kwa kumalizia nizungumzie kuhusu suala zima la kupata wataalamu.Pia, nichukue fursa na nafasi hii adhim kuwashukuru Serikali ya Ras-el-Khema, ambayo ndio imejitokeza kutufadhili kwa kutusomeshea vijana wetu. Lakini naamini sana haya yote yanatokana na juhudi kubwa ambayo ilikuwa ikifanywa na Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake na tukaweza kufanikiwa kuyapata haya yote. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika pamoja na shughuli kuwa nzito tena ni kubwa, lakini tunatoka mbali pamoja na watendaji wako wote kwa ujumla. Hivyo, nakuombeni sana muendelee na juhudi hizi kwa faida ya nchi yetu pamoja na hatma ya vizazi vyetu vijavyo ili suala hili kama ambavyo sisi tunalipata, basi tusilitegemee tena kwa vizazi vyetu vinavyokuja.

Mhe. Spika, namshukuru sana na kumuomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote waendelee na juhudi hizi za kutafuta wafadhili wengine mbali mbali licha ya hawa Ras-el-Khema, basi wakitokea na wengine hakuna ziada mbaya. Kwa sababu katika kuliimarisha shirika ni pamoja na kuwa na wataalamu tena wa kutosha na wakiwepo wa hakiba si vibaya.

Nakushukuru sana Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Sera hii ya Nishati ya Zanzibar.

Kwanza naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Naibu Waziri pamoja na wataalamu wake wote, ambao waliosaidia kwa njia moja au nyengine na kuweza kuleta sera hii katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Sekta hii ya Nishati ni muhimu sana kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Kwa kweli sera hii imechelewa sana kuja kwenye Baraza hili na muda mrefu tumekwenda bila ya kuwa na sera, ndio maana matatizo mengi sana yamejitokeza hadi leo karibu mwezi na zaidi tumo kwenye kisa hiki ambacho hatujui lini tunaondokana nacho.

Kwa kweli tunayo matatizo makubwa sana ya umeme, mafuta, ukataji miti ovyo pamoja na mengineyo. Lakini tukiangalia katika sera hii nashukuru *Alhamdulillah* Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake wameangalia kwa kina masuala yote muhimu na wameyaingiza katika sera hii. Ukiangalia kuna mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Kwa kweli sera hii ni nzuri, inatekelezeka na ina aminika, lakini tu ni kwamba hakuna kizuri kisichokuwa na ila. Kutokana na hali hiyo, ndio tumesimama hapa ili kuichangia kidogo angalau tuboreshe zile sehemu ambazo tunahisi kuna kasoro ndogo ndogo.

Mhe. Spika, kwanza nashukuru kuona kwamba katika ukurasa wa tano sera imetambua kwamba Zanzibar ni dola, hili ni jambo la kushukuru sana. Kama mwenzangu aliyetangulia Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kwamba katika

kutengeneza sera lazima kwanza watafakari ile hali halisi ilivyo ya sasa nchini mwetu kuhusu sera ya nishati. Kwa sasa hivi Mhe. Spika, tukiangalia historia ya Zanzibar suala la umeme na mafuta lilianza mwanzo kuliko nchi yoyote katika Afrika ya Mashariki. Tangu karne ya 18 umeme Zanzibar ulikuwa unapatikana na ulisambazwa katika mji wa Zanzibar na matangi ya mafuta yalikuwepo katika bandari ya Zanzibar. Hali hiyo sifa ya Zanzibar ilisikilikana kwamba Zanzibar ina umeme kuliko nchi nyengine za Ulaya. Kwa hivyo, suala la umeme Zanzibar sio suala geni ni suala la muda mrefu kabisa na wananchi wa Zanzibar wanalifahamu.

Mhe. Spika, hali halisi ilivyo sasa ni kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa sasa hivi tunatumia umeme unaotoka Tanzania Bara na hatuna njia yoyote mbadala kuhusiana na umeme hapa visiwani mwetu.

Jambo la pili, ni kwamba tunatumia gesi, mahoteli yote ya hapa sasa hivi wanatumia gesi na baadhi ya watu binafsi, gesi hii inapatikana kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, pia. mafuta yote tuliyonayo tunaagiza kutoka nje, nusu ya kuni zinatoka Tanzania Bara na mwisho kuni zitapatikana hapa hapa Zanzibar kwani taka taka za kilimo, makozi, vifuu na makumbi yanapatikana hapa Zanzibar kama ilivyoeleza hii sera yetu.

Mhe. Spika, tukianza na suala la umeme kwa bahati mbaya kwa muda mrefu tumekaa tunatarajia kwamba umeme kutoka Tanzania Bara ungekidhi haja yote yakuweza kuiendesha Serikali yetu ya Zanzibar hasa katika miradi hii ambayo tumeita wawekezaji wengi kuja kuekeza katika masuala ya viwanda, mahoteli na miradi mengine mengi. Tunategemea umeme tegemezi ambao unatoka Tanzania Bara hatukuwa na njia nyengine yoyote mbadala tuliyofikiria yakuweka angalau jenereta za akiba pakitokezea matatizo madogo madogo.

Mhe. Spika, lakini kwa miaka ya karibuni suala kubwa limejitokeza hapa kwamba wenzetu wa Tanzania Bara ambao tunawategemea kwa umeme na wao pia wana matatizo tena makubwa sana. Mvua kidogo tu ikisita kunyesha tayari umeme unakuwa ni wa mgao na hali ya Tanzania Bara inakuwa mbaya sana. Kwa hivyo, nasema kwamba kuendelea kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara ni tatizo.

Mhe. Spika, umeme upo Zanzibar na tunatarajia katika kipindi kinachofuatia tutapata hayo matengenezo na hiyo *cable* mpya. Kwa hivyo, tutapata umeme. Lakini umeme wa Zanzibar ni ghali kuliko malipo ya umeme katika Afika ya Mashariki na nchi nyengine hasa kutoka South Africa na ukija huku juu

kwenye *SADEC,* Zanzibar umeme ni ghali. Hili linasababishwa kwa wawekezaji kuja kuwekeza hasa katika shughuli za viwanda kuwa doro sana. Mhe. Spika, wawekezaji wa viwanda wanahisi kwamba wakizalisha bidhaa Zanzibar hawawezi kwenda ku-*compete* kwenye Soko la Afrika Mashariki kwani vifaa vyao vitakuwa ni ghali sana.

Mhe. Spika, ni kwamba tusidanganyane Zanzibar ni kisiwa na kisiwa uchumi wake ni biashara, viwanda hivyo ni lazima kwa sababu visiwa vinatoa *service*. Sio vibaya kwenda kusoma wenzetu wa Mauritius na *source* zao za umeme, wenzetu wa Singapore na wenzetu wa Hong Kong. Juzi nilikuwa Hong Kong nikakuta jamaa wanashereheka miaka 20 ya Hong Kong kuwa haujakatika umeme hata dakika moja. Mhe. Spika, kwa sababu umeme ukikatika dakika moja hiyo hasara yake haisemeki.

Kwa hivyo, wameshereheka kwa sherehe kubwa sana mpaka nchi nzima imerindima. Wao hawana *cable*, lakini tujue wanafanya nini hata wakaweza kuupata umeme ambao kwamba viwanda vingi na *investors* wengi wamekwenda ku-*invest* katika nchi zao na umeme wao ni rahisi wa kuweza wawekezaji kuja kuwekeza na ikawa wanaweza kufanya biashara zao bila ya matatizo yoyote. Mhe. Spika, nasema Zanzibar tunahitaji viwanda.

Mhe. Spika, licha ya kuwa umeme wenyewe uko ghali, kuna jengine ni kubwa sana kwamba umeme wenyewe hautimii viwango. Umeme unakuja ukifika pale ukipimwa uko *less by forty or by fifty*, haya ni matatizo makubwa sana. Mhe. Spika, vifaa au mitambo ya siku hizi ambayo inatumia teknolojia ni kwamba vifaa vinaungua mara moja na viwanda vingi sasa hivi ukenda ukinunua mitambo sio kama ile ya zamani, mitambo ya sasa hivi mingi inakuwa ni *control electronically,* hasa umeme kupanda na kushuka unasababisha vifaa kuungu na vifaa vikishakuungua tayari *machine* hizo zinakuwa hazifanyi kazi.

Kwa hivyo, wawekezaji wanataka *stable power supply*, sio iwe inapanda ikishuka utakuta kila mmoja sasa hivi ameweka *stabilizer* kwa sababu yakuwa umeme unaokuja hauna viwango vya kuweza kuendesha viwanda. Kwa hivyo, haya ni matatizo ambayo tunayo sasa hivi hapa Zanzibar. Kwa hiyo, tukitaka kurekebisha hali, sera yetu ingeliangalia kwamba tuwe na uhakika wa kuweza kusambaza umeme ambao utakuwa wa uhakika na vigezo vyengine. Kwa mfano ukiweka *city scan* ni lazima kuwe na *stabilizer* tena iwe inafanya kazi vizuri, kama si hivyo, inaungua.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wananchi wa Zanzibar kwa kweli ni wananchi ambao wanaipenda serikali yao na kwa sababu hili Shirika la Umeme ni la serikali, lakini naamini kama shirika hili lingekuwa ni la mtu binafsi basi sasa hivi ameshafungwa. Kwa sababu vitu vinavyoungua majumbani na katika

sehemu za biashara huwa vinaungua kwa matatizo ya umeme. Mhe. Spika, nchi nyengine kitu chochote kikiungua, basi unakwenda Mahakamani na ikitokea kama kweli kitu kimeungua kutokana na ukosefu wa umeme basi kampuni hiyo inashtakiwa na inalipa gharama.

Mhe. Spika, tuangalia mji huu vitu vingapi vimeungua kutokana na ukataji wa umeme ovyo na umeme kuwa hauko *stable*. Kwa hivyo, mimi naomba kwamba suala la umeme liangaliwe upya katika sera hii, lakini hakukuwa na hoja madhubuti yakuweza kuboresha Shirika la Umeme. Mhe. Spika, imeonekana kwamba ipo nafasi yakuweza kuanzisha mashirika ya watu binafsi kuweza kusambaza umeme. Hili ni suala muhimu sana na la kupongezwa katika sera hii kwamba halikusahauliwa. Pia, tungeomba ifanyike jitihada ya makusudi ili tuweze kufanikiwa na suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu suala la gesi mpaka sasa hivi hakuna mwekezaji hata mmoja aliyekuja Zanzibar kuekeza kwenye suala la gesi. Suala hili ni muhimu sana kwa sababu gesi inapotumika kwanza katika nchi zote ambazo masikini kama sisi walikuwa wanasema kwamba gesi ndio *source* rahisi ya kufanyia kazi zao kuliko mkaa na kuni. Mhe. Spika, gesi kutoka Tanzania Bara ni ghali sana na inakuja kwa njia ya usafiri wa majahazi na meli. Lakini hapa utakuta kuna *double handling*, *double tax* na *double profit.* Kwa hivyo, hiyo ndio inasababisha kuwa gesi imepanda bei sana.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya hapa kwetu sisi Zanzibar tuna jambo moja ambalo sio zuri, *ZIPA* ipo ambayo kazi yake ni kuwapokea na kuwavutia wawekezaji. Lakini *ZIPA* imekaa kama buibui, buibui anatega pale kwenye kona anaweka wavu wake kinachokuja pale ndio chake, akija nzi ni wake, akija mbu wake anayekwenda, ndio ameshafika hatoki. Kwa hivyo, *ZIPA* haiwezi kukaa pale kwenye kona ikangoja wawekezaji waje pale, hiyo hapana ndio ukaona hapa Unguja hakuna zile hoteli za kimataifa labda hiyo Kempiski. Mhe. Spika, ni kwamba hawatoki nje ya nchi kama wenzao wakawasaka wale wawekezaji, mwekezaji hasa mwenye fedha yake hapa haji mpaka umfuate umwambie kiwanja hiki hapa na mradi huu umpe vile vichecheo na umpe ule ushawishi wa kuweza kujiimarisha katika nchi yako.

Kwa hivyo, mimi naamini kabisa kwamba tukiweza kuwashawishi wakaja wakawekeza kwenye suala la gesi na tukawapa muda mzuri wa kufanya kazi zao. Naamini kwamba suala la gesi hapa Zanzibar itakuwa ni rahisi na wananchi watahamasika na mahoteli yote haya yatatumia gesi na viwanda vyengine vinavyokuja vitatumia gesi. Mhe. Spika, gesi ya Zanzibar hainunuliki jamani na hii ni njia moja wapo itakayotuokoa katika masuala ya kutumia umeme mwingi zaidi.

Mhe. Spika, nikija katika suala la mafuta ni kwamba matatizo yake tumeshayazungumza hapa tangu juzi na tumeelewa kwa kiasi fulani. Lakini mafuta tumeona kwamba sasa hivi pana kampuni tangu zinazosambaza mafuta, jawabu kwa Mhe. Waziri, zimekuja na zimeturidhisha kwa kiasi fulani, lakini ukiangalia kwa mbali utakuta kampuni tatu haziwezi kushindwa kusambaza mafuta katika nchi hii bila ya kuadimika. Iko kampuni moja tu ilikuwepo hapa na ilifanya kazi kwa muda wa miaka mitano hatukuona shida ya mafuta itakuwaje kampuni tatu zishindwe kufanya hivyo.

Mhe. Spika, ni kwamba kampuni hizi zinategeana ikiwa mafuta yamepanda bei wakiingiza mafuta nchini, mafuta yale yakishuka bei hawa jamaa huwa wanakula hasara kidogo. Huko Bara kuna kampuni nyingi sasa hivi zimeacha kuagizia mafuta kwa sababu walikuwa wanaagiza mafuta mengi na mwaka jana mafuta yakapanda bei sana wakawa wana *stock* kubwa ndani, mafuta kuja kushuka bei ile *stock* walikuwa hasara kubwa sana. Kwa hivyo, wakashindwa kuagizia mafuta sasa hivi wananunua kwa wenzao tu pale pale Dar es Salaam.

Kampuni ya BP tu ndio inayo *survive* katika pigo lile utakuta kwamba matumizi yaliyokuwepo ni haya kwamba hawa jamaa wanategeana, wanaangalia nani anayo anaweka hapo kuangalia bei akiona bei inapanda basi mafuta hanunui, bei ikishuka mafuta ananunua analeta kwa sababu anaona ikija ikishuka atakula hasara.

Kwa hivyo, mimi ningeona kwamba Mhe. Waziri angechukua hatua za haraka za kuweza kwenda kuzungumza na hawa wawekezaji wa mafuta. Mhe. Spika, jambo hili limo katika sera ya muda mfupi kwamba wanaweza kufanya *joint procurement*. *Joint procurement* itaweza kuleta bei ndogo na itaweza kuhakikisha kwamba mafuta yapo na ule utegeaji wa mtu unaweza ukaondoka itapatikana *bulk procurement by joint procurement.*

Mhe. Spika, tukija katika mafuta ya ndege kwa bahati mbaya kabisa mafuta haya yetu sisi hapa ni ghali zaidi kuliko mafuta ya ndege ya Dar es Salaam na Mombasa. Kwa hivyo, *competition* hapa iko kubwa sana. Hii inatokana kwamba Zanzibar kuna *petroleum levy*, *exercise duty* na kuna *transportation*, ndio maana ikasababisha mafuta ya ndege yakawa ghali zaidi hapa Zanzibar.

Tunashukuru kwamba mafuta ya ndege Zanzibar husikii mara kwa mara kuwa yanakatika kwani *supply* ni nzuri, lakini bei ni kubwa ukilinganisha na bei ya Dar es Salaam na bei ya Mombasa. Mhe. Spika, watalii wanakuja wengi Zanzibar. Kwa hivyo, tunahitaji usafiri kwa watalii uzidi kuongezeka, Uwanja wa Ndege unajengwa sasa hivi, kwa hivyo, tungeomba sera hii ikaangalia namna gani itaweza kuona kwamba inaangusha bei ya mafuta ya ndege ambayo kwamba *competition* ipatikane vizuri baina ya Mombasa na Dar es Salaam.

Mhe. Spika, tukenda katika suala la kuni na makaa nina hakika kwamba tukiweza kufanikisha suala la umeme, tukafanikisha suala la gesi, tutafanikisha suala la mafuta, basi *naturally* suala la utumiaji wa kuni na makaa unaweza ukapungua kwa kiasi kikubwa sana. Leo ukenda katika nchi nyingi utakuta makaa ni ghali kuliko gesi, watu mpaka mishkaki sasa hivi wanachomea gesi badala ya kuchomea makaa kwa sababu makaa ni ghali zaidi kuliko gesi. Kwa hivyo, naamini tukifanya hivyo tutafanikiwa.

Mhe. Spika, nikenda suala la uchimbaji wa mafuta ambamo humo vile vile umetajwa. Mimi ningeomba kwamba Mhe. Waziri aone kwamba kutakuwa na sheria nzuri ambayo itajadiliwa, kutakuwa na *transparency* katika masuala ya uchimbaji mafuta na ufanyaji wa tathmini ya upatikanaji mafuta. Mhe. Spika, ningeomba kusema kwamba indhari kubwa ichukuliwe katika suala hili, nchi nyingi duniani zinatoa mafuta hasa tukiangalia kwa mfano huku Afrika, lakini mikataba ile na makampuni ya mafuta mikataba yake iko ovyo ovyo haiko wazi, mikataba ile ikiwa haiko wazi inaleta madhara makubwa sana katika nchi. Tuangalie wenzetu walioko Equatorial Guinea.

Katika nchi hii kuna watu laki tano na hamsini wetu, nchi hii inatoa mafuta mengi sana na yule mtawala wao anaitwa Tidioro huyu mshahara wake ni $ 60,000 kwa mwezi, lakini ni mtu tajiri anamshinda Queen Elizabet kwa utajiri. Yeye ana *jetty* sita na *jetty* zake zote hizo zinagharimu $ milioni 35, ana *palace* Malibu, Johannesburg, Maryland, lakini wananchi wake taaban. Mhe. Spika, kila katika watoto wanne basi mtoto mmoja anakufa kabla ya kutimia *birthday* yake na watu wake na watu wake umri wao ni miaka 49 hawazidi.

Mhe. Spika, hakuna mtu anayeweza kumuuliza mikataba iko karibu na yeye na kampuni za Kimarekani. Kwa hivyo, tunapotafuta mikataba tuwe makini zaidi. Kwa mfano hapo Tanzania Bara tunaona matatizo yaliyopo ya maadini.Pia, tuangalie DRC Congo katika mwaka 2007 imesafirisha maadini ya $ milioni 200 kupeleka nchi za nje. Lakini serikali ilipata tax kiasi gani 86,000 tu. Tuangalie Angola mwaka 2006 imesafirisha mafuta yenye thamani ya bilioni $ 30, lakini kwa bahati mbaya *operation* yao ni milioni 12 .Kwa hivyo, kila mmoja ana *two thousand five hundred dollars*, lakini watu wa Angola bado hali zao ni mbaya katika kila watoto kumi watatu wanakufa kabla ya kutimia miaka mitano.

Mhe. Spika, na umri wao ni miaka 41, hiyo ni mifano katika nchi za Afrika, mifano michache ambayo kwamba hili tatizo tayari liko Tanzania Bara makaburu wanachimba dhahabu wanaichukua, lakini Tanzania Bara hawafaidiki na mapato yatokanayo na madini mengine. Kwa hivyo, mimi natahadharisha kwamba ipo haja yakuwa wazi zaidi na kuweza kuangalia njia

gani za kuweza kudhibiti hao wawekezaji watakaokuja kuwekeza katika ubia na Serikali ya Zanzibar kuhusu masuala ya mafuta. Baadhi ya hili limeshiriki kikamilifu katika kulikomboa suala hili kutoka katika mikono ya muungano imeingia katika mikono ya Zanzibar, lakini kuna wengine wanaweza wakachukua kwa njia rahisi na wakafaidika watu wachache na Wazanzibari wakabakia na matatizo yale yale. Kwa hivyo, naamini kwamba ikiwa mikataba itakuwa mizuri na mipango itakuwa mizuri tunaweza tukakabiliana vizuri na suala hili.

Mhe. Spika, sera ni nzuri tumeangalia mambo mengi sana, ina kurasa 51 ambazo ukiangalia wameweza kutia *bold* zile sehemu ambazo ni muhimu na ukiziangalia utakuta kwamba kweli wameweza kuangalia mambo muhimu kabisa. Katika ukurasa wa 27 kuna mkakati wa hoja ya nane ya sera, hapa lazima tumpongeze Mhe. Waziri kutokana kwamba mambo haya ameona kuwa yana umuhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kwamba sera hii izingatie masuala ya nishati yaende kibiashara zaidi kuliko kwenye mpango wa *succeed.* Kwa mfano hapa asubuhi amezungumza Mhe. Waziri amesema kwamba Pemba umeme uliopelekwa umetumia bilioni 75 na ili kujilipa gharama hizi itachukua muda wa miaka 30. Hii inamaanisha kwamba kila mwaka itabidi Pemba zipatikane bilioni 2.5 ili iweze kulipa gharama zilizokwenda.

Mhe. Spika, kila nikiangalia vyanzo vya mipato, nikiangalia wimbi la uwekezaji Pemba sioni kwamba iko tamaa ya kuweza kupata bilioni 2.5 kwa mwaka. Kwa hivyo, mikakati kama alivyosema mwenyewe Mhe. Waziri katika sera yake kwamba kuna *institution* nyingi ambazo kwamba zinahitaji kushirikiana na *institution* hii ione kwamba inaweza kufikisha malengo yake ya sera hii.

Mhe. Spika, vile vile, naomba sera hii iangalie kwa undani namna gani itawezesha Wizara ya Biashara na Viwanda kwa sababu nyenzo ya nishati ni muhimu sana kwa wawekezaji, sio kupata nishati tu, lakini kupata nishati ambayo kwamba itakuwa ya bei nafuu.Pia, itaweza kuwavuta wawekezaji kuja kuekeza na kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu. Mhe. Spika, kwa hayo naomba kwa mara nyengine tena nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia juu ya suala la Sera hii ya Nishati ya Zanzibar.Pia, naomba nimshukuru tena Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake na jopo lake la wataalamu kwa kutuletea sera hii na kwa moyo mkunjufu kabisa naomba kuunga hoja juu ya Sera hii ya Nishati ya Zanzibar.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu mdogo katika Sera hii ya Nishati.

Mhe. Spika, nianze kwa kutoa tafakari juu ya namna ya uchumi wetu ulivyoanzia na unavyoendelea. Nadhani mtakubaliana na mimi Wajumbe kwamba katika miaka iliyopita tabia za watu wetu katika uzalishaji ziligeuza makaazi yenye vyanzo hasa vya baharini kama ni sehemu zao za kukaa kwa maisha na uzalishaji. Ni bahati mbaya kwamba makaazi haya baadae yalibadilika kuwa ni sehemu za watu kuzitumia katika uzalishaji, lakini si kwa makaazi. Mhe. Spika, *experience* hii sana unaweza ukaiona sehemu za Pemba katika sehemu ambazo tunaziita za makaani ndimo mwahala ambapo watu walikuwa wanakaa na shughuli zao kubwa ilikuwa ni kilimo na uvuvi.

Lakini kadiri miaka ilivyokuwa ikiendelea watu waliweza kuhama katika sehemu hizo na wakaja katika sehemu za Bopwe sio kufuatia karafuu tu katika sehemu zile, lakini kwa sababu ni sehemu ambazo serikali iliwekeza katika huduma hizi hasa umeme na barabara. Kwa hivyo, kadri miaka ilivyokuwa inasonga tuliweza kupata uzalishaji uliopungua katika sehemu hizi ambazo ni muhimu sana kwa sababu watu ilibidi waondoke masafa makubwa sana kufuatia uzalishaji. Nimetoa *experience* hii ndogo ya kihistoria ili kuonesha namna ambavyo umeme na huduma nyengine ni muhimu katika uzalishaji.

Mhe. Spika, lakini *experience* ya karibuni hivi imetufundisha namna ambavyo Wazanzibari sasa katika maelezo yetu, mazungumzo yetu na katika tafiti na uchambuzi mbalimbali za kuzungumzia uchumi na maendeleo, basi tunastahiki kuzungumzia nishati kwanza. Maisha yamegeuka kwa muda wa mezi mmoja tu, hali ya umasikini ambayo tulikuwa tunafikiria inaanza kupungua kwa kweli imewakumba watu. Si kiza tu katika majumba, si kukosa kuangalia mpira ule unaochezwa pale Angola tu, lakini hata hali ya umasikini.

Kwa kweli mimi napenda nimpongeze sana Waziri wa Elimu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Prof. Jumanne Magimbi kwa tangazo lake la kuondosha ada ya wanafunzi za mitihani kwa sekondari. Kwa sababu wanafunzi tayari walishaelezwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hapa Zanzibar kwamba mara hii hata *Form IV* itabidi mlipie mitihani na taarifa hizo wazee tulikuwa tumeshazipata, najua yote hii ni kwa sababu ya ukosefu wa umeme.

Mhe. Spika, ndio maana nilimuuliza Mhe. Waziri wa Fedha swali tumeathirika kiasi gani, najua kwake yeye ni vigumu sana sasa hivi kwenda kila sekta ya kuangalia taathira namna ilivyo, lakini kwa Baraza hili kuna umuhimu sana wa kujua namna ambavyo *interruption* hii ya umeme ilivyotokea ilivyoweza kuathiri shuguli zetu za kiuchumi kwa sababu bajeti ndio msingi wa uchumi na ni Baraza hili ndilo ambalo linapitisha bajeti. Bila shaka itakuwa tumeathirika.

Mhe. Spika, nikija kwenye sera ukiiangalia Sera ya Nishati namna ambavyo imeandikwa na kwa kweli mimi nimezunguka sana katika mitandao kuangalia sera za nishati za nchi, Marekani, Uingereza na nikaiangalia sera yetu unaweza kushindwa kutia neno ku-*improve* sera hii, huo ndio ukweli.

Lakini niseme tu, pamoja na mazuri yote yaliyomo humu lazima tuwe na mambo madogo madogo ya kuyasisitiza ili kuifanya sera hii iweze kufanya kazi vizuri. La mwanzo pamoja na kwamba limeandikwa humu, lakini lazima tulisisitize hilo, nalo ni *efficient* na namna ya ku-*conserve* utumiaji wetu wa umeme.

Mhe. Spika, hili ni suala lililo muhimu sana, kama tutaangalia *supply production* tu na *transmission* na matumizi, lakini tusiangalie namna ambavyo matumizi yanavyopotea, umeme unavyopotea, nishati inavyopotea, tunaweza tuka-*concentrate* tukasema kwamba *production* yetu ni ndogo, *transmission* ni ndogo, lakini tukasahau kwamba ndani ya *process* yote hiyo kwa kweli kuna upoteaji mkubwa na kuna *weakness* kubwa inayotokea kutokana na kwamba hatuna mipango ya ku-*conserve energy*.

Kwa hivyo, nilisema hili nilizungumze na kwa kutoa mfano, nilisema nilikwenda katika sera ya nishati ya Marekani. Kwa mfano nikaona kwamba Marekani kuna kampuni wanaita Chevron nadhani, hii ni kampuni mashuhuri sana. Kampuni hii imeeleza namna ambavyo imetumia *production* hii ya *power GO thermal* ambayo humu sikuiona katika sera hii. Nimeona maelezo mengi *solar, wind, read active* kutokana na mambo mengi lakini *GO thermal* sikuiona.

Wamefanya hivyo inawezekana pengine sikwenda *deep* zaidi, *GO Thermal* wame-*establish plant* katika nchi ambazo zinafanana na zetu, maana yake hizi ni nchi za visiwa. Nadhani ni nchi ziko mbali baadae zikija nitazitaja. Lakini kwa ku-*establish* viwanda vya kutoa umeme kwa kutumia *GO thermal* wameweza kusaidia watu milioni kumi na sita katika nchi hizo.

Waheshimiwa Wajumbe *GO thermal* ni neno la Kigiriki linatokana na *GO* kwamba ni *earth* na *thermal* na *heat*. Ni namna ambavyo kila unavyokwenda chini ya ardhi *temperature* inakuwa inaongezeka na inasemekana kwamba ukienda *centre of the earth temperature* ni karibu 6,000 *degrees cessions.* Kwa hivyo, kila unapokwenda *25 mitres atleast one degree cession* inakuwa inaongezeka.

Kwa hivyo, katika *system* kama hiyo utakapoweza kuchimba na ukaweka *cold water* mpaka ukafika kwenye pahala ambapo *scheme* itakuwa inafanya kazi na *heat* inakuwa ni kubwa na kuna *temperature* ya kuyeyusha mawe na ndio

maana kuna sehemu nyengine ukasikia kuna miripuko inayotokana na *volcano*. Kwa hivyo, uwezekano wa kutoa umeme kwa kutumia *GO Thermal* upo kwa sababu ukiweka maji baridi yanageuka yanakuja *steam* na ukiweka *steaming* basi uwezekano wa kutoa umeme upo. Nchi moja iliyonijia ni Philippines inatumia umeme wa aina hii.

Ninachotaka kukisisitiza hapa Mhe. Spika, ni kwamba lazima katika sera hii pamoja na kutaja lakini lazima tu-*practice* hii *diversification* ya *power. Diversification* sio tu kwamba itapunguza gharama za uzalishaji, lakini itapunguza utegemezi ambao Wajumbe wengi wameuelekeza. Kwa sababu ukiwa na utegemezi wa *energy* kwa kweli una nafasi ndogo sana ya kupanga mipango yako ya kiuchumi.

Nimeona humu kwa mfano katika ku-*predict long term prices* za *energy* lazima twende tukae pamoja na *TANESCO* pamoja na *EURA. EURA* zenye sera zake, *TANESCO* yenye matatizo yake, inafika siku *TANESCO* tunajua mashaka yake, lakini hatutoweza kukaa ku-*predict long term prices* ya *energy* yetu bila ya kukaa na hao. Kwa maana hatuwezi ku-*influence policy* ya *TANESCO* wala ya *EURA,* lakini tutalazimika kukaa nao kuweza kupanga bei. Nadhani hili ni tatizo moja kubwa, lazima katika mipango uwe unaweza ku-*influence factors* ambazo ni muhimu ku-*control* katika mipango yako.

Sasa nasema tukiwa na utaratibu wa kuwa na *diversification,* tukawa na mbadala katika *energy,* kwa kweli ni njia moja iliyo muhimu na hili lazima tulisisitize.

Wananchi wanasikia kwamba kuna umeme unatokana na bahari, lakini tumezungukwa na bahari. Wengi wanataka kujua ni kwa nini basi kama kuna umeme unaotokana na bahari *Zanzibar* hatuwezi kuwa na umeme? Yawezekana ikawa kuna matatizo hatuyafahamu, lakini ni wajibu wetu kama viongozi kuwafahamisha wananchi kwamba bahari hii iliyoko hapa ya *Indian Ocean* kwa sababu ya tabia zake pengine mawimbi madogo na mambo mengine hayawezi kutoa umeme, lakini wananchi watakuwa wamekwishaelezwa na tutakuwa tuna-*focus* mambo mengine.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika mada hii, mimi naomba sana wizara na serikali kwa ujumla lazima tuhakikishe kwamba tunao *experts* wa kutosha katika *energy sector.* Tumesikia idadi ile ya kuanzia sijui watu 25, lakini mipango ifanywe kuhakikisha kwamba tuna wataalamu wengi mno. Tukiwa na wataalamu wa kutosha katika nishati kwa kweli tutakuwa tumepiga hatua katika mipango yetu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, suala la ku-*conserve energy* wataalamu watakuwa wanajua zaidi, lakini upo uwezekano. Wataalamu wanasema unaweza sio tu una-*produce* kwa kutumia, lakini uwezo wa ku-*conserve energy* ili uweze kutumia kwa wakati mwengine yawezekana hiyo. *Experience* ya hiyo Chevron wao wameweza kuwa ni kama kampuni iliyokuwa *established* kuwasaidia *climes* wao ku-*conserve energy*. Wameweza kufanya hivyo na wanasema wana-*save* kwa wananchi wa *country* moja, kama mkoa mmoja wa Marekani kiasi ya dola mia mbili na sitini elfu kutokana na matumizi ya wananchi katika *energy*. Kwa hivyo, tuangalie vile vile na sisi katika mipango yetu ni namna watu wanavyoweza kusaidiwa ku-*save energy*.

Mhe. Spika, nikiondoka katika suala hilo la *efficiency* na *conservation* na huwezi kulizungumza kwa maana ya kuwasaidia wananchi katika kupunguza gharama tu, lakini sasa hivi mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanatufanya na sisi lazima tuwe wabiya katika kuhakikisha kwamba tunapunguza *emission* za *carbon*. Kwa hivyo, hatuwezi kufikiria kuwa na *energy* ambayo inaongeza, lakini lazima tufikirie kuwa na *energy* ambayo inaweza ikapunguza *carbon emission* katika jamii yetu na hiyo nadhani tutakuwa tumelenga sana katika suala la mazingira.

Mhe. Spika, nimeangalia katika kampuni hii ya Chevron moja katika jambo ambalo wanalifanya ni ku-*design* pamoja na ku-in*stall high efficiency equipments* ambazo zinasaidia ku-*save power*. Leo uagiziaji wetu wa vitu kutoka nje hautuhakikishii hata tukiwa na umeme kwamba kweli *efficiency na conservation* itakuwa ipo, kila mmoja anaagizishia chombo cha kutumia nyumbani, chombo cha kuendesha barabarani, chombo cha matumizi bila ya kuzingatia, lakini hatuwezi kuwalaumu watu kwa hili kwa sababu hapa panataka taaluma kubwa, lakini ni lazima wizara iwe ni waelekezaji sasa wa kuishauri *market* kwamba aina ya vyombo hivi mtakavyokuwa mnaagizishia hata kama tutakuwa tuna umeme wa kutosha, lakini suala la *efficiency* na *conservation* litakuwa lina mapungufu makubwa.

Ndio maana leo tunasikia katika *diversification* watu wanatoka katika kununua gari zinazotumia petroli wanakwenda katika gari zinazotumia gesi na pengine sasa hizi zinazotumia hata maji ya moto na aina nyengine tele, zinakuwa zinaagiziwa ili kusaidia ku-*stream line* matumizi ya *energy* katika nchi. Nasema hayo ni mambo ya kuzingatia na kuona kwamba tunawasaidia wananchi wetu na tunasaidia taifa katika matumizi ya *energy*.

Suala la matumizi ya *energy* tusiliangalie katika uchumi wetu wa leo, lakini tuangalia vile vile *future,* tunaelekea wapi kiuchumi na ni *sources* gani ambazo zitakuwa zinakubaliana na teknolojia ambayo itakuwa ina-*image.* Inawezekana ikawa tunafikiria mafuta, umeme unaotokana na *hydro plants* kutoka Tanzania

Bara, lakini ikawa teknolojia ya sasa hivi iliyo-*supportive* katika *energy* ikawa inalenga katika *renewable energies*, kama *solar*, pengine ni *winds* na mengineyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachotaka kusema hapa yote tutakayokuwa tunayapanga katika *energy* lazima tuangalie yanakwenda sambamba na teknolojia ambayo ina-*image* sasa hivi katika dunia. Kwa sababu usipozingatia *technology* utakuwa unajitosheleza kwamba unayo *energy*, lakini kwa sababu ya kuangalia namna *technology* ingeweza kurahisisha vipi *energy* ile kuwe *efficient* ukawea kukosa na ikawa ni *energy* ambayo ni ghali sana.

Mhe. Spika, watumiaji wetu wa *energy* ni wananchi wetu, hali zao za kiuchumi zinaeleweka na bahati mbaya tunapopanga bei za matumizi ya *energy* hatuangalii uwezo wa wananchi wetu. Kwa mfano kwa umeme huu wa leo tunaangalia gharama ya *TANESCO* wanatu-*supply* kiasi gani, hata tukija katika suala la *VAT* ongezeko la thamani ambalo inabidi lazima lilipwe katika umeme tunaangalia *rate* inasemaje ya *VAT*. Ikiwa Tanzania Bara ni 20% na Zanzibar nayo ni 20%, ikipungua 18% pengine na sisi tunakwenda kwenye 18%.

Ninachotaka kusema katika suala la sera ya *energy* tuangalie vitu hivi *succeed* zimetajwa lakini *taxes*, vitu ambavyo tunaweza tukavipanga vikaweza kusaidia bei za wananchi. Si vibaya hata kidogo katika sera na mipango badala ya kuwa na *blanket rate* ya *VAT* kwa kila kitu, kwa sababu ya ku-*stimulate* uchumi katika sekta fulani, Mhe. Spika, na hii *rate* nayo ika-*focus* katika hivyo, badala ya kuwa 18 ikawa hapa tuna 10 na hapa tuna 12. Hatuwezi kuwa na *rate* moja ya kila kitu.

Iko *experience* ya nchi za nje ambapo kama wanataka ku-*stimulate* utalii, basi huko *rate* ndio vitu ambavyo wanacheza navyo. Sasa *physical policy* imetajwa humu, lakini nazidikusema kwamba *physical policy* hii sio ya kwetu, hatuwezi tukakaa tukacheza na *physical policy* kama vile ambavyo tunaweza tukacheza na *VAT* ambayo inatolewa hapa *ZRB*, *physical policy* inatolewa *TRA* ambayo ni ya Muungano.

Kwa hivyo, tufike basi pahala tuone *physical policy* nayo haitumiki kisiasa ikawa kwa sababu *physical policy* tumesema tunasawazisha. Kwa hivyo, Tanzania Bara wanatumia hizi na sisi ndio hichi, hatuwezi kuwasaidia watu wetu kwa fikra kama hizo Mhe. Spika. *Rate* ya Tanzania Baraza ita-*focus* katika uchumi wao uwezo wa wananchi kuweza kuilipa, yawezekana hiyo na hivi ndivyo ilivyo ikawa haiwezekani kabisa kwa Zanzibar.

Kwa hviyo, kuna masuala nyeti kama ya *energy* lazima Baraza hili na serikali iwe na mamlaka juu ya kuona ni namna gani tunaweza kuzungumza na upande

mwengine wa Muungano ili walegeze masharti na *incentives* ambazo tunaweza tukazitumia katika kuwaleta wawekezaji. Ningependa kumshukuru sana Mhe. Waziri aliposema baadhi ya wawekezaji hawatokuja ni kweli, wawekezaji wengine kwa kuwatangazia tu kwamba tuna hichi, kwa sababu kila nchi inafanya hivyo, lakini *effort* lazima ya kuwafuata, lakini ukiwafuata na uwe na uwezo watakuuliza, *rate* hii ni kubwa kuliko ya nchi hii kwa nini nije kwako? Kwa hivyo, ni lazima kuwe na uwezo juu ya vitu kama hivi.

Mhe. Spika, suala la wananchi kuelezwa na kusomeshwa sio kuelezwa tena, kuhusu utoaji na matumizi ya *energy*, sasa liwe ni suala la lazima katika nchi yetu. Mhe. Spika, inawezekana ziko njia ambazo ni rahisi mno kwa wanachi kuweza kutumia vya kupata *energy*. Leo tunapata hadithi kutoka kwa wenzetu Tanzania Bara na sehemu nyengine wanavyotumia kinyesi kwa kutoa *energy*, wanavyotumia *remains* za kwenye miti na kwenye mashamba kwa *energy*. Lakini hizi si utaratibu ambao leo hapa kwetu upo, kwa sababu wananchi hawajui chochote na si wananchi tu, hata sisi viongozi, tunachokijua ni mafuta na umeme tu.

Mimi nasema wizara hii sasa hivi igeuke kuwa ni mwalimu wa kuwafundisha watu kuanzia viongozi mpaka *grass root* nini umuhimu wa *energy*. Kama ikiwezekana na iwezekane kwa sababu ndio mipango, lazima liwe ni somo ndani ya *curriculum* zetu katika skuli, watu wakikua wajue umuhimu wa *energy* na *source* za *energy* na Zanzibar tuna *opportunity* gani za kuweza kupata *energy* kutoka *sources* mbali mbali. Kwa hivyo, nilisema kwamba hili ni muhimu na kwa kweli haitoshi kuwa sisi tu kuwa tumepitisha leo sera halafu tukaiachia tukasema sera hii ndio itafanya kazi.

Mhe. Spika, nilisema sera hii unaweza vitu vingi sana ukawa huna vya kusema kwa namna ambavyo kila kitu kimezungumzwa. Lakini kitu kimoja cha muhimu na tutakapoingia mambo ya *exploration* na hasa tutakuwa tunatumia wenzetu kutoka nje na wengine wamekwishaonesha nia ya kutaka kusaidia, sasa tunaingia katika suala la sheria za nje, mikataba ya nje. Wanasheria najua wapo katika wizara, lakini tunahitaji wanasheria *International Lawyers*, wanaofahamu sheria za kimataifa, tutaingia sio tu katika furaha ya ku-*sign* mikataba, lakini tutaingia katika migogoro mikubwa sana ya mashtaka hasa kwa sababu sisi ni wapya katika masuala hayo. Kwa hivyo, tutakuwa ni *losers* wakati tumekwishakuwa tunataka ku-*consume*.

Kwa hivyo, yote tutakayokuwa tunayafunga katika mikataba yetu lazima *International Lawyers* wamekuwa *trained*, wamepewa fursa ya kuona wengine wanafanya vipi na wana kesi zilizo hai za kuweza tukiingia katika migogoro tukaweza kui-*relive* nchi yetu katika masuali kama haya. Nimesema hilo nalo nilizungumze kwa sababu ni jambo ambalo muhimu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina fikira tu pamoja na *legislation* hii na sera hii ambayo tume-*focus* katika *energy* peke yake, lakini ikiwezekana tukiwa na sera ndogo ndogo wala mimi siziiti mipango sera yenyewe hasa ya *energy* ambayo inatokana na matumizi ya miti ingekua ni jambo la busara sana. Kwa sababu vyovyote tutakavyokwenda ikiwa leo karibu 70% tuko katika mti Mhe. Spika, hii ni hali mbaya sana na hatuwezi kugeuka nyuma hata tukifanya nini, kwa sababu kama hatukuwafundisha watu wetu matumizi mengine, lakini tukawarahisishia matumizi mengine hatuwezi kuwatoa katika kukata miti.

Leo Mhe. Spika, ipo gesi hapa nchini, hata sisi wengine ambao ndio tunasema tumekwenda skuli kidogo tunaiogopa gesi, kabisa. Tunaiogopa gesi kwa sababu ya kusikia vile vitukovyake, gesi iko hivi, iko vile, inawezekana yanayozungumzwa ikawa ni *exaggeration* katika gesi, lakini kumtoa mtu katika umeme ukampeleka katika gesi basi ni kui-*change mind set*, si vitu rahisi. Leo nimekosa mkate kesho nitakula muhogo na viazi ni vitu rahisi sana, lakini katika matumizi ya mambo ambayo yana hatari ndani yake ni ku-*change mind set* za watu.

Inawezekana leo ikawa tungekosa kuangalia mpira lakini tusingekosa watoto wetu kupata mwangaza wa kuonea mule ndani ni kwa sababu hiyo na gesi iko rahisi ukilinganisha na umeme huu, sisemi rahisi kwa maana kwamba ni rahisi, ni rahisi ukilinganisha na huu umeme , angalau. Lakini wanafunzi leo wanakwenda kuingia katika mitihani *Form VI* miezi miwili hawajasoma vizuri ni mchanga tu. Hata wawakilishi wako Mhe. Spika, tunakuja bila ya matayarisho mazuri kwa sababu hakuna usiku anayekaa kusoma vitu hivi, kila jambo limeathiri. Kwa hivyo, tu-*change mind set* za watu na hili linataka ku-*culcate education* katika masuala ya *energy*.

Nasema wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bado wana dhima kubwa katika masuala haya ili angalau yanapotokezea *interruption* ndogo ndogo mtu anaweza aka-*switch*.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, ni suala la *security* na *safety* katika masuala haya. Mhe. Spika, ukishaingia na mataifa mengine katika kutafuta nyenzo za kusaidia nchi hasa katika mafuta. Maana yake kwa upande mwengine umejitangazia vita ambavyo wewe mwenyewe huvijui kwa sababu ya choyo tu cha mataifa mengine au nchi nyengine kuhusu mafuta. *Influence* ya mataifa hayo itakuwa kubwa na. Kwa hivyo, sera zetu ziangalie namna ambavyo tunaboresha mashirikiano yetu ya nje na mataifa makubwa ambayo yametangulia katika mafuta.

Kwa kiasi gani Zanzibar itakuwa ina-*say* katika mashirika makubwa ambayo yanatoa mafuta tusije tukayaacha mambo yakaja yakatuvamia kumbe tulikuwa na njia ya kuweza kujipenyeza na sisi tukawa ni sehemu yao. Hili ni jambo muhimu sana na hilo suala la *safety* ni pamoja na suala la mazingira ni mambo ambayo lazima ndani ya wizara kuwe na kampeni maalumu kwa wananchi wetu kufundishwa namna ambavyo wanaweza wakalizingatia suala la *safety* katika maisha yao kwenye matumizi ya *energy*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache ambayo kwa kweli nimekazia nguvu yale ambayo yote takriban yamo, basi la mwisho kabisa. Mhe. Spika, tumelizungumza jambo kubwa mno katika uchumi, jambo hili chanzo cha kuja kwake mpaka ikawa sera hatutaki kuzungumza humu, lakini sote ni mashahidi. Kwa hivyo, tujenge mazingira ya kuendelea Wazanzibari wote bila ya kujali tafauti za siasa ku-*support* suala la *energy* katika nchi kwa sababu huu ndio ufunguo pekee wa maisha yetu kiuchumi na maisha yetu ya kijamii.

Baada ya kusema hayo, mimi nawashukuru wote watayarishaji, wataalamu, Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa sera nzuri sana na mimi naiunga mkono kwa sababu siku-*pause* hata *question* moja ambalo nataka kujibiwa, lakini angalau ufafanuzi wa mambo namna ambavyo sera hii uzuri wake utakuwa *putting to practice* ili kuona kwamba tulikokusudia kwenda tunafika kwa salama. Nakushukuru sana Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Abass Juma Muhunzi. Sasa ni zamu yake Mhe. Haji Faki Shaali na baada ya hapo Mhe. Ali Denge Makame.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru na niwashukuru wachangiaji wote waliopita kwa kweli wametufilisi sisi wengine. Namkumbuka Mhe. Said Omar aliyekuwa Mwakilishi wa Tumbe siku moja alituachia falsafa kubwa sana katika Baraza hili naikumbuka mpaka leo. Alisema "Ikishapigwa ngoma ya zumari huyo anayekuja na ngoma ya kinanda inakuwa haileti mvuto tena". Maana watu zumari imewakolea sawa sawa wameshacheza wewe unakuja na mambo ya kinanda. Sasa Mhe. Spika, watu waliotangulia wamepiga ngoma ya zumari, sisi tunaokuja tunapiga ya kinanda, lakini hata hivyo tuvumiliane. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Hiyo ni falsafa ya Mzee wa Karatu. *(Kicheko)*

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, mimi niseme kitu kimoja. Mhe. Said Ali Mbarouk, mara nyingi analeta utani katika Baraza katika vile vionjo kwamba Zanzibar ni matajiri wakubwa sana wa sera. Leo kwa mara nyengine inathibitisha ule utani wa Sheikh Said kwamba kwa kweli Zanzibar Mhe. Spika, lazima tukubali kama alivyozungumza Mhe. Abass Juma Muhunzi kuwa

sera zetu kwa maandiko basi hata akija mtaalam kutoka wapi kuzikosoa inakuwa shida sana. Lakini changamoto ya sera zetu iko katika utekelezaji.

Kwa sababu ukiangalia Mhe. Spika, kwa miaka mitano hapa au zaidi kidogo nyuma sera tulizozipitisha katika sekta mbali mbali za maendeleo, lakini ukiangalia na hali halisi hailingani. Sitaki kusema sera gani labda tuliyoipitisha na mambo yakawa mabaya, kila mmoja atatumia akili yake au atakwenda kuangalia katika *shelf* yake, utaziangalia sera kwanza tumezipitisha halafu uangalie na uhalisia wa mambo ulivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, changamoto iliyopo sasa ni kuhakikisha kwamba hizi sera ambazo tunazipitisha katika Baraza lako tukufu basi zinafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Lakini bila ya hivyo, basi tutabakia na uzuri wa maandiko, lakini mwananchi wa kawaida hahitaji maandiko. Mwananchi wa kawaida analohitaji ni umeme sio *document* hii. *Document* hizi tukizipeleka majumbani kwetu watu wanaweza wakazichukua wakafungia sambusa au kachori hawajui umuhimu wake. Wao wanajua umuhimu wao ni umeme na nishati nyengine wanayoihitaji, hii *document* haina umuhimu kwa watu, hii ina umuhimu kwetu sisi watungaji wa sheria na katika serikali. Sasa Mhe. Spika, changamoto iliyopo tena ni kubwa sana katika utekelezaji.

Mhe. Spika, nije pale wenzangu wawili ambapo wamelizungumza na hii nadhani kila mmoja lazima atazungumza, hii katika hoja ya 3 "Kubadilisha matumizi ya nishati inayotokana na kuni na kuanzisha kichocheo". Mhe. Spika, kwa kweli sasa hivi hali hasa Pemba nasema mbaya, maeneo mengi miti inamalizika na majangwa yanakaribia kwa nguvu sana. Lakini Mhe. Spika, licha ya umaskini kama alivyozungumzia Mhe. Abass Juma Muhunzi mazoea.

Mhe. Spika, nafikiri watu wengi wanaogopa sana hii kwamba umezoea kitu hichi, sasa kubadilika ukenda katika kitu kingine inakuwa inajenga hofu sana kwa watu, sio suala la gesi tu na umeme kila kitu kwa kweli. Hata wazee wetu zilipokuja hizi skuli wanatwambia, mimi baba yangu bahati nzuri alisoma skuli ile ambayo sasa hivi ni Polisi Mkoani, lakini baba yake akamtoa kwa hofu tu kwamba huyu mwanangu sasa atakuwa mkristo apelekwe Unguja. Sasa hofu zikitawala katika mioyo mara nyingi zinaturudisha nyuma katika maendeleo, maendeleo mengi tunayakosa kutokana na hizi hofu.

Lakini wengine wanaogopa kwamba anakwambia aaa mimi nisipotumia kuni sitopata matandu, maana yake Mpemba akila wali kama hauna matandu haoni raha na gesi halina matandu. Kwa hivyo, kubadilisha *mind set* za watu ni tatizo, iwe mambo ya kiuchumi, mambo ya kisiasa, mambo ya kijamii *mind set* za watu kuzibadilisha ni tabu. Hata kama mtu ataliona hili jambo ni zuri, lakini ule woga utamjia tu atasema naogopa gesi nitaungua. Hili ndio tatizo letu.

Mhe. Spika, nije katika hoja ya 5 ya sera "Uhakika wa Ugavi". Hapa katika mkakati sisomi yale yaliyomo katika kiboksi naanza katika ule mkakati. Mhe. Spika, sera hii inaliagiza Shirika la Umeme kuandaa mpango wa dharura wa kudhibiti hali ya umeme pale itakapotokea kukatika kwa umeme.

Mhe. Spika, hili tumelizungumza sana. Sasa nadhani tulipolizungumza kwanza labda lilikuwa gumu kutekelezwa kwa sababu hatuna sera. Lakini imani yangu sasa maadam sera ipo labda hamu ya kutekelezwa itakuwa ipo. Maana hili suala tumelizungumza muda mrefu zaidi ya miaka mitano kwamba lazima tuwe na majenereta ya akiba. Nataka niinukuu *hansard* ambayo sina hapa lakini naikumbuka. Siku moja Mhe. Spika, nilisema kwamba "Katika siasa hakuna rafiki wa kudumu wala hakuna adui wa kudumu". Leo tunaiondoa Tanzania Bara tunaweza tukaelewana kesho tusielewane. Kitu kama hicho niliwahi kusema.

Mhe. Spika, mimi nilipozungumza miaka mine nyuma nakumbuka kuhusu suala la kuwa na majenereta ya akiba wala sikujua kama *lines* hizi zitakufa, lakini niliangalia mambo tu ambayo yanaweza yakatokea katika huu urafiki wetu na wenzetu, kumbe Mwenyezi Mungu kajaalia limetokezea jengine. Kwa sababu siku zile ilikuwa tunazungumza jambo ambalo halimo katika sera, lakini sasa hivi maadam limo katika sera ni imani yetu kwamba serikali labda tukisema itatukubalia kwa kuwa limeshaingia katika sera. Pengine siku zile ingeonekana hii si sera yetu, tukifanya hivi itakuwa si sera yetu, lakini maadam sasa hivi ni sera yetu sote basi na imani yetu kwamba hili suala litarekebishwa.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la kutafuta njia mbadala ya kurejesha umeme. Mhe. Spika, njia mbadala Mhe. Abass Juma Muhunzi kazitaja nyingi, kataja *G. O. Thermal* ambayo nafikiri hapa sijui kama inawezekana, lakini kaitaja. Nafikiri *G. O. Thermal* zaidi katika watu walioko katika *Rift Valley* katika *East Africa* ndio uwezekano ni mkubwa zaidi, sijui hapa hali ikoje.

Mhe. Spika, mimi ninachokizungumza kwamba lazima tuwe na njia nyengine na tusitegemee huu umeme wa kutoka Tanzania Bara. Kwa hivyo, ombi langu Mhe. Spika, hata Pemba baada ya kupata ule umeme wa kutoka Pangani Tanga, basi naomba yale majenereta mabovu yakarabatiwe ili ikitokezea dharura tusije tukapata matatizo kama yaliyokikumba kisiwa cha Unguja. Kwa sababu Unguja baada ya kuletwa umeme ule, watu hawakufikiria hata siku moja kwamba itakuja tabu majenereta sijui yako wapi leo ndio shida kama hii.

Mhe. Spika, ombi langu na hili nasisitiza sana kwamba yale majenereta yaliyoko Pemba pamoja na ubovu wake yatafutiwe vipuri yakae *stand by*, ili siku yoyote itakayotokea dharura tutapata japo siku moja moja huo wa vivunge

kupigia pasi nguo zetu. Umeme wa Pemba ni wa kupigia pasi na kuchajia simu tu lakini unatusaidia.

Mhe. Spika, kama nilivyosema napiga kinanda ngoma ya zumari imekwisha nije katika hoja ya 9 "Utafutaji wa kiwango cha kutosha cha hifadhi ya mafuta na gesi asilia". Mhe. Spika, hapa hoja ya sera iko wazi, hizi kama ni kur-ani tunasema *Ayat Muhakamat* sijui *Mutashabihat* au sio Mhe. Rashid Seif Suleiman, yaani aya ambazo ziko wazi wazi kabisa hazihitaji kupata tabu katika tafsiri zinajitafsiri wenyewe.

Lakini zaidi Mhe. Spika, mimi kilichonifurahisha nasema tumekwenda mbali na tumewatangulia wenzetu Watanzania Bara kwa hili. Pale tulipolipa uwezo Baraza letu kuthibitisha mfumo wa mikataba yote ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Nasema hili tutakuwa tumewatangulia wenzetu wa Bara.

Kwa sababu Mhe. Spika, mimi nafuatilia sana mijadala ya Bungeni, Wabunge muda mrefu wana kilio cha kutaka mikataba yote ile ya gesi, mafuta, dhahabu na madini mengine wayaone, lakini mpaka leo wameshindwa kuiona mikataba. Mzee Visenti mkali sana hataki yaonekane mambo haya na wenzake. Lakini sisi Waziri wetu kathubutu kuliweka wazi na mapema suala hili. Kwa hivyo, hapa Mhe. Mansoor Yussuf Himid anaziba kabisa mwanya wa watu kuja kufunga mikataba mibovu.

Sasa Mhe. Spika, kama kuna jambo la kumpongeza Mhe. Mansoor Yussuf Himid na serikali kwa ujumla ni hapa. Kwa sababu mamlaka haya ukayakabidhi kwa Baraza ya kuthibitisha kuidhinisha hii mikataba hata kama kuna watu mafisadi katika wizara kidogo wanaweza wakarudi nyuma. Nasema hili ni jambo moja ambalo mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, hii ni njia moja nzuri sana ya kudhibiti ufisadi katika hatua za mapema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakwenda kwa haraka haraka kwa sababu nasema mengi yamezungumzwa na wenzangu sitaki nipoteze muda sana, nije katika hoja ya 18 ya sera "Ubora wa nishati katika sekta ya majumbani, biashara na taasisi".

Mhe. Spika, tamko linasema "Zanzibar lazima iwe na mkakati wa matumizi bora ya nishati kwa sekta zote za kiuchumi na kijamii ikijumuishwa utoaji sahihi wa mwamko katika kuelekeza faida juu ya matumizi bora ya nishati".

Sasa katika ile mikakati pana mkakati wa pili unasema "Kushajiisha uingizaji wa vifaa bora vya nishati ikiwemo taa zinazotumia kiwango kidogo zaidi cha nishati".

Mhe. Spika, hapa ndio nilipokuwa nataka nizungumze. Mhe. Spika, ukenda Shirika la Umeme pale Gulioni katika ubao pale wameweka taa balbu hizi za kawaida na hizi zilizoingia siku hizi sijui zinaitwaje za *coil* zile, sasa kila moja wamekuwekea na pesa wanakwambia ukitumia hii *unit* 100 utalipa kiasi hiki na ukitumia hii *unit* 100 utalipa kiasi hiki. Sasa mwananchi anaiona ile tofauti ni kubwa mno ukitumia hizi taa zilizoingia siku hizi na hizi za zamani mabalbu haya tunayotumia.

Lakini sasa suala linalokuja wananchi wanakosa elimu. Hivyo, ni watu wangapi wanaokwenda pale wakaweza kusoma wakafahamu lile tangazo. Bado wananchi wanashikilia mabalbu yale ya kizamani. Mimi bahati nzuri zote nimetoa katika nyumba yangu sina hata moja na nimeona ile faida yake.

Lakini Mhe. Spika, nasikia sina uhakika Mhe. Waziri atanisahihisha kama ni kweli au si kweli. Nasikia wenzetu Serikali ya Uganda wamekwenda mbali zaidi, wametoa taa hizi bure kwa wananchi wote kwa kuanzia ili kuhamasisha watu watumie taa hizi. Haya mabalbu ya kizamani yamepigwa marufuku kwa sababu yanatumia umeme mkubwa. Kama hili ni kweli kwa nini sisi muda wote tushindwe kulitekeleza hili, hata kama tusiwape wananchi bure, lakini angalau kupita tukatoa ile elimu wakafahamu, wanaweza kwenda kulipa bili ya umeme pale lakini hawafahamu kitu. Mhe. Spika, mambo kama haya ndio nasema kubakia katika mabuku yanakuwa hayaleti faida sana kwa wananchi, mahitaji ya wananchi hasa ni utekelezaji.

Mhe. Spika, jengine wakati tunahamasisha watu wasikate kuni, basi vile vile tuihamasishe serikali na Shirika la Umeme nalo lipunguze bei. Mhe. Spika, leo kuunga umeme ni ghali mno, kama nguzo ipo mita moja tu kutoka kwenye nyumba yako gharama zinafika shilingi laki tatu. Hivyo, kweli mwananchi wa kijijini atakuwa na uwezo huo.

Mhe. Spika, kilichopo sasa hivi katika nchi yetu unaweza ukakuta vijiji vingi vina umeme, lakini katika kila kijiji kizima pengine kina watu wanne wanaotumia umeme. Hili ni tatizo kwa sababu serikali inatumia gharama kubwa sana kuupeleka umeme katika vijiji, lakini ukenda watumiaji katika vijiji ni wachache. Sasa kwa nini wanakuwa wachache?

Kwa sababu mwananchi umwambie shilingi laki tatu, tena hata ile sera ya kusema kwamba mtu alipe kidogo kidogo sasa hivi haitakiwi. Zamani nasikia angalau ilikuwa mwananchi anaweza akalipia kwa *installment* mpaka akamaliza, lakini sasa hivi unaambiwa ulipie zote kwa pamoja, mita unaambiwa ununue, kama una ile kongwe inabadilishwa basi pia unaambiwa uinunue. Sasa kwa kweli haya mambo tunayafanya magumu, huku

tunahamasisha watu kwa maneno, lakini kivitendo tunawafanya watu wasifunge umeme. Kwa hivyo, lazima maneno yetu yaende sambamba na matendo yetu.

Mhe. Spika, jengine nirudi kidogo katika mafunzo tuliyoyapata kutokana na wafadhili wetu wa Norway. Yote waliyozungumza Wanorway katika semina yetu ya mafuta Mhe. Spika, huwezi ukayaingiza katika sera, lakini nasema yanatosha kuwa sera tuliyoyapata humu katika semina ya Wanorway. Mazingatio makubwa tuliyoyapata katika semina ile ni haya matumizi yatokanayo na bidhaa hii ambayo bahati nzuri Mhe. Waziri kaeleza vizuri sana, hali yetu tuwe vipi. Sasa nadhani Mhe. Waziri yale makaratasi anayo, atakuwa akiyapitia mara kwa mara. Masuala ya mazingira nafikiri vile vile Mhe. Waziri kayaeleza katika *document* yake hii atakuwa anayaelewa vizuri sana.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumze kidogo ni huu utekelezaji ambao Mhe. Waziri ameuanza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa katupa taarifa kwamba anaandaa vijana kuwapeleka masomoni. Katutajia fani gani wanakwenda na *inshaallah* niwatakia kheri waende wasome wafanikiwe, warudi wajenge nchi yetu. Lakini Mhe. Spika, hapa mimi nitoe angalizo na mapema.

Mhe. Spika, fursa tumepewa na serikali hiyo ambayo ametutajia, lakini hofu yangu kwamba hawa vijana watakwenda watasoma watarudi tuwa- *misuse* watukimbie. Kwa sababu tunayo mifano mingi. Mhe. Spika, Zanzibar sasa hivi ina wataalamu wengi sana nje ya nchi na wengine huwezi ukaamini kwamba hawa ni Wazanzibari.

Mhe. Spika, sisi tuliobahatika kutembea japo nchi mbili tatu tunaona hii hali, tunaona hazina ya Zanzibar inavyopotea. Lakini usiende nje ya nchi nenda hapo Tanzania Bara, nenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nenda Chuo Kikuu cha Dodoma, nenda Chuo Kikuu cha Morogoro ile *Islamic University,* wahadhiri pale sijui ni asilimia ngapi Wazanzibari. Ukiwauliza kwa nini mko huku sio kwamba hawapendi kukaa hapa, lakini maslahi duni au kuwa *ill-treated* mtu. Kuna ma-*professor* sasa hivi na ma-*doctor* wengi mno.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naweka mkazo sana hapa kwa sababu naogopa sana kwa juhudi aliyonayo Mhe. Waziri sasa hivi na ameshamkabidhi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amtafutie vijana wakasome nje. Vijana hawa wanarudi hapa tunawachezea wanatukimbia, wameshasomeshwa kwa mamilioni ya pesa za nchi iliyotusaidia. Sasa itakuwa tumefanya nini? Mhe. Spika, nasema yanatia uchungu sana, hakuna kitu kinachotia uchungu kuona kwamba mnasomesha watu kwa gharama kubwa sana matokeo yake mnawa-*ill treat* wanakimbia mnabakia na watu ambao wa kupapasa papasa tu.

Sambamba na hili Mhe. Spika, pia nataka nimuombe Mhe. Waziri kitu kimoja. Katika hii juhudi ya kutafuta watu kwenda kusoma nje asiwasahau na wafanyakazi wake ambao muda mrefu wapo pale. Kuna haja ya kuwa- *upgrade* wafanyakazi wake kwa sababu Waswahili wanasema "Usiache mbachao kwa msala upitao". Sasa Mhe. Waziri ana wafanyakazi katika Idara yake hii ya Nishati pengine muda mrefu, kama mtu anayo *degree* yake moja basi fursa hii na yeye apewe akajiendeleze. Lakini atajisikia mnyonge kuona wanaletwa wafanyakazi wapya wakati wao pale wameachwa.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kutoa fursa kwa vijana wapya, lakini wafanyakazi wake alionao katika sekta zake kuna haja nao kuwaangalia. Kunakuwa na malalamiko sana katika Shirika la Umeme na katika taasisi mbali mbali za wizara yake kwamba watu wanasahauliwa katika suala la kujiendeleza kielimu.

Mhe. Spika, la mwisho nizungumze kitu ambacho juzi kimejitokeza kwa namna nyengine na leo kimejiingiza katika sera. Sera katika ukurasa wa 11 *paragraph* ya 3 kutoka juu inasema, "Matumizi fanisi ya nishati yanategemea sana juu ya ubora hasa magari makubwa na magari madogo katika Sekta ya Usafiri. Matumizi ya idadi kubwa ya vyombo vikongwe vya usafiri Zanzibar inapelekea matumizi makubwa ya suala zima la bidhaa za mafuta na athari zake mbaya kwa mazingira na hali ya hewa ya dunia. Vifaa kama vile majiko, mafriji na viyoyozi vilivyozeeka mara nyingi vinakuwa sio fanisi na havina faida ya kutosha kwa mtazamo wa nishati.

Mhe. Spika, hivi juzi tulikuwa tunazungumzia mabadiliko ya Sheria ya Tume ya Utangazaji ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna, bahati mbaya mwenyewe alikuwa hayupo. Sasa katika kuzungumza tukatoa mifano ya mambo kama haya, haikuwa ndani ya sheria yake *actually*, lakini pia tulitoa mifano kama hii na leo bahati nzuri yamejitokeza katika sera.

Mhe. Spika, hili suala muda mrefu linazungumzwa kabla hata hii sera yenyewe kuja. Sasa sijui mawaziri waliohusika walikuwa hawataki kutusikia kwa sababu sera ilikuwa haijasema au vipi. Lakini leo bahati nzuri sera imesema hapa kwamba haya magari mabovu yanayoletwa katika nchi ni tatizo, viyoyozi vibovu ni tatizo, mafriji mabovu ni tatizo, makuka mabovu ni tatizo. Sisi hatukuangalia mtazamo wa kinishati, ilikuwa tunaangalia mtazamo mmoja wa kimazingira. Lakini sasa Mhe. Waziri hapa leo katuletea katika mtazamo mwengine wa matumizi ya nishati.

Sasa Mhe. Spika, ikiwa katika sera jambo hili limezingatiwa nadhani mawaziri itakuwa hawana sababu tena tukiwaambia mambo haya kwamba kidogo

yadhibitiwe, tena itakuwa hawana namna ya kutwambia bla bla. Nadhani itakuwa nguvu za utekelezaji zipo kwa sababu sera tayari ipo, iliyobakia labda kama sheria hamna ni kufanya sheria mambo haya yakatekelezwa kwa haraka.

Mhe. Spika, kweli mimi nakubaliana na Mhe. Waziri, wala siangalii katika suala la umeme kwamba unakwenda mwingi tu, lakini suala kubwa hasa ninaloliangalia ni mazingira. Mji ukipita sasa hivi umejaa madubwasha mabovu haya yaliyochukuliwa kwao kuja kuyatupa hapa yanachafua mji, halafu mengine yana masumu mabaya watoto wanachezea. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa hili kwamba katuingizia katika sera. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika mkakati kasema "Kushajiisha uingizaji wa vifaa bora vya nishati" ambayo nimeshaizungumza hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo kama nilivyozungumza mwanzo "Ngoma ya zumari ikipigwa, ngoma ya kinanda inakosa ladha" lakini nadhani mchango wangu umekidhi haja. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Zipo dakika kama 10. Nadhani tuje jioni tu moja kwa moja ambapo tutakuwa tunaanza na Mhe. Ali Denge Makame nilitangulia kumtaja mapema, anafuata Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Ali Abdalla Ali na wengine ambao watapata baada ya hapo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji Ali Abdalla Ali nimeona jina lako hapa, yupo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Nipo.

Mhe. Mwenyekiti: Maana yake nimeona jina lako hapa. Lakini mimi nimeambiwa watu wawili tu, nimeambiwa Mhe. Abubakar Khamis Bakary na Mhe. Ali Denge Makame.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, tulipoondokeana hapa Mhe. Spika alikwishamuarifu Mhe. Ali Denge Makame jioni atakuwa ni wa mwanzo.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa jioni hii kunipa nafasi ya mwanzo kuchangia sera hii ya nishati. Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote kwanza niwashukuru Mhe. Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri pamoja na

watendaji wake wote, lakini zaidi Mkurugenzi wa nishati kwa fani yake kubwa aliyokuwa nayo na utaratibu wake na utulivu wake mkubwa anaoongoza idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tunatembelea katika shughuli zetu za kamati. Kwa hivyo, niliona ufanisi wake kwa sekta mbali mbali za uwekezaji jinsi alivyokaribisha na kuleta maslahi, manufaa kwa serikali hii na kuingiza mapato. Kwa hivyo, kwa hilo Mkurugenzi nampongeza sana kwa juhudi hiyo aliyochukua pamoja na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kuchangia sera hii kwenye ukurasa wa 5 kifungu cha 2(1) kuhusu tathmini ya hali ya nishati Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi umefika wakati mzuri na muafaka kwa kuileta sera hii ya nishati katika Baraza ili kupata kuichangia na kuipa baraka zake.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki cha sera kuna mambo mengi tu yaliyokuwa yameandikwa na baadhi yake mengi yameshazungumzwa. Kwa hivyo, na mimi nitazungumza machache kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya watu wengi wa Zanzibar inategemea kilimo kwa ajili ya maisha yao. Jambo hili Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi, baadhi ya wanakijiji wetu wengi mtizamo wao mkubwa uko katika kilimo cha aina mbali mbali. Ukulima wa mazao ya kutegemea chakula, ukulima wa kupata vitu mbali mbali vya kutoa nishati inayotumika ndani ya majumba mbali mbali.

Lakini tatizo kubwa tulilokuwa nalo maeneo ya kilimo katika nchi yetu ni madogo sana. Mtu kama analima kilimo cha mazao ya kula, basi wengi wao ni kilimo cha kuwasaidia wao wenyewe binafsi tu, kubwa na kumsaidia jirani yake. Lakini baadhi ya wakulima wengi hawana ule ukulima mkubwa wa kupata mazao wakauza nje ya nchi na mengine wakatumia kwa maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, hii yote inakuja kulingana na hali ya maeneo yetu ya ardhi ni madogo sana. Kwa hivyo, ukulima wa kujitegemea wa kufanya biashara nyingi ukatumia na nyingine ukapeleka nje kunakuwa na upungufu. Ukulima hasa mkubwa kama wa biashara ilikuwa kama mtu anamiliki melitano au melikumi za maeneo ya kilimo tu, ndio utakuta mtu yule anapata ziada ya kusafirisha nje na mengine ya kutumia yeye binafsi. Lakini utakuta wakulima wetu wengi wanamiliki maeneo madogo tu kama heka tano, tatu au masafa ya meli moja.

Mhe. Mwenyekiti, masafa makubwa kwa kweli hatuna mengi ya kutosha kama hivyo, isipokuwa ukulima mkubwa ambao una masafa makubwa kidogo ni ukulima wa mazao ya mkarafuu ambapo humo ndio tunapata mazao ya kuuza

nje na mafuta ya kutumia katika shughuli zetu mbali mbali. Upungufu wa maeneo yetu ya ardhi ndio yanayosababisha kuchangia umaskini katika masuala ya kilimo na kupata baadhi ya nyenzo za nishati kwa kuwa maeneo madogo. Kwa hivyo, utakuta hata wale wanaopanda miti kwa ajili ya kupata kuni au makaa wanakuwa na maeneo madogo sana hayatoshelezi, ndio baadhi ya wafanyabiashara wengi huwa wanatumia nishati hizi kuzitoa nchi jirani.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa masuala ya maeneo ya kilimo kama hayo. Hivyo, kuna haja Mhe. Waziri na taasisi husika watafute miundombinu mingine ili kukuza masuala ya kupunguza umaskini kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja zaidi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili na Idara ya Nishati kutilia mkazo zaidi maeneo ya bahari kuu yasiyo ya Muungano, kwa kuwa huwenda tukapata wafadhili wa nishati ya umeme wa kutumia mawimbi. Kwa hivyo, pindipo maeneo haya ya bahari kuu kama yatatolewa katika masuala yaliyokuwemo ndani ya Katiba ya Muungano.

Kwa hivyo, itatusaidia wananchi wetu ajira pindi tukiwapata wafadhili mbali mbali wa kuekesha mipango ya nishati ya umeme unaotokana na mawimbi au utafutaji wa nishati nyengine zinazopatikana kwenye bahari kuu, hii itasaidia wananchi wetu kupata ajira na kuondokana na kupungua umaskini. Lakini ikiwa maeneo haya bado yatakuwemo ndani ya shirikisho la Muungano. Kwa hivyo, itakuwa hakuna uhuru wa kuyatumia ili wananchi wetu wakafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoeleweka visiwa vyetu hivi havina mzunguko mkubwa wa miradi, miradi yake mikubwa tutegemee katika masuala ya uvuvi, bandari, utalii. Lakini masuala mengineyo kama zilivyo nchi za wenzetu za jirani jinsi walivyokuwa na njia na nyenzo nyingi za kujipatia maisha, Kwa hivyo, sisi tuna usumbufu mkubwa.

Suala hili Mhe. Waziri, nitaomba uliangalie sana ili lipatiwe ufumbuzi kwa kuwa dalili ya mwanzo hapa imeshaonekana kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Kikwete, kuwa suala letu kubwa tulilokuwa tukilalamikia hapa liondolewe katika masuala ya Muungano, suala la uchimbaji wa gesi na mafuta. Kwa hivyo, hili limeshakuwa na kufanyiwa masawazisho kuondoshwa. Kwa hivyo, lisiwe hilo tu, yatizamwe na masuala mengine yaliyokuwa yanatusaidia kibiashara katika nchi yetu ili kufufua uchumi wa nchi.MKwa hivyo, nayo yaondolewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda mrefu tokea Muungano, tumevumilia vya kutosha zaidi ya miaka kumi nyuma.Hivyo, sasa hivi tumeshakuwa makini kwa kujiendesha na kutumia rasilimali zetu tulizokuwanazo kwa faida ya wananchi

wa Zanzibar na hata Tanzania kwa jumla. Kama inavyoeleweka baadhi ya miradi mingi ikiekeshwa hapa, watumiaji wa miradi hiyo sio wa Zanzibar peke yao hata nchi jirani nao huwa wanatumia miradi hiyo. Kwa hivyo, tukipata fursa hii ya kuachiwa baadhi ya shughuli muhimu kama hizo za biashara au za uwekezaji, basi itasaidia kuondosha umaskini na kuondoa kero mbali mbali kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 16 kifungu cha 4 katika mwanzo wa kuanza dira ya 2020 tulibuni mambo mengi tu ikiwemo sera ya nishati. Tulibuni mambo ya biashara, utalii na kilimo. Baadhi ya mengi sasa hivi yameshafikia hatua nzuri ambayo inaonekana, sasa hivi 2020 tumefikia 2010. Kwa hivyo, *Inshaallah* kama tutakuwa makini na kuangalia zaidi katika masuala haya ya nishati na hususan nishati ya gesi asili, huwenda tukifika 2020 tutakuwa tuna msimamo mzuri wa kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe kigezo kimoja tu kwa kutumia mfano wa nchi jirani, kwa ruhusa yako nitaomba nizungumzie hapa. Kuna baadhi ya nchi jirani kama Afrika ya Kusini, kuna kipindi katika TBC kama siku ya tano leo, kuna mwandishi wa habari kule alitembelea kwa kipindi kirefu na kuangalia hali ya maendeleo na uchumi jinsi unavyoboreshwa. Kwa hivyo, utakuta wenzetu wamefika hatua ya mbele zaidi kutokana na mambo ya uwekezaji kama wa mahoteli, utalii na uchimbaji wa madini.

Utakuta sekta nyingi zinakwenda vizuri na kila sekta imepangiwa wasimamizi wake na kila msimamizi ikifika mwaka anatoa maelezo jinsi utaratibu wa ile sekta yake jinsi unavyoendelea. Kwa hivyo, utakuta mambo mengi yanakwenda kwa mpango kwa mujibu yalivyopangwa. Hata ukija kwenye masuala ya wananchi katika kujisaidia miradi midogo midogo, ndio mara nyingi wanawezeshwa kwa mipango ili wapate kujinyanyua na shughuli zao zinakwenda vizuri.

Kwa hivyo, na sisi juu ya udogo wa nchi yetu, viongozi wetu wanajitahidi kuboresha mambo mbali mbali, nitaomba kutilia mkazo zaidi ili na sisi tujitahidi kuzidisha uadilifu na uaminifu ili masuala haya yaende kama yalivyopangwa ndio tutaondosha makero na mapungufu mbali mbali ambayo yanawakabili watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lengo mahususi ya mkazo ni mahitaji ya nishati katika ukuaji wa sekta ya uchumi Zanzibar ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar, tukifanikiwa ndio wananchi wetu Zanzibar na Bara watafaidika katika miradi yao mbali mbali. Kama nilivyoeleza mwanzo kuwa sasa hivi mategemeo ya nyenzo hizi tulizokuwa tukizitumia na uwekezaji tuliokuwa tukiutumia sasa hivi utakuwa umezidiwa na idadi ya watu. Ukija kwenye

mahoteli sasa hivi kumeshakuwa na upungufu, ukija kwenye kilimo kumeshakuwa na upungufu. Kwa hivyo, kuna haja tuangalie zaidi kwenye uwekezaji mkubwa kama wa bandari kuu tuliyoizungumza hiyo ya maruhubi, uwekezaji wa bahari kuu. Tukibuni huko basi tunaweza kupata viwanda ambavyo vitasaidia kwa wananchi kupunguza umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 18 kifungu cha 5.0 nishati ya kuni. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wengi wanatumia nishati hii ya kuni toka hapo kale. Kwa hivyo, utakuta kuna upungufu mkuba kwa nishati hii ya kuni kulingana na mazingira ya nchi yetu na udogo wake ulivyo, kwa kuwa wengi watu wa vijijini na mijini matumizi yao makubwa mara nyingi ni kuni.

Utumiaji wa kuni huu Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi huwa unaleta athari kwa wananchi wetu, kwa kuwa kuni hizi huwa zinatumika kwenye mabekari, vikosi, mahoteli, na majumbani. Lakini tatizo lililojitokeza sana watu wetu wengi ukipita mitaani unapata taarifa ya kuwa wanaathirika na matumizi haya ya kuni, kwa sababu kuni kama zinavyoeleweka zinatokana kwenye miti ya aina mbali mbali. Baadhi ya miti mingine inajulikana kuwa ni dawa na mingine inakuwa na sumu. Kwa hivyo, wananchi wetu wakiipata miti ile wanaifanya kuni na kuitumia kwa kupikia na miti ile inatoa moshi na moshi ule hatujui baadae utaleta madhara gani kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi utawasikia baadhi ya wafanyakazi wanaofanyabiashara zao za kupanga samaki, maandazi na kwenye mabekari huwa wanaathirika kwa moshi unaotokana na kuni hizo. Wanaathirika mapafu au mishipa mbali mbali, wanapata mafua. Kwa hivyo, utakuta kuni hizi ingawa wengi wanazitumia lakini ukitizama zinaleta athari kama hizo, baadhi ya watu wengi utawasikia yule kaathirika kwa moto au moshi unaotokana na kuni.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akawa anatoa maelekezo mazuri zaidi kuwafahamisha wananchi wetu kuwa sasa tubadilike, baada ya kutumia nishati hii ya kuni kwa muda mrefu, sasa tutumie utaalamu huu wa kileo ambao unatokana na gesi asilia na vifaa vyenginevyo ili kupunguza athari inayotokana na nishati hii ya kuni. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri wa nishati akatoa maelekezo mazuri ili kuwafahamisha wananchi wetu ili kupunguza matumizi ya kuni kwa usalama wa maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi cha nyuma hapa Mhe. Waziri Kiongozi alitoa tangazo la kuzuia utumiaji wa mifuko ya plastiki ambapo mifuko ile moshi wake ulikuwa unaathiri sana wananchi wetu, ingawa wengi tulikuwa tunapenda kutumia kwa kurahisisha kuwasha moto, lakini kumbe hatujui kama unaleta athari moshi wake kwa maisha ya binadamu. Kwa hivyo, toka kuzuiwa mifuko ile,basi imenusuru watu wetu wengi kupata athari hiyo. Hili nalo ningemuomba

Mhe. Waziri aliangalie zaidi katika kutoa hamasa kwa vyombo vyetu vya habari na hili litapunguza uharibu wa mazingira kwa kukata miti na kutumia nishati hii ya miti kwa masuala ya kupikia na matumizi mengineyo ndani ya majumba.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la gharama za utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia. Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi fulani Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi, ilitembelea katika Bodi ya TPDC, nashukuru tulipokelewa vizuri na Mwenyekiti wa bodi kwa kipindi kile alikuwa anaitwa *Major General Boma*. Namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, huyu alitupokea kwa nia nzuri na alitufahamisha mengi tu ambayo yalikuwa yanapatikana katika gesi asilia hii na faida zake.

Kwa kweli alitupa ukweli na uwazi uliokuwepo, kuwa gesi asilia ikitaka kutafutwa basi wanatokeza wafadhili wanakubali kuitafuta na kuchimba kwa gharama zao. Kwa hivyo, kwa masuala haya inaonesha dhahiri kwamba na sisi hapa tutakapoanza huwenda na sisi tukapata baraka ya kuwapata wafadhili wa kuweza kuchimba gesi asilia hiyo, ili na sisi tufaidike na wananchi wetu kuitumia na kupunguza uharibifu wa mazingira na kuwaweka katika afya nzuri.

Vile vile, tulipata maelekezo na kupelekwa katika kisiwa kinaitwa Songosongo, tukaoneshwa jinsi ya uchimbaji wa gesi ile na faida yake. Kwa kweli tulifarajika sana kwa sababu tuliambiwa wanakijiji wa kisiwa kile wote wanaotaka kuunga umeme ni bure, hulipii ukishaunga umeme unatumia bure, kulingana na kisiwa chao kimepatikana nishati hii ya gesi ambayo inafaida nzuri tu. Hata maji ya mifereji ni bure na misaada mingi tu wanapata ya kujengewa maskuli na zahanati kutokana na faida ya uchimbaji wa gesi hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningeomba suala hili aliangalie zaidi, pindi na sisi tukifanikiwa basi itasaidia kupunguza umaskini na kuboresha shughuli mbali mbali za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoeleweka gesi asilia ina faida nyingi tu. Sasa hivi wenzetu wameshakuwa wanaitumia kwa kuendeshea magari, hata kwa kuendeshea viwanda mbali mbali. Wenzetu wanaitumia gesi hii ni kama umeme wa kuendeshea viwanda vyao. Pindi na sisi tukilisimamia suala hili katika kipindi hiki hadi tukifanikiwa, basi katika ule mpango tuliouanza wa dira 2020 tutakuwa tumebuni kitu ambacho ni tegemezi kwa wananchi wetu ili kujiondoshea umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sera hii mimi imenipa uchangamfu mzuri, kwa maelezo yote yaliyokuwa yameandikwa katika kitabu chake hiki, ni maelezo mazuri tukiyaangalia na kuyasoma na yakija kufanyiwa kazi, kwa kweli yatatusaidia katika mambo yetu mengi ya kimaendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hii sera mimi naiunga mkono kwa kushirikiana na wananchi wenzangu wa Jimbo la Amani mia kwa mia na Wajumbe sote tuipitishe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo tu katika suala hili la sera ya nishati. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa ni mdogo na zaidi ni baadhi ya mapendekezo ambayo naamini wenzetu hawa ikiwa wataona yanafaa, basi wanaweza wakayachukua kwa kusaidia kuboresha sera hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze katika ukurasa wa 28 wa sera yenyewe, kifungu 7.1, kwenye hoja ya 9 ya sera hii, katika vile vijumba, kijumba cha 2 kinasema:

> "Zanzibar itaimarisha na kusimamia ugunduzi kwa juhudi zote, uzalishaji na kusambaza gesi na bidhaa za mafuta. Ugunduzi na uzalishaji huo utatilia maanani hali ya kimazingira, kijamii na kiuchumi"

Na kijumba cha 1 kinasema:

> "Zanzibar itaanzisha mazingira yake ya kisheria na usimamizi kwa ajili ya uchunguzi zaidi na utafutaji na itahakikisha udhibiti wote wa hifadhi ya mafuta katika maeneo yake yakiwemo maeneo maalum ya kiuchumi"

Mhe. Mwenyekiti, suala ninalotaka kulizungumza ni suala hili la maeneo ya kiuchumi. Kuna sheria nambari 3 ya mwaka 1989 ambayo inazungumzia *territorial sea* na *exclusive economic zone.* Sheria hii ni ya Jamhuri ya Muungano na sheria hii katika kifungu cha 1(2) kinasema kwamba:

> "*This Act. Shall extend to Zanzibar".* kwamba sheria hii itatumika mpaka Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo yaliyozungumzwa katika sheria hii ni mambo mawili. Kuna suala la *exclusive economic zone* na kuna suala la *territorial sea*. Sasa hizi zote kwa mujibu wa sheria hii ni maeneo ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tujuwe tu kwamba suala la mafuta ni suala ambalo si kwetu sisi tu, lakini hata kwa hao ambao wameshaanza kupata mafuta, basi inaleta mgongano sana na inaleta ugomvi. Sasa sheria hii inaweza ikatusababishia matatizo. Kwa hivyo, ningependa kujua wenzetu wizara

wemefanya nini kwa sababu katika hii sera mimi sikuona hatua ambazo zinaweza zikachukuliwa ili kuepusha matatizo haya. Kwa sababu ukizungumzia suala la *exclusive economic zone* ambayo ni meli 200 kutoka ufukwe wa bahari, meli hizo kwa sababu ukichukua Tanzania kama ni moja, ukitoka Chwaka kuendelea mbele kule ndio unaanza meli 200, eneo lolote lilioko baina ya Dar es Salaam na Chwaka lile ni *territorial sea*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika suala hili, kwa mfano mafuta ambayo sasa ni yetu na yameonekana Chumbe au yameonekana Chwaka tuseme meli 2 kutoka ufukwe wa Chwaka, wakati huku tunasema ni yetu, lakini huku kuna sheria inayosema maeneo yale ni ya Muungano. Sasa sisi tumejiandaa vipi katika sera hii ili kuondoa matatizo kama hayo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima linalozungumzia *equidistance principle*, sijui hii limezungumziwa vipi katika utaratibu huu, kwa sababu hapa sikuiona. *Principle equidistance* kwa mambo ya bahari inasema kwamba kama nchi mbili zimepakana. Kwa hivyo, nchi mbili zile maeneo yao au lile eneo la bahari sio kubwa sana. Kwa mfano baina ya Dar es Salaam na Zanzibar. Kutoka Dar es Salaam mpaka Unguja hapa ni meli kama sikukosea ni 22 za bahari, sasa *distance principle* inasema kwamba kila mtu atachukua meli 11. Sasa hii imezingatiwa vipi?

Kwa mfano ukichukua meli 11, kuna maeneo mengine ambayo Zanzibar ni zaidi ya meli 11. Kwa mfano kuna kisiwa kinachoitwa Latham Ireland, kisiwa hiki ni cha Zanzibar na hii iko karibu sana na Dar es Salaam, tunasema hivyo kwa sababu nchi hata ukitizama kwenye makaratasi yaliopo ni kwamba kisiwa hiki ni chetu. Mfano kisiwa kile kiwe kimegundulikana nishati ya mafuta *principle* gani iliomo kwenye sera ambayo itatuhakikishia kwamba mafuta yale yaliopo katika kisiwa kile ni ya Zanzibar au utaratibu gani ambao umewekwa katika sera ambao unahakikisha kwamba yale yote ambayo yatapatikana yanaweza yakawa ni mali ya Zanzibar?

Halafu pia kuna suala la *internal water*, sasa haya maji ya ndani sio mito au maziwa, lakini ni yale maji ya bahari ambayo yako ndani ya visiwa au kwenye bara. Kwa hivyo, maji yale yatagaiwa vipi?

Kwa mfano kuna eneo katika maeneo hayo yamegundulikana nishati hii ya mafuta, hapo hapo ukilinganisha na suala zima la ule upana wa *territorial sea* ambayo ni meli kumi na mbili kutoka *low water mark* ya Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo nadhani yangeliwekwa uzuri katika sera hii ili yakaweza kutusaidia hata katika kutunga sheria zetu ambazo baadaye zitatungwa. Kwa hivyo, tukesha kuyajua na kuyaweka kwenye sera,

nafikiri yatatuharakishia au yatatufanyia mambo yetu kuwa rahisi katika utungaji wa sheria unaohusiana na matatizo haya.

Hivyo, namuomba Mhe. Waziri au wizara kwa jumla kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ikatuelezea kidogo kwamba kuna utaratibu gani, ambao wamechukua katika suala hili la *Exclusive Economic Zone* pamoja na *Territorial Sea*, ambazo nazo ni muhimu kwa taifa letu.

Ninavyofahamu Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Tanganyika ni nchi peke yake na Zanzibar ni nchi peke yake, kwa bahati mbaya Tanganyika imepakana na Zanzibar.

Kwa hivyo, kisheria hii *Exclusive Economic Zone* kwa Tanganyika katika maeneo yale yanayoanzia Kaskazini ya Pemba mpaka Kusini Unguja itakuwa hawana *Economic Zone*. Isipokuwa *Economic Zone* ile itakuwa ya Zanzibar. Je, hii tumeiweka vipi katika sheria yetu, ili iwe wazi katika suala hili?

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba wenzetu wanafahamu suala hili, lakini ni vyema tukaiweka kwenye sheria au sera, ili sisi tukajua pamoja na vizazi vyetu navyo vikajua. Kwa kweli hili ni suala muhimu ambalo ningependa kupata ufafanuzi juu ya sera yenyewe. *(Makofi)*

Lakini zaidi katika sheria hiyo Nam. 3 ya mwaka 1989 inasema kwamba Waziri ndiye atakayeweka mipaka ya zone hizi ambazo tunazizungumza. Katika suala hili Waziri anakuwa *referee* kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. kwa kweli hakuna hata pahala pamoja ambapo atleast Waziri angekuwa anamshauri Waziri wa Zanzibar katika masuala haya. Sasa je hili nalo linawekwa kwa utaratibu gain?

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka nilizungumze wakati Mhe. Hamad Masoud Hamad ambaye ni msemaji wa Kambi ya Upinzani alilizungumza katika ukurasa wake namba 3, alisema kushajihisha wananchi wengi kuunga umeme kwa matumizi ya nyumba, Shirika la Umeme halina budi kupunguza masharti magumu na gharama za uungaji umeme majumbani, ambazo kwa sasa ni kubwa mno na zinakwazwa juhudi za wananchi wanyonge kujiungia umeme.

Kwa kweli nataka nimuunge mkono. Isipokuwa tatizo ninalodhani ni kwamba Shirika la Umeme lingejaribu kujirekebisha, ili haya matatizo ambayo naamini wanaweza kuyatatua, yaani wakayaondoa na wananchi wakashajihika katika kuunga umeme. Kwa mfano wakati wanapounga umeme kuna kuwa na tofauti kubwa sana ya jinsi umeme unavyoungwa kwa Unguja na kule Pemba, halafu tofauti hizi hata za ulipaji.

Tukiangalia Mita za TUKUZA unalipa kwa kadri unavyotumia. Kwa hiyo. unaweza kununua umeme wa shilingi 30,000/- kwa Unguja na kutumia, lakini unapokwisha kutumia kama utamaliza leo, kesho au baada ya miezi sita. Hivyo, wakati unapokwenda utanunua umeme unaotaka na wala hakuna suala la kulipa mita kwa mwezi katika ile miezi ambayo hujatumia umeme. Mhe. Mwenyekiti, sijui vipi labda kuwe na sababu ambazo sizifahamu, lakini ni tofauti na hali halisi.

Kwa mfano Pemba ukinunua umeme wa shilingi 40,000/-, basi unaweza kutumia miezi sita au saba, lakini ukifika mwezi wa saba unapokwenda kununua unatakiwa ulipe miezi saba ile shilingi 1,500/- mara 7 na wala sijui kwa sababu gani.

Kwa kweli nalizungumza hili kwa *experience*, kwani mimi mwenyewe nimeshalipa katika nyumba yangu hununua umeme miezi mitatu au minne. kwa hiyo, ule umeme unaweza kukaa mpaka siku unapomaliza, unapokwenda basi kwanza utoe gharama zile za miezi mitatu au minne ambayo hukununua. Kwa mfano Januari, Febuari, Machi na Aprili, inamaana kila mwezi wanavyotaka wende ukanunue, vyenginevyo kama hukununua unakuwa *charged* mwezi mmoja kila siku na wala sijui kwa sababu gani au kuna kitu gani ambacho kinafanya hivyo. Hili nalizungumza *with experience.*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kwa wale ambao hawana mita za TUKUZA, tatizo ni baadhi ya wafanyakazi wakati wanapotumwa kwenda kutizama umeme, basi hawendi au wanakwenda sehemu nyengine na baadhi hawendi na matokeo yake wanakuletea bili ambayo ni kubwa sana na *experience* hiyo ninayo.

Katika nyumba yangu ya shamba kwa mfano *bill* ambayo imeletwa kwa miezi miwili ambayo sikuwepo walileta shilingi 70,000/- labda waliona kwa sababu ya lile jina, kwamba huyu atakuwa na *computers*, *television* pamoja na vitu vyengine, jambo ambalo si kweli.

Kutokana na hali hiyo wao wanakisia tu na kuleta *bill* ile ya shilingi 70,000/- nyumba ya shamba kwa sababu ya jina, pengine umeme uliotumiwa hata gharama za shilingi 10,000/- haufiki na wala hakuna chochote kinachotumika. Sasa nalo hili linawavunja moyo sana wale watu ambao wanataka kuunga umeme, tukiacha gharama kubwa za ulipaji wa uungaji wa umeme.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa kile alichokisema kuwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar litathibitisha mfumo wa mikataba yote ya utafutaji wa mafuta na gesi. *(Makofi)*

Kwa kweli hili ni suala zuri sana napenda kumpongeza, lakini naomba tuongeze hapo kwamba si lazima iwe ni suala la utafutaji wa mafuta na gesi tu. Isipokuwa ni mikataba yote inayoambatana na masuala haya yawe ya mafuta, gesi na umeme kwa sababu mikataba ni uzuri kwa Baraza la Wawakilishi kuiridhia.

Kwa hivyo, tusiwe kama wenzetu Mhe. Mwenyekiti, wakati mikataba yote ya mambo yote haya hayajaonekana wala hawataki yapite katika Bunge na ndio maana karibuni tukapata lile suala la *Richmond* na kama hayo, kwa sababu gani? Kwa kuwa mikataba iliyofanywa imefanywa na watu wachache wenye *interest* zao, mikataba hiyo hata mtoto wa skuli wa darasa la nne atajua kwamba ikiwa mimi tumekubaliana na wewe ufanye kitu fulani na ikiwa kitu kile hukukifanya basi wewe ndio unawajibika kulipa, huo ndio utaratibu wa mkataba.

Sasa hawa waliokubaliana kuleta umeme kule na wakenda *to the extent* kwamba ikiwa yule ambaye ametakiwa atoe umeme na akashindwa kutoa, basi yeye ndio alipwe gharama zake za kukaa hapa. Kwa kweli hii ni kizungumkuti na matokeo yake ikiwa kila siku moja si chini ya shilingi milioni 100 ambazo serikali inatoa kwa watu kama hawa. Kwa hivyo, namshukuru Mhe. Waziri kwa kujaribu sana kama anavyoweza kuondoa ile tunayoweza kusema *Richmond* na *Mansoormond*. *(Kicheko)*

Kwa hivyo, hili ni suala zuri sana ambalo naunga mkono moja kwa moja. Lakini hapa lazima sheria hizo ziwe si kwa haya masuala ya utafutaji wa gesi na mafuta na hata ile mikataba ambayo inahusiana na *production* ya mambo hayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo napenda kulisisitiza ni kuhusiana na vifaa vinavyoletwa kwa ajili ya kuwarahisishia watu wetu. Kwa kweli vifaa vinavyokuja vingi ni *substandard*. Sasa je, wizara kwa kupitia shirika wanao mpango gani wa kuvifanyia uchunguzi vifaa hivi angalau kwa wale wateja wanaonunua na wakaridhika kidogo. Kwa sababu masikini ya Mungu mtu ambaye yuko kijijini anaponunua kifaa, basi kifaa kile ni siku mbili tu kinaharibika. Kwa hiyo, ni kumvunja moyo mtu kama huyo.

Nadhani kama kungekuwa kuna chombo angalau cha kujaribu kufanya au kutafuta ama kuweka utaratibu wa kuvikagua hivi vifaa ambavyo vinavyoleta na vinavyohusiana na kuwekwa na hapa ni masuala ya umeme tu, lakini hata kwa mambo mengine.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema suala hili kwa kweli tunajaribu kuboresha tu sera hii. Nafikiri niwakumbushe katika sheria zetu za Zanzibar ambazo ziko tatu kama sijakosea, yaani kuna Sheria ya *Mining, Mineral Oils* na *Regulation Mineral Oil* kwenye *Chapter* ya 106, 107 na 108.

Sasa hizi zipo ni sheria zetu tokea enzi za zamani kwa ufahamu wangu sheria hizi bado hazijafutwa. Je, tumeziangalia katika kuboresha sera hii na hapo ambapo wakati tunayo azma ya kufanya sheria, basi sheria hizi tutazifanya vipi au zitatusaidia kwa kiwango gani katika kuboresha zaidi Sheria hizi za *Mining* na mambo yanayohusiana na hayo. Kwa sababu sheria hizi bado ni zetu na wala hazijafutwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nazo sheria hizi wenzetu hawa wazitizame ili kwa kupata mwelekeo zaidi katika masuala hayo.

Kwa hayo, machache kama nilivyokwambia Mhe. Mwenyekiti na mimi niunge mkono hii hoja, lakini *atleast* nifanye *observation* zilizo ndogo kwa faida ya sera pamoja na wizara kwa jumla kwa ajili ya kuziangalia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ile nyumba ya shamba au *beach* uliyopata *bill*, si ya *beach* ni ya shamba. Ahsante sana Mhe. Mjumbe. *(Kicheko)*

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu katika kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kututayarishia sera hii. Lakini napongeza zaidi kwamba Baraza hili pamoja na serikali kuweza kuzinduka, kuwa kumbe tulikuwa na maradhi makubwa ya kutokujua uhai wa taifa letu ni umeme hatuna miliki nao ni *petrol* na wala amri nayo. Kwa hivyo, Baraza hili limefika mahala na kusema iwe iwavyo, lazima suala la mafuta na umeme liwe chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa kweli ni hatua kubwa kwa sababu tukiangalia sera hii kuna sehemu inasema bila ya umeme na *petrol* uchumi mzima unaporomoka, kila sekta utakayoishika. Kwa mfano ukitaja afya utakuta wagonjwa hawawezi kufanyiwa *operation*, maji na umeme, maji hayapo kwa sababu hakuna umeme, yaani kila sekta utakayoishika utaona aidha inahitaji *petrol* au umeme.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema umeme kwa serikali ni sawa na damu mwilini hata kama utakula biriani na kuvimbiwa ikiwa unalo tatizo la damu, basi

chakula hakitotembea mwilini na kila ukipimwa utaonekana afya yako nzuri, lakini unao upungufu wa damu. Kwa hivyo, taifa umeme ni upungufu wa damu.

Wenzangu wamezungumza mengi na wala nisingependa niyarudie tena labda *context* ndio naweza kubadilisha. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba vizuri tukakumbuka kwamba dunia nzima vita vinavyopigwa, vilivyokuwepo duniani hivi sasa. Kwa mfano tukisikia vile vya Iraq, Afghanistan, kule Nigeria Agony na alivyotaja Mhe. Abubakar Khamis Bakary, nimekumbuka hivi sasa kuna tofauti fulani kati ya Kenya na Uganda kuna kisiwa katikati pale ambacho kimeanza kuzaa ugomvi kila mmoja anasema cha kwake, suala lote hilo kwa sababu kuna harufu ya mafuta.

Kwa hivyo, utaona kwamba dunia nzima vita vyengine vina sababu ya ukabila, lakini vita vingi hivi sasa duniani ni wakubwa kutaka kumiliki nishati ya mafuta.

Iran hivi sasa ina ugomvi mkubwa na mataifa ya Magharibi, inajaribu kutumia nguvu za *nuclear* kujenga viwanda vya umeme kwa ajili ya maendeleo yao, lakini wakubwa wameshituka wanafikiria kwamba wanafanya mambo mengine.

Hivi karibuni kulikuwa na maelezo mengi hapa Serikali ya Muungano kwamba tuna *uranium* nyingi sana, hilo wakubwa haliwatishi, siku tutakayosema tunachukua *uranium* kutaka kujenga viwanda vya kufua umeme ugomvi unaweza ukaanza. Kwa ufupi ninalolisema kwamba nishati ya umeme na mafuta ni moja katika vianzio vikubwa vinavyosababisha vita, aidha vya wenyewe kwa wenyewe au wataalamu wanaita *Geo Politics*, mvutano wa mataifa makubwa.

Kama mta-*notice* hivi sasa China imepata hamu sana ya kuongeza mahusiano yake na nchi za Afrika. Hivi sasa China ni rafiki wa Sudan, China sasa inaingia Congo, China ina mashirikiano na Angola, yote ni kutafuta uwezekano wa kuwa karibu na nguvu za nishati *petrol* msingi wake.

Kwa hivyo, na sisi tuelewe hivyo, kwamba tunapofurahia kuwa Mwenyezi Mungu atupe mafuta na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatupa, lakini tunahitaji kujiandaa katika hali hiyo ya dunia. Mwenyezi Mungu atuepushe na balaa hilo.

Suala la pili nililotaka kuzungumza ni kwamba sera hii ukurasa wa saba kwa lugha ya Kiswahili kuna kama keki pale imekatwa nzuri tu. Keki ile ni keki inayoonesha aina ya nguvu za nishati tunazoziingiza kwa matumizi yetu. Wenzangu asubuhi nadhani Maalim Rashid Seif alisema 79, lakini mimi

nasema ni 82. Kwa sababu 54 ni kuni, 3 ni mabaki ya kilimo na 25 ni makaa, zote baba mmoja mama mmoja.

Sasa kama nchi 82 ya nishati yake ni kuni basi hiyo ni hatari hata kama makaa mengine tunayatoa Bara, lakini maana yake huko Bara kuna miti inakufa. Mhe. Mwenyekiti, tumeambia kwamba si chini ya hekta tano za mwitu wa hapa visiwani inakatwa kila mwaka. Nilikuwa na mtaalamu mwenzangu hapa Mhe. Hamad Masoud Hamad tukafanya *calculation* hizo ni *square* kilomita ngapi? Kwa wastani ni *square* kilomita tano, yaani kila mwaka zinakwenda tunazitafuta kwa makaa au kuni zinazopikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sasa umeme labda ungesaidia kubadilisha hiyo hali ni asilimia nne na *petrol* ni asilimia 14. Kwa hivyo, umeme na *petrol* vyote hatuna na tunategemea watu wengine. Nadhani nilieleza kwamba sasa tunahitaji kuamua katika taifa hili *priority number one* ya nchi hii ni kitu gani?

Kwa hivi sasa tunahitaji kuamua *priority number one* nishati na jinsi tutakavyoweza kujirekebisha tukawa na miliki nayo. Kwa sababu kuwa na miliki nayo, angalau kuwa na maamuzi ya kusema hili ndilo na lile silo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati fulani nilikuwa nikisoma Japan, basi waliniambia hivyo kwamba mahitaji ya nchi ni mengi, lakini lazima wakati mmoja mnasema hili kwanza na wala sio mengine yasubiri, lakini mnasema hili kwanza. Kwa hivyo, mwalimu wangu aliniambia ingekuwa ni kama mtu unayetembea kwenye barabara au unaendesha gari na kuiona *pole*, kwa mfano tunaelekea Makunduchi, yaani unaiona mbali na baadaye ukiipita unaiangalia kwa nyuma na ukiangalia mbele unaiona nyengine ya pili.

Kwa maana hiyo, kuna haja ya kuangalia mahitaji yetu kwa mpangilio wa umuhimu katika hali hiyo, yaani tuseme hasa kwamba hili *Alhamdulillah*. Baadaye tunaangalia jengine lipi, barabara pia tunafika mahala tunasema hili *Alhamdulillah*, tunaangalia la tatu sasa nini hospitali au elimu. Mhe. Mwenyekiti, haina maana tunapofanya hivyo yale mengine si muhimu, lakini lazima tujiamulie.

Kwa kweli mimi mwezi mzima najiuliza na kumuomba Mwenyezi Mungu atunusuru na wala sina nia mbaya Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa jumla, ingekuwa tuko kwenye vita hali hii ingekuwaje. Kwa sababu askari wetu wanataka kusonga mbele wanaambiwa *petrol* hamna, basi wacha taa *generator* haliwaki, hali hii ni ya hatari sana.

Kwa hivyo, naomba kutoa ushauri Mhe. Mwenyekiti kwamba Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na kuwa tumeziruhusu kampuni binafsi, lakini tunahitaji kuwa na *National Reserve* ya *Petrol*, angalau pale wananchi wanapokosa *petrol* au wanayo nusu nusu, lakini shughuli za serikali pamoja na vituo muhimu viwe vinapata huduma bila ya matatizo. *(Makofi)*

Vile vile, nimeambiwa kuna mtu mmoja binafsi anajenga *reserve* Mangapwani na wala sina hakika ni sehemu gani kwa sababu sijafika. Lakini *reserve* hiyo inahitaji kuwa kubwa kiasi angalau tuwe tunaweza kusema kwamba tunayo *petrol* ya mwezi mmoja au miwili kwa ajili ya matumizi bila ya matatizo.

Ushauri wangu ni kwamba tutafute moja kati ya visiwa hivi vya *Prison Island* au chengine badala ya kufanya visiwa vya kwenda kufanya starehe na watu kupiga *disco*, tukasema hiki ni kisiwa kwa ajili ya kujenga *tanks* ya *National Reserve* kwa ajili ya taifa hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwamba sawa raia wetu wanatumia kuni na kuua miti. Nakumbuka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipoingia madarakani mwaka 2005 moja katika vitu alivyoviona vinaathiri mazingira ilikuwa ni ukataji wa miti kwa ajili ya makaa. Sijui alipata washauri gani akaja kuzuia makaa yasije Dar-es-Salaam. Hivi mnakumbuka ile hali ilikuwaje.

Kwa kweli ilikuwa ni *crisis* kubwa sana. Kwa hivyo, kutoka pale kibati cha makaa Dar-es-Salaam kilitoka shilingi 200/- mpaka 700/-. Sasa huku tulifikia tunaikinga miti isikatwe, lakini huko ikawa tumefungua *switch* ya kupandisha maisha ya masikini. Kutokana na hali ile makaa yalipanda bei na ikawa balaa Dar-es-Salaam na baadaye ikanyamaza kimya na wala haikuendelea tena.

Nakumbuka Waziri wa Fedha wa Muungano alisema tutaongeza gesi na tutaifanya rahisi, pia tutafanya mafuta ya taa yawe rahisi. Hivyo, haikuwezekana kuwa rahisi na ikawa gesi haipo, mafuta ya taa ghali na maisha ya masikini yakawa magumu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukitaka kuwasaidia masikini, basi lazima mafuta ya taa yawe rahisi na kama inawezekana gesi ambacho ni kitu kipya kwa Wazanzibari kutumia na wala sio wengi wanaoweza kutumia nyumbani. Kwa mfano leo Mhe. Mjumbe mmoja alisema tunaiogopa gesi na mimi ninaiogopa sana kwa sababu akinamama siwasemi vibaya, lakini hadhari ya gesi kama huko *careful* mtaungua nyote.

Pengine mama anaweza kuifungua na huku anazungumza masuala ya harusi, basi kesho njoo harusini haya nitakuona na anapopiga wanawaka wote na hiyo

ni hatari. Isipokuwa nilichogundua kwamba wale wataalamu wanaoshughulikia nishati ya gesi siku hizi wanahakikisha kwamba kile kifungulio cha gesi ndicho kibiriti, kwa maana hiyo, kidogo hatari ile imepungua. Kwa hivyo, kama mipango itaanza kufanya kampeni ya kutumia gesi labda gharama za kutumia makaa zinaweza kupungua. Kwa hivyo, tunaona sote ukosefu wa mafuta ya taa, ukosefu wa umeme ndio maisha ya jamii yetu yamepanda ghafla. Ndio maana nikasema kwamba umeme ni damu ya taifa.

Kwa hivyo, moja katika njia pekee ya kuwasaidia masikini maisha yawe rahisi ni kupata mafuta rahisi na umeme rahisi, lakini je, tutaupata umeme rahisi na mafuta rahisi? Kwa sababu kodi za mafuta na umeme hatuna mamlaka nazo wanaoamua bei ya mafuta ni Dar es Salaam tunakokwenda kununua labda zile meli zinazochukua mafuta moja kwa moja kutoka Mombasa, hasa nikitoa mfano wa umeme.

Mhe. Mwenyekiti,umeme unaotoka *TANESCO* tukichukua kama ni bidhaa una gharama iliyoingizwa ya uzalishaji umeme, halafu kuna gharama za uendeshaji, halafu kuna kodi zinazoingizwa pale, halafu wanaweka kitu kinaitwa faida. Kwa hivyo, tunajua madudu yale ya *IPTL*, dudu la *Richmond*, *DOWANS*, gharama zote hizo zinazojazwa kwa mchanganyiko wa yale madudu yanakuwa *duded* kwenye *price*. Mhe. Mwenyekiti,yanapoingia *ZECO* nao wanakuja na gharama zao. Kwa hivyo, mtumiaji wa umeme wa Unguja anabeba gharama zote ambazo hazimuhusu, madudu ya *TANESCO* yaliyokuwa hayatuhusu ndewe wala sikio anabebeshwa mlaji wa umeme.

Kwa hivyo, kupunguza bei ya umeme kwa Wazanzibari sio jambo rahisi, ni jambo ambalo mpaka pale tutakapokuwa na sisi tuna njia ya kupanga bei zetu wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nasikia huwa mnajadiliana na wenzetu kuhusu bei na wakati mmoja niliona kwenye magezeti kwamba bei ilitaka kufika 700, lakini umasikini wa Wazanzibari sababu yake moja ni gharama kubwa za matumizi ya nishati. Tangu juzi nilikuwa nawatafuta watu wa takwimu wanisaidie wanipe ile *price index* ya matumizi ya nyumbani kwamba umeme unagharimu kiasi gani? Baada ya chakula, dawa, pesa za watoto za skuli, nauli ya watoto kwenda skuli na kurudi na umeme, kodi ya nyumba pengine itakuwa ya kwako japo matofali hayana *plaster*.

Mhe. Mwenyekiti, pale nyumbani kwangu ninavyojua tunanunua *unit* za umeme, tunanunua makaa na tunanunua mafuta ya taa. Mhe. Mwenyekiti,yote hiyo ni katika kujaribu kutaka ku-*balance* gharama hizo. Kuna wakati tulikuwa tukitumia *cooker* tu wala hatujali, lakini mambo yalipokuwa magumu inabidi tukatafuta makaa yawepo akiba, lakini ni kwamba lazima ufuate mafuta, lazima upate makaa na lazima upate umeme. Hiyo ni gharama kubwa sana kwani kodi hatuna milki nazo na hilo ni tatizo kubwa kwa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, tukisema tuendelee kukata kuni basi kila mwaka *five kilometer squares* zinakwenda, tukisema tuendelee kutumia mafuta hali zetu ni ngumu, ufumbuzi wa haya ni nini? Ni kushirikiana kuhakikisha kwamba tunapata mafuta yaliyo rahisi na umeme ulio rahisi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nililotaka kulizungumza ni suala linalosema kulinda maafa. Mhe. Mwenyekiti,hebu twendeni mpaka pale Mtoni jamani tuyatizameni yale matangi, *audhubilahi mindhalik* itokee hasara ya moto. Hivyo tuna *fire brigade* ya kuzima yale, mimi sijui, lakini najua ipo Idara ya *Fire Brigade*, lakini ni kweli tunayo magari yakutusaidia kukabili hatari ya aina hiyo. Hii inanikumbusha wakati fulani niko masomoni Ulaya nilikuwa nakaa jirani na kiwanda fulani cha madawa. Moja katika zile ghala zake zilikuwa na dawa inaitwa *phosphorus* wengine mliosoma *Chemistry* mnaijua. Dawa hiyo ni aina fulani madini ambayo kila mara inabidi yawekwe ndani ya mafuta lisitokeze hata nje kupata hewa, ikipata hewa inawaka wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti,kwa bahati mbaya nadhani ikaja likawaka, sisi tulikuwa tunakaa jirani ni masafa kidogo, lakini tukawa tunaona yale mambo yanaanza. Wenzetu mawasiliano yako sahihi pengine kila nyumba ukenda unaambiwa *in case for fire*, basi mimi nikanyanyua simu kupiga, kubwa nilichoulizwa uko wapi na uko *street* gani unaweza kutwambia hilo. Nikawaambia niko mahali fulani na mtaa fulani hapo jirani pana kiwanda cha madawa. Waheshimiwa Wajumbe nakwambieni kweli hazikufika hata dakika 15 walifika hapo. Mimi najiuliza hawa walikuwa wapi mbona wamefika upesi. Kumbe ule mji mzima ile *system* ya *fire* imegaiwa kwa *zone*. Kwa hivyo, nilipopiga simu nilikuwa katika *zone* fulani.

Kwa hivyo, sio kwamba lile gari limetoka tuseme hapo Maisara sio hivyo, kama mimi nakaa Malindi basi hapo kuna *sub-zone* ambayo inalinda usalama wa eneo lile. Mhe. Mwenyekiti,basi hazikufika dakika 15 nasikia wanakuja, baada ya pale kwa sababu niliwaambia ninapokaa wakanigongea tukasalimiana baadae wakanipa fomu pale nikajaza kwamba nimeona moto unawaka kwenye kiwanja wakati huo wameshazima. Mhe. Mwenyekiti, hali tuliyonayo hapa Zanzibar hatuna hilo ndugu zangu na Mwenyezi Mungu anatunusuru kinaungua kijumba kimoja, vinaungua vijumba viwili, lakini tunapoweza kupata *disaster* ya mafuta inaweza ikawa balaa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri sera yako inasema kwamba utashirikiana na sekta nyengine, nadhani suala la usalama wa jinsi ya kukabili majanga haya ni muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na tabia nzuri ya kufanya sera, mimi kwa wakati fulani nilikuwemo serikalini nikasaidia. Lakini moja katika tatizo letu kubwa kama walivyosema wenzangu kwamba tukeshakutunga sera inakuwa aidha ni

document ya *reference* au *document* ya kueleza katika bajeti kwamba nimekamilisha sera na sasa sekta yangu ina sera. Lakini moja katika kazi ngumu ya kutengeneza sera ni kupanga jinsi ya kutekeleza. Wataalamu wa *strategies* wanaita *Time Action Plan* (*TAP*). Kwa hivyo, Mhe. Waziri tuna tatizo la umeme na kwa sasa hapa ndio kubwa pamoja na kwamba la petroli, lakini la umeme ndio kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika umeme kwa muda tunajipa moyo kwamba Pemba tunao ule unaotoka Tanga na Unguja unaotoka Bara. Lakini hizi hazijawa ufumbuzi wa matatizo yetu ya kudumu. Kwa hivyo, tunahitaji kuanzia baada ya kupitisha sera hii ukakaa na wataalamu wako mukayaweka yote yale yanayohusu dhamana zenu halafu mkajiuliza hivyo katika haya lipi la kwanza na lipi la pili mpaka mkafika mwisho. Hili la kwanza tutalitekelezaje katika mfumo upi na kuanzia lini? Mkimaliza hiyo, mnamuendea bosi hapa Mhe. Waziri wa Fedha mnamwambia kwamba mambo haya ili Wazanzibari wapate nafuu ya balaa hii angalau ikifika mwaka 2013 liwe hili tayari, hili liko njiani na hili linafuata. Mhe. Mwenyekiti,vyenginevyo tutafika tena mwaka 2015 tuanze kuulizana mbona hatuna umeme, ni vizuri hilo likafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, pamezungumzwa hapa kuwa na nishati mbadala na hizi ziko nyingi sana. Vile vile, wakati wa Sherehe za Mapinduzi tulialikwa na Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii tukenda kufungua Kituo cha Utafiti wa Malaria pale Mwanakwerekwe. Alituhadithia tu kwamba kituo hiki tusikione leo kimefika daraja hii, lakini kilianza kwenye kibanda pale Afisi ya Panya. Mhe. Mwenyekiti, leo baada ya miaka kumi au kumi na tano tumeweza kujitafakari kwamba tuna kituo cha *research* ya malaria na ahadi aliyoitoa pale kwamba watajitahidi ifike siku iwe kituo kile cha *research* ya malaria dunia nzima ije kututizama.

Mhe. Mwenyekiti, kama suala la malaria tumeliweza, kwani yana athiri maisha ya watu na watoto wetu, lakini malaria haiwezi kufanyiwa *research* kama hakuna umeme. Kwa hivyo, tunahitaji nalo kuzingatiwa kuwa na kituo cha *research* hata kama tutaanza kwa milioni moja. Nasema hivyo nina mifano miwili mmoja siusemi maana nikiusema nitawashitua wale wengine wakaja kutuchanganya. Nilishafanya mawasiliano Dar es Salaam nikifika nitamfuata.

Kuna mzee mmoja hapo Dar es Salaam nimeshamuona ametengeneza mashine anasema kwa kutumia hewa baridi, yule mzee akaulizwa hewa baridi ndio nini? Kumbe ni *oxygen* na akaliweka dudu pale anaonyesha kabisa ana *compress* hewa kwenye *cylinder* anaipeleka mahali anai-*release*, ana-*inject* anawasha moto madudu yanafanyakazi. Alikuwa ni mstaafu wa jeshini nadhani huko kazi yake ilikuwa ni *mechanic*, lakini imeoneshwa mara mbili kwenye TV, nilitegemea siku moja nimsikie kusema nimeitwa na fulani na fulani, lakini

hakuna mwenye habari. Mhe. Mwenyekiti, lakini inaweza kuwa mwanzo ni pale tukaacha kutegemea petroli ya watu na madudu mengine haya tukatumia hiyo hewa ya Mwenyezi Mungu maana hapa kila mmoja anahewa kwa sababu kuna *oxygen twenty percent* humu ndani ikipungua tu, Mhe. Mwenyekiti, tuahirishe.

Kwa hivyo, uwezekano wa kufanya *research* kuanzia katika hali ya kawaida na kuendelea tukafanya kitu cha maana, tusijidharau, tuanze sasa, mimi siku zote husema hatujachelewa na hatukuchelewa kufanya maamuzi kwamba nishati iwe chini ya mikono yetu na hatujachelewa kufanya maamuzi mengine vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kueleza kwamba, waliosoma *geography* wanakijua *Island*, yaani ile *north pole* iko hapa wao wako hapa, mwaka mzima wako kwenye baridi, wakitaka wasitake lazima waishi na ili waishi lazima wapate ujoto ili mwili huo uwe 37.5 basi wamefikia *stage* maji, samahani mimi nimesoma *chemistry*, maji ni H_20. Wamepata na wamefanya *research* wanavunja *hydrogen* na *oxygen*, tayari wana gari na wanatumia kama nishati, *necessity is the mother or invention.*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Ali Denge Makame ndio utaalamu wake huo. Hivyo, alikuwa anasikiliza kwa makini sana. ahsante sana.

Mhe. Ali Abdala Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Sera hii ya Nishati iliyowasilishwa na Mhe. Waziri. Kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuwasilisha sera hii ambayo imefika wamati muwafaka.

Nataka niungane na wenzangu kwamba ni nzuri na popote utapoiuza itanunuliwa kwa sababu imeandikwa kitaalamu sana na mimi nilikuwa sina la kuchangia humu, lakini nimeona lazima nitoe baraka japo kwa maeneo mawili mpaka matatu. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniwiye radhi kwamba mengi wenzangu wamezungumza, lakini na mimi nitazungumza halafu nitoe mawazo yangu katika hoja hizo hizo, japo kidogo nitalingana nao, lakini nitakwenda kwenye tofauti kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, sera imetuonesha tunatoka wapi? Tupo wapi? na tunakwenda wapi? Nimefurahi zaidi kwamba sheria nyingi zikitungwa hapa zinatangulia sheria halafu sera inakuja nyuma yake, lakini cha kufurahisha kwenye upande wetu huu sera imetangulia na baadae ndio itakuja sheria.

Nadhani hapa tumekwenda vile inavyotakiwa. Sasa nashukuru na kuwapongeza kwamba, sera yetu ni nzuri, lakini pia inataka usimamizi ili tufikie kwenye malengo yetu.

Nikiingia kwenye sera nitakuja kwenye utangulizi ukurasa wa nne, *paragraph* ya pili, hapa pameelezwa sera yetu kwamba, popote pale ambapo mtatumia nishati lazima pawe na uharibifu wa mazingira. Hilo ndio kubwa sana na wenzangu waliotangulia wamezungumza, lakini na mimi ni wajibu wangu kama nina mawazo nitoe katika eneo hili. Kwa hivyo, nishati yoyote katika jamii lazima italeta athari na bahati nzuri sera hiyo nimeiona. Sasa ningeliomba nipendekeze mambo kama matatu katika eneo hili.

Kwanza, uharibifu wa mazingira lazima uzingatiwe wakati ambao tunatayarisha mikakati ya mwisho. Sasa hivi wenzetu wataalamu kwenye viwanda vyote kama kuna kiwanda kinachotoa moshi mbaya, basi kinatafutwa kitu kinakuwa kinaua ule moshi, hauenei katika maeneo mengine. Kwa hivyo, na hili la mazingira nadhani itakuwa vizuri likazingatiwa kwa nyanja zote, kwa jamii na kwa hali yenyewe katika nchi. Nadhani hapo tutaweza kufikia pahala palipokusudiwa.

La pili, wenzangu walizungumzia habari ya mikataba. Mikataba hivi sasa tuna mifano mingi hai katika nchi yetu, nchi yetu ilikuwa tunategemea sana zao la karafuu, lakini Waswahili wanasema, “Mungu akikupa kilema hakunyimi na mwendo”. Bado mikarafuu wenzetu wengi wanalima sasa hivi ushindani umekuwa mkubwa, zao limeporomoka katupa rizki ya kuendesha utalii.Utalii sasa hivi ndio sekta kiongozi tunavyozungumza wenyewe katika nchi yetu na mimi nakubali hilo.

Lakini katika uanzishaji wake tumepata matatizo mengi sana na bado yanaendelea na mengi yalisababishwa na mikataba. Watakuja wawekezaji watapatana na wanakijiji, watakubaliana, lakini wakishaanza kazi makubaliano yanabadilika. Penye njia inazibwa, huduma zinakuwa tabu sasa serikali inakuwa tunaiongezea mzigo, lakini kama tungeweka mikataba yetu mizuri huko tusingelifika. Sasa napata hamu ya kuzungumza hili kwamba kwa kuwa tunataka kulianzisha basi na haya yote tuyaangalie.

Sasa hivi wenzetu Bara wamepiga hatua kidogo, mkataba wowote wa serikali hauko siri, yaani unapitishwa kwenye Kamati za Baraza ama Kamati za Bunge na wao wanatoa mchango wao halafu baadae unaidhinishwa. Kwa hivyo, ule utaratibu wa mikataba ya siri sasa hivi umepitwa na wakati, lazima mikataba iliyokuwa halali kiserikali basi iwe wazi kama kamati yetu inayohusika na mambo ya madini ioneshwe mkataba huo katika hatua za awali na wao watoe maoni yao halafu baadae serikali ichukue mikataba na wizara kuunga mikataba

na huyo anayehusika. Kwa hivyo, naomba sasa hivi mikataba iwe wazi ili na sisi tuweze kutoa michango yetu. Kwa mfano, linapotokea tatizo inakuwa hakuna wa kulaumiwa na sisi tumeshiriki kwa niaba ya wananchi wetu.

Mhe. Waziri, sasa naliomba na hilo kupitia chombo hiki lizingatiwe kwa lengo la kuimarisha sera yetu pamoja na sheria yetu hiyo ambayo baadae tutaipitisha ya kuweza kutafuta hizo nishati mbadala.

Nikiendelea kwenye mchango wangu hapo hapo kwenye mikataba wenzetu wengi ambao wanapata manufaa katika mikataba mbali mbali, mfano kama mikataba ya hoteli za kitalii, kuna mikataba inayojazwa na wale wanajamii wakawa wanafaidika na mikataba ile. Sasa naomba na haya yazingatiwe kwamba pale ambapo patatumika basi jamii ya pale nayo iweze kupata tija kwa lile ambalo litapatikana katika eneo lile, hiyo pia itasaidia kupeleka maendeleo yetu mbele.

Wenzangu wametoa mfano, mimi pia nilikuwa katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kipindi kilichopita tulikwenda Kilwa katika Kisiwa cha Songosongo. Kule tumekuta wenzetu wawekezaji wamechimba visima sita vya gesi ambavyo tayari sasa hivi gesi hiyo imejengwa bomba maalumu inafika Dar es Salaam Ubungo inazalisha umeme, lakini na pale pale kijijini unazalishwa umeme ambao wanatumia bure wananchi pamoja na kujengewa hospitali, zahanati, yaani ukienda kijiji kile huamini kama uko kijijini au kisiwani utaona kama uko mjini, yale ni maendeleo.

Lakini pia, Dar es Salaam sasa hivi wamepiga hatua nyengine kwamba na gari pia zipo zinazotumia gesi, unafunga chombo ndani ya gari unaacha kutumia mafuta unatumia gesi yako imekwisha gesi unarejesha chombo cha kawaida unatumia petroli. Sasa kidogo wenzetu wamepiga hatua mbele. Lakini ninachoomba mimi ni kwamba gesi sielewi kuwa ni ya Muungano au ya kawaida tu hivi, sasa nadhani na sisi muda muwafaka umefika na sisi tuchimbe gesi kwa sababu wawekezaji wasije wakakaa kwenye mahoteli tu, sera imesema hapa kwamba wizara itashirikiana na taasisi mbali mbali, sasa *ZIPA* wahangaike na wao kutafuta wataalamu wa kuweza kuchimba gesi hapa na sisi tutoke kwenye tabu hii, tukipata gesi umeme utapatikana, gari itatumia gesi, tutakuwa tunapikia, itakuwa hakuna madhara.

Kwa hivyo, na hili Mhe. Mwenyekiti, naliomba sana. Sera imeeleza vizuri iko wazi, lakini na sisi tuchacharike kushirikiana na hizo taasisi ambazo zitusaidie katika kuweka sera yetu vizuri katika utekelezaji. Kwa hivyo, niliona na hilo nilitolee mawazo ili liweze kusaidia na tuweze kupata maendeleo.

Jengine sera imeeleza kwamba itatoa mafunzo ili tuwe na wataalamu wetu. Kuna mwenzangu alizungumza asubuhi hapa kwamba roho zinaumbwa na choyo na zaidi ya maendeleo. Wenzetu huko nchi za juu, sisi dunia ya tatu wanaweza kusema hee, Zanzibar hata kuchimba mafuta! Wanaweza wakatuwekea vikwazo vingi, lakini tukiwa na wataalamu wetu wenyewe tunanunua zana zetu tutaweza kwenda kadiri tunavyotaka. Sasa naomba na wataalamu kuwa ni kitu muhimu katika hii sera, tusiiandike, lakini wataalamu watafutwe.

Lakini pia, niiombe serikali kwamba nimebaini nchi yetu bado vijana wetu wengi wanasoma taaluma moja ambapo imekuwa kama mtu *dost* mguu upande. Unasoma sheria, wanasheria wamekuwa wengi unakaa nyumbani huna kazi, lakini unaweza kusoma sheria, ukasoma utaalamu wa mafuta, ukasoma *engineer*, umekosa kwenye sheria unakwenda kwenye *engineer*, umekosa kwenye *engineer* unakwenda kwenye utaalamu wa mafuta. Sasa vijana wetu hawana taaluma hizo, sasa naiomba wizara kupitia serikali tushawishi vijana wetu wasome taaluma nyingi ili akikosa huku apatie huku.

Sasa imekuwa vijana wengi wamesoma kazi, hakuna ile taaluma waliyosoma hapana cha kufanyia kazi. Naomba hilo kwa kutumia chombo hiki kwamba vijana sasa hivi wageuke wasome taaluma mbili, tatu hata nne, kakosa moja kuifanyia kazi, atapata ya pili, kakosa ya pili, atapata ya tatu. Kwa kweli taaluma nne huwezi ukakosa kazi katika nchi hii. Hilo nalo litawaondolea vijana kuzurura waweze nao kufanya kazi katika nchi yao ya kimapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka katika ukurasa huu nije kwenye ukurasa wa 6 kifungu 2(2), uiyano wa nishati Zanzibar. Wenzangu wengi wamezungumza kwamba nchi yetu ni masikini na wengi wanatumia nishati ya kuni na mkaa. Kijumla wenzangu wameshaitaja keki ishakatwa yote, mimi nabakisha sehemu ndogo tu, niimalizie. Wamesema kwamba asilimia 79 ni kutumia kuni na mkaa, lakini nadhani tuko kwenye nishati ya kupikia tu, lakini ukifuatilia utaratibu wa kuumiza miti na mazingira watu wanajengea, watu wanachonga mbao, miti hiyo hiyo sasa tukienda utakuta pengine imebakia asilimia moja ya miti yetu na ndio ukakuta sasa hivi hali ya mazingira imekuwa mbaya zaidi.

Sasa na hapa nadhani nitoe mawazo ya kuweza kutumia nishati mbadala ikapunguza pia kukata miti. Kwenye mbao sasa hivi ukienda wanaolanda mbao kutengeneza milango na madirisha ule unga sasa hivi huupati, watu wanajaza kwenye mabeseni ya mapipa wanakata wanachomeka na mti kati wakichomoa wakiwasha unaweza kuwaka kucha. Sasa wananchi ile wametafuta wenyewe mbinu za kufanya kupunguza kuathiri miti na kutumia mkaa. Nadhani kwa kupitia chombo hiki, basi naomba unga wa mbao utumiwe katika nishati ya kupikia inasaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendelea na hayo, wenzangu wamezungumzia matumizi ya umeme kuwa ni ghali na mimi nakubali umeme ni ghali kwa sababu hatuuzalishi. Lakini tayari utakuta baadhi ya visiwa sasa hivi wanatumia umeme wa *solar*, visiwa vidogo vidogo vyote kama vile Uzi, Tumbatu, lakini mpaka baadhi ya majumba mengine sasa hivi wanatumia *solar*.

Mimi nakaa kwa Said Washoto pale Amani kuna nyumba tatu sasa hivi wanatumia *solar* na hawana matatizo yoyote, anatumia simu anachaji na vitu vyake vyote ndani. Sasa ningeliomba pia katika kufuatilia mambo ya sera yetu hii yote imezungumzwa ya umeme mbadala kama *solar,* na upepo pia wako watu tayari wamefanya utafiti, lakini hawajaweza kuutumia.

Nilikwenda njia ya Chwaka kuna maeneo fulani wanapiga *pump* ya maji kwa kutumia upepo, imeunganishwa kwenye chuma fulani kimewekwa kipepeo kikubwa kikizunguka kile kinapandisha maji. Ningewaomba wataalamu katika tatizo kama hili wangeendelea na visima vyengine kufanya utafiti huu wakaunganisha tukatumia upepo. Pia,ingelipunguza kutumia majenereta.

Nadhani na hili kama serikali itakuwa na uwezo kwenye visiwa vyote ambavyo viko shamba basi wangejaribu utaratibu wa kuweka huu utumiaji wa upepo kwa kuvuta maji kwenye *pump* na kusambaza katika maeneo. Nadhani na hii itasaidia katika kupunguza umeme utumiaji wake.

Lakini suala la umeme vile vile nimeona mimi ukitumia umeme wa TUKUZA kidogo pana unafuu kwa sababu umeme wa TUKUZA unatumia kile ambacho unalipa. Lakini umeme wa kutumia mita za kawaida utakuta watu wengi wanapata athari kubwa na ndio watu wengi wakapata njia ya kuiba. Sasa ningelishauri Mhe. Waziri kama itawezekana basi angalau mji wetu wote tungetumia TUKUZA kwanza unapata pesa yako *cash*, mtu ananunua umeme ndio anatumia ukisha ananunua kuliko mtu anatumia kwanza halafu anakulipa inakuwa ni kinyumenyume. Sasa naomba kwa kuwa zoezi hilo lipo tayari, sasa hivi Bububu kumeshajengwa ofisi ya kuweza kuuza huo mradi, mfunge mita watu watumie.

Nashukuru na Mwanakwerekwe tayari imeshajengwa ofisi mnataka msambaze mita. Kwa hivyo, na maeneo mengine yaliyobakia ya mjini tungefanya hivyo ingesaidia pia usumbufu wa shirika kuibiwa. Tuongeze TUKUZA ili wananchi waweze kununua kile ambacho wanaweza kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka ukurasa huo nije katika ukurasa wa 9 mahitaji ya ugavi wa nishati. Mimi nadhani hii imezungumziwa kwamba hivi sasa na sisi

katika matumizi tuweze kutoa taaluma kwa wananchi wetu, sasa waweze kugeuka badala ya kutumia pengine nishati moja tu, sasa hivi tuanze kujaribu nishati mbadala, kama hatukutoa taaluma itakuwa kipindi kigumu wakati tukiweza kuwageuza kwa mara moja itakuwa ngumu.

Sasa ningelishauri kipindi hiki cha mpito basi taaluma ikaanza kutolewa na shirika ili watu waweze kufahamu gesi ikitokezea mtu anatumiaje na ina faida gani. Lakini ukitokea umeme wa *solar* mtu anatumiaje na una faida gani, nadhani ukifika muda mambo hayo yakishakuwa tayari inakuwa mwananchi hana tena kupewa taaluma anaingia moja kwa moja kwenye zoezi la kutumia.

Kwa hivyo, muda huu ungekuwa muda muwafaka wizara yako ikatumia maaluma kama redio, vipeperushi, televisheni kama vile wanavyofanya kutangaza mambo mengine ya TUKUZA pamoja na utumiaji wa umeme katika majumba. Sasa nadhani huu ni muda mzuri wa kuweza kutoa taaluma hiyo ili watu kuweza kuelewa na pale unapofika muda watu wakatumia kama kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuzungumza wenzangu pia wamezungumza kwamba Sekta ya Viwanda petu imekufa kutokana na tatizo la umeme. Viwanda tulikuwanavyo vingi, lakini umeme umesababisha gharama kubwa na viwanda hivyo vilivyobakia hivi sasa vinasua sua. Sasa naomba katika utaratibu wa umeme mbadala basi na sisi tungejaribu tukashiriki na taasisi nyengine tukaweza kutafuta wafadhili sasa hivi wakawekeza kwenye umeme ili kuweza kuwa tukipata umeme uliokuwa nafuu viwanda vikiongezeka basi na ajira ya vijana wetu itakuwa kubwa.

Kwa mfano Mahonda tu walima miwa ni watu 3,500 hujagusa kiwanda, sasa tukipata viwanda kama hivi vitano tu, tatizo la ajira petu lingeondoka. Ningelishauri bado wizara itafute taasisi zinazohusika kama inavyosema sera ishirikiane kushawishi wawekezaji waje kuweka petu, umeme wa njia rahisi ili watu waweze kununua na tuweze kuweka viwanda.

Wenzangu wamezungumza hapa kwamba ziko nchi watu wanatumia mawimbi ya bahari, sisi bahari imetuzunguka kila unakokwenda bahari ipo. Kama upande wa kusini bahari yetu ni ndogo, lakini upande wa kaskazini mashariki bahari yetu ni kubwa. Sasa tungeshauri na wao wangekuja wakatizama upande wa bahari kubwa kama upo uwezekano tukaweza kuweka umeme unaozalishwa kwa mawimbi. Hilo lingesaidia na pengine lingeondosha dhiki zote hizi za kufanya umeme tegemezi. Naomba na hili likiwezekana pia lifanyiwe kazi ili liweze kusaidia katika kutimiza azma ya sera yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nije ukurasa wa 26 hapa panazungumzia mikakati. Hapa pana mikakati mingi. lakini mimi nitazungumzia mkakati mmoja tu

ambao upo nambari 1, naomba ninukuu. Unasema, “kuandaa mazingira ya kisheria kwa ajili ya kuimarisha uanzishaji wa vinu vya kuzalisha umeme vya kisasa hapa Zanzibar kwa kushirikisha sekta za umma za watu binafsi”. Nadhani hili nimelizungumza kama litasimamiwa vizuri basi tatizo hilo linaweza likaondoka na likatufikisha pahala ambapo pataweza kutusaidia katika nchi yetu na kuondokana na matatizo yote yaliyojitokeza.

Mwisho kwa kuwa na mimi tayari nimeshatoa baraka katika sera hii, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii na mimi kusema machache ingawa wasemaji waliotangulia naweza kusema wamenifilisi kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, zamani nilipokuwa nikisikia neno nishati likitajwa nilikuwa nafikiria maana yake ni umeme na si jambo jengine, kumbe ni tofauti. Nishati kumbe inajumuisha kuni, mkaa, takataka za kilimo, gesi asilia na gesi inayotokana na viumbe hai, umeme, mafuta na kadhalika. Yote hiyo ni nishati. Kwa sababu ya tafsiri hii ya nishati tunaweza tukasema kwamba kumbe nishati ni jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu, kiasi ambacho kwa tafsiri ile ya kwanza ya umeme binadamu angeweza kuishi bila ya nishati. Lakini kwa tafsiri hii kumbe binadamu hawezi kuishi bila ya kuwa na nishati, ni nyezo muhimu sana.

Tunaweza kusema ni nyezo muhimu tukaigawa mara mbili kwanza inasaidia sana kukidhi mahitaji ya lazima ya mwanadamu na ndio tunaona hivi watu wanapikia, wanapata taa za kuonea majumbani. Lakini pia kwa upande wa pili nishati inasaidia sana kumuendeleza mwanadamu kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nizungumzie hili tatizo liliyopo Zanzibar sasa hivi kuwa hatuna umeme, mimi kule kijijini kwangu hivi juzi tu, kulivuma upepo na upepo ule ukenda ukausukuma mfenesi ukaangukia *wire* wa umeme. Kwa hivyo, umeme ule uliokuwa unakwenda kijijini kwetu ukawa haupatikani kama siku nane hivi mpaka tisa, kelele zilikuwa kubwa sana. Zilikuwa kubwa kwa sababu kuna watu walikuwa wanatumia ule umeme katika miradi midogo midogo tu kama ya kufanya *juice* na mambo madogo kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi walikuwa wakinung’unika sana na kwa kweli tukapiga kelele mpaka juzi nashukuru shirika limekwenda kuunyanyua *wire* ule. Hii inaonesha kwamba umeme ni nishati muhimu sana ambayo mwanadamu anaitegemea katika maisha yake.

Sera ya Nishati nitakuwa najaribu kuisoma nimeona moja katika malengo yake makubwa ni kuhakikisha serikali inatayarisha nishati ya kutosha itakayokidhi mahitaji ya jamii ya Wazanzibari. Moja katika malengo ni hilo, lakini lengo la pili, ni kulinda mazingira. Wenzangu wengi wamesema hapa na ndivyo ilivyoandikwa katika sera, ukiangalia ukurasa wa saba kila mtu ana-*refer* pale. Hiki kiwango cha 54% cha kuni na 25% za mkaa pamoja na takataka za kilimo 3% ambapo jumla inafanya 82% kwa kweli ni kiwango kinachotisha sana. Mhe. Ali Abdalla Ali kasema hapa hii ni kwa upande wa mahitaji ya kupikia tu, yaani watu wanategemea misitu kwa mahitaji ya kupikia karibu 82%, kuna wengine sijui itakuwa asilimia ngapi nafikiri watafiti wanaweza wakafanya, watu wanategemea misitu kwa kujengea.

Kule kwetu siku za nyuma nilipokuwa nikienda pwani kuchokoa pweza *Wallahi* kulikuwa na mkoko wa kutosha. Hivi karibuni nilikwenda nilikamata mikono kichwani ni jangwa kabisa, watu wamekata huku mnaita majengo sisi tunasema miti ya kujengea, kwa sababu zile nyumba za kutumia tope sio matofali watu wanaweka ile miti, sasa wamekata wengine wanapiga mkaa ilimradi sasa hivi misitu ina maadui wengi sana.

Kwa upande mwengine hatuwezi kuliepuka hilo, hatuwezi kuliepuka kwa sababu ukitafuta mbadala wa hilo ni gharama ambazo wananchi hawaziwezi, si watu wote wanaoweza kujengea matofali hapa, ukienda huko vijijini nyumba ya tofali ni adimu sana, si watu wote wanaoweza kutumia umeme, wala si watu wote wanaoweza kutumia taa za *stem* kwa kuonea majumbani.

Kwa hivyo, hili linafanywa hapa nchini si kwa hiari ni kwa sababu ya unyonge, hatuwezi kuwalaumu watu sana. Sasa nadhani ni muhimu na nafikiri ndivyo ilivyo, ukisoma hii sera imezingatia namna ya kukuza uchumi. Kwa hivyo, ni muhimu hili likatiliwa mkazo wananchi kwa kutumia sera hii ya nishati ambayo ndani yake mna jambo muhimu sana kalizungumza Mhe. Juma Duni Haji, pale kwa urefu suala la mafuta ambalo mimi naliita suala hilo ni mkombozi wa Wazanzibari. Tutakapofika kufanya utafiti wa kina na siku moja Mwenyezi Mungu akatuwezesha tukachimba mafuta na mapato ya mafuta yakawasaidia Wazanzibari, nafikiri tutaweza kuihami hii hali ya misitu kupotea namna hii.

Lakini pia, na sera nyengine isiwe ya nishati tu, lakini na sera nyengine pia zifanyiwe kazi ili kuhakikisha kama zinawatoa Wazanzibari katika hali ya unyonge huu tulionao na kuwapeleka katika pahala ambapo tunaweza kumudu kutumia nishati mbadala kwa kupikia. Kwa sababu nina hakika kwamba, Prof. Ali Denge Makame alisema hapa, ukitumia kuni unapata athari nyingi, unapata mafua, utakohoa na siku nyengine unaweza kupata hata athari ya mapafu kwa sababu ya kuvuta ule moshi. Kwa kweli unaweza kufika pahali ukienda vijijini

huko ukamuonea huruma mama jikoni, kwa sababu huku anapika moshi mwingi, macho mekundu machozi yanamtoka. Sasa pale anaathirika.

Mhe. Mwenyekiti, yale anafanya si kwa sababu anataka, lakini ni kwa sababu ya unyonge. Kwa hivyo, nafikiri ni jambo muhimu sana tuzingatie namna ya kuhifadhi mazingira, lakini kwa kumuwezesha Mzanzibari aweze kutumia nishati mbadala kwa kazi hizi za kupikia kwa sababu ndio asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri sera hii kama nilivyoeleza awali kwa mashirikiano na sera nyengine zikaendeleza suala hilo la kuhakikisha linamkomboa Mzanzibari kutokana na unyonge huu.

Nishati ya umeme ni nishati moja muhimu sana, kwa kweli wenzangu wameeleza kwa urefu sana. Ukiangalia hapa ukurasa wa 7, umeme una asilimia ndogo sana ni 4% tu, lakini ukweli asilimia 4% hii kazi yake inayofanya katika nchi ni kubwa sana. Huwezi kuendesha hata shughuli za serikali kama huna umeme, kwa kweli sasa hivi katika kipindi hiki kifupi ambacho tuna matatizo ya umeme basi mambo mawili yatakuwa, ama watu watakuwa hawafanyi kazi maofisini au wakifanya kazi watakuwa wanafanya kwa gharama kubwa sana.

Nimewasikia watu wa taasisi mbali mbali wakitathmini gharama wanayopata kwa kuwasha majenereta ni kwamba hawana budi tu, lakini ni kazi ambayo hailipi tena sasa hivi. Sasa unaweza ukakuta umuhimu wa umeme kuendesha shughuli za ofisi, lakini shughuli nyengine za umeme ni muhimu kweli kweli ni tatizo ambalo tunakabiliana nalo sasa hivi la maji. Asilimia hiyo 4% tulipoikosa katika mji wa Zanzibar ni tafrani sasa hivi.

Wewe ukiwa na jenereta na kisima unavuta maji basi utavuta maji wee mwisho utaangukiwa na ugomvi kwa sababu hatimaye utashindwa kumudu yale mafuta. Serikali inajitahidi kusambaza magari ya maji yale, lakini hapo linapotuwa gari lile likasimama basi watu watapigana kwa kuwania maji. Asilimia 4% imekosekana. Biashara zote zinakwenda kwa hasara sasa hivi na viwanda vingi vidogo vidogo vimefungwa. Kuna vijana wanajiajiri sana katika shughuli za ufundi seramala. Hivi sasa wameshindwa kufanya shughuli zao kwa sababu ya umeme.

Jana au leo asubuhi Mhe. Abass Juma Muhunzi alimuuliza Mhe. Waziri wa Fedha ni hasara ngapi tunaweza kuziona zimepatikana kutokana na muda huu ambapo umeme haupo? Ni suala ambalo kwa kweli halijibiki, lakini kama utafanya tathmini basi ni mabilioni ya pesa tayari yamepotea kwa siku hizi chache. Kwa hivyo, umeme pamoja na kuwa ni asilimia ndogo, lakini ni muhimu sana.

Sasa tuna umeme hapa Zanzibar, lakini wengi wamesema na mimi nasema tena, umeme tuliokuwanao na nimesema mara nyingi ninapozungumzia Shirika la Umeme, ni umeme wa kuazima, tumeazima umeme kwa marafiki zetu, haizuri wanatuuzia, lakini ni bidhaa yao. Siku moja wakikasirika wakasema mimi siuzi tena umeme wangu tutafanya nini sisi? Kwa hivyo, nilikuwa na kilio cha muda mrefu cha kuwa na vyanzo vyengine ambavyo hivyo tutakuwa tunavimiliki wenyewe Wazanzibari. Nashukuru sera hii imezingatia yale yote tuliyokuwa tukiwaambia Shirika la Umeme mara nyingi.

Kuna vyanzo vya nishati ya jua ambapo kwa mazingira yetu Wazanzibari tuna jua muda mrefu sana kwa mwaka ambapo tunaweza tukautumia sana na wako wachache ambao wanafaidika kwa kutumia nishati ya jua. Nishati ya upepo nashukuru imeelezwa vizuri katika ukurasa wa 29 kama hivyo. Sasa ni muhimu haya mambo kwa kweli kama wenzangu walivyotangulia kusema yasibakie humu ndani ya daftari la sera, lakini mambo haya Mhe. Waziri, tukitoka hapa leo au kesho tukiipitisha sera yako ni muhimu mambo haya yatafutiwe nyenzo haraka sana yaanzishwe. Wazanzibari tunahitaji kujikomboa na huu ndio ukombozi, sasa katika ukombozi lazima *seriousness* iwepo.

Halafu ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme likaimarishwa vya kutosha. Kwa sababu sasa hivi hata *labour force* nafikiri ni ndogo. Hili mimi nime-*experience* kule Pemba. Miundombinu ya umeme sijui ni kwa sababu muda umekuwa mrefu au sababu gani, lakini mara kwa mara inapata matatizo. Mfano mzuri ni ule niliyoutoa kule kijijini kwangu, *wire* umeanguka na siku hizi kuna vibaka, *wire* ukianguka tu wanaukimbilia na wanauiba, umekaa chini *wire* ule siku kumi, nimekwenda katika shirika jamani *wire* umeanguka, kila nikienda meneja ananambia bwana vijana wako kazini nafasi hatuna.

Sasa hii inaonesha kwamba wafanyakazi wa shirika Mhe. Waziri ni kidogo, basi ni muhimu katika kuimarisha Shirika la Umeme basi na wafanyakazi wakaongezwa ili likitokea tatizo iwe kama ule moto uliyotokea kule Manchester wakati alipokuwepo Mhe. Juma Duni Haji kule. Ukitoa taarifa, robo saa watu wamesuluhisha lile tatizo, tujitahidi tuwe huko.

Mhe. Mwenyekiti, kila nililokusudia kulisema wenzangu wamelisema kwa hivyo, sioni haja ya kupoteza wakati mwingi sana. Nataka nitamke tu, na hili nalitamka kutokana na *spirit* nzuri tuliyonayo hapa Zanzibar sasa hivi ya maridhiano. Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa 4 sijasema hivi nitakavyosema leo. Leo nasema sera hii naiunga mkono mia kwa mia na nadhani kwa kuwa nawawakilisha wananchi wa Jimbo la Chonga nasema kwa niaba yao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza na mimi kunipatia nafasi kidogo ya kuweza kuchangia baadhi ya mambo. Kwanza napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wizara hii ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutengeneza sera ambayo tulikuwa tunaisubiri kwa muda mrefu na kwa bahati nzuri sera hii tumeipata na kwa kweli sera hii imetupa mwelekeo mzuri sana iko wazi, inafahamika, inaeleweka na ina tija ndani yake na tutafaidika.

Kwa hivyo, mbali ya kumshukuru yeye Mhe. Waziri, lakini pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa wale watendaji wake katika afisi yake. Makatibu na wafanyakazi wote katika wizara hii kwa kushirikiana na Waziri kwa kuweza kutoa sera nzuri sana kama hii ambayo inatupa mwelekeo katika mambo yetu ya baadae. Namshukuru ahsante.

Lakini la pili, ni kwamba mambo mengi yamezungumzwa tangu asubuhi, lakini kuna mambo mengine ambayo hayajazungumzwa na mimi nataka kidogo niyagusie ambayo yamo katika sera yetu.

Mimi nataka nizungumze mazingatio maalumu. Katika mazingatio maalumu haya kuna mambo mawili ndani yake, kuna suala zima la hali ya hewa na suala jengine ni mazingira. Sera yetu hii ya nishati imeshatueleza vya kutosha kwamba ipo Sera ya Mzingira ya Zanzibar tangu mwaka 1992. Madhumuni makubwa ya sera hii yalikuwa ni mambo mawili, moja ni kulinda mazingira haya na la pili ni kuhifadhi mazingira haya. Sasa katika suala la mazingira bila shaka ni muhimu katika suala la sera hii, lakini kama vile walivyozungumza katika sera kwamba pamoja na yeye Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, lakini vile vile kuna sekta nyengine zina shughuli za kumsaidia Waziri katika kuweka mambo sawa.

Kwa hivyo, suala la mazingira utakuta kuna wizara ambayo inashughulikia suala hili, lakini tuangalie. Je, ikiwa suala ni la kulinda na kuhifadhi mazingira kwa kiwango gani tangu siku hiyo mpaka leo wizara imechukua? Kwa sababu hali inajitokeza kila mahala kuna mazungumzo mazito juu ya suala la mazingira. Je, wizara hii upande wake imechukua hatua gani?

Mhe. Mwenyekiti, sera hii inahitaji kuwa na mwelekeo mzuri ambao utakuwa unafuata mila zetu na desturi za zamani, kwamba watu wetu si wakaidi sana katika kufuata mambo. Lakini labda niseme tu elimu imekuwa ndogo kwa watu hawa. Kwa sababu hali inayojitokeza sasa hivi ya kimazingira ni mbaya sasa kusema tu kwa kulinda na kuhifadhi bila ya kuweza kuchukua hatua zozote, lakini vyenginevyo ni kwamba wananchi wanahitaji kuelimishwa vya kutosha,

nini faida ya mazingira kuwepo na nini hasara ya kutokuwa na mazingira mazuri. Kwa hivyo, kuwaelimisha wananchi ni jambo muhimu sana.

Vile vile, ningeshauri kwamba kuna miradi mingi sana ya maendeleo katika nchi yetu. Pia, watu hawa wangeshirikishwa vya kutosha ili kuweza kutusaidia kupiga vita uharibifu wa mazingira. Lakini kubwa zaidi tuone kwa pamoja sote kwa sababu hili si suala la mtu mmoja, ni suala letu sote. Kwa hivyo, upatikane mwamko wa kimazingira, nafikiri hili litaweza kutusaidia vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili ni hali ya hewa. Hapana anayekataa kwamba hali ya hewa kwa muda mrefu sasa hivi imebadilika kutokana na kupanda sana kwa kiwango cha joto. Kiwango cha joto kimepanga takriban sio hapa tu, lakini ni nchi nyingi duniani. Kadiri kiwango cha joto kinavyopanda juu bila shaka kutakuwa na athari nyingi katika nchi na kinaonekana.

Jambo jengine vile vile ambalo linasababisha kuongezeka kwa kiwango cha kima cha bahari, bahari imepanda juu na tunaona siku zote kunakuwa na mmong'onyoko wa ardhi kutokana na kima cha maji kupanda juu. Kwa hivyo, hizi ni sababu tosha za kuonesha kwamba kuongezeka kwa maji na joto kubwa lilioko katika nchi na kadiri tutakavyofanya hata tukiwa na hii nishati ya umeme, lakini utaona nayo pia inaongeza joto na lazima upate viburudisho vyake baada ya kuona na *bulb* ndani ya nyumba lazima uwe na feni au *air condition* kupunguza joto liliomo ndani.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana tukashauri kwamba ni vyema kwa wakati tulionao tuweze kutumia *energy sever* ambazo kidogo zinaleta ubaridi katika nyumba ili kupunguza joto, kwa sababu lisitubane lile la kawaida na hili joto la ndani ya nyumba pamoja na kuwa tunahitaji taa tuone kwa kufanyia shughuli zetu mbali mbali, lakini vile vile linatuumiza kwa upande wa pili.

Mhe. Mwenyekiti, ukame umekuwa mkubwa sana kutokana na suala hilo kwa hivyo, ningeshauri kwamba watu wapate elimu ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja muhimu vile la utoaji wa gesi chafuzi. Suala hili liko kila pahala kutokana na hali ya joto ilivyokuwa imepanda juu na kufanya ushajihishaji wa uezekaji tuwatafute hawa wawekezaji na utekelezaji wa teknolojia. Hatuna budi tuingie katika teknolojia kwa sababu gesi hii mbaya ambayo inachafua mazingira yetu ni lazima tuweze kuidhibiti.

Kwa hivyo, ni teknolojia ambayo sisi hatujawa nayo, lakini kama tunataka kuhifadhi gesi hii chafuzi inayosababisha hali ya joto kupanda juu lazima kipatikane chombo muhimu cha kimataifa ambacho kitaweza kupunguza gesi chafuzi. Sasa ikiwa katika nchi yetu hapana basi tuweze kukitafuta.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kwamba serikali ina mambo mengi na wizara ina kazi nyingi sana, lakini Sera hii ya Nishati imekusudia kuleta maendeleo kwa wananchi. Katika maendeleo haya tunayotaka kuwaletea wananchi wetu ni mazuri na yenye manufaa kwetu. Lakini pia, tuangalie upande wa pili hali ya umaskini walionao watu wetu. Hakuna mtu anayekataa mambo mazuri, lakini kuna sababu za kukataa mazuri. Umaskini unapokuwa mkubwa hata hayo mazuri kama unayataka wakati mwengine ni vigumu sana kupatikana.

Kwa hivyo, umaskini umetanda na utakuta mara nyingi maendeleo haya ya nishati na mambo yote haya mazuri mazuri utaona yanaanzia mjini, ndio maana utakuta watu wanahama mashamba wanakuja mjini kutafuta zile raha za mji.

Sasa kwenye suala la nishati ya asili kwa watu wetu hawa tulionao, kuna suala la kuhakikisha kwamba hili suala tuliondoshe, tutaliondosha vipi. Lazima tuweke katika *long term programme* ni mambo ya muda mrefu, *medium* ya kati na kati na yale ya *shorter*. Yaani haya mambo ya muda mrefu kwa sababu hatuwezi tukayaondosha yote hayo kwa mara moja, matatizo ya ndani ya nchi hatuwezi kuyaondosha mara moja, ni lazima tuyaondoshe mambo haya kidogo kidogo.

Kwa hivyo, kwa kutumia *programme* mbali na kwa sababu mambo haya ni ya kiasili si rahisi kwa mara moja kuweza kuyaondosha. Nia ya sera hii ni kuwatoa watu huko tuliko na kuwapeleka katika mambo yetu ya kisasa ambayo ni mazuri zaidi. Sasa kuwatoa watu ambao wanashughulika na mambo yao ya kiasili ni vigumu sana kutokana na hali hiyo, ndio maana utakuta leo miti inateketea na mambo kadhaa wa kadhaa yanajitokeza katika nchi.

Kwanza katika suala hili tunahitaji kuwaelimisha watu wetu, ni vizuri sana waelewe ili waachane na mambo haya. Lakini utakuta suala la kupiga vita ukataji wa miti bado utakuwa unaendelea, pamoja na jitihada yote minazi inakatwa, miti mikubwa mikubwa inakatwa na miti midogo midogo inakatwa. Kuna watu wanaokata miti midogo midogo kwa ajili ya kupata kuni, kuna watu wengine wanakata miti kwa ajili ya kujengea, kuna watu wanakata miti kwa kutafuta fito za kutengenezea bustani zao.

Kwa hivyo, kwa njia moja au nyengine mazingira yanaumizwa, ndio maana hii hali kama hatukuwa na hadhari kubwa mwisho hii nchi tutaifanya iwe jangwa. Kila tukiondosha miti joto linaongezeka na ni hasara kwa nchi yetu.

Sasa pamoja na kuwa sera hii ya kutaka kuondosha hili tatizo, lakini tuone tu kwamba tukiangalia katika nchi yetu kuna mambo kadhaa wa kadhaa. Kuna watu wanatumia kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, matumizi ya kuni

katika majumba yetu tuliyonayo ni njia moja ambayo ni rahisi zaidi na ni nyepesi zaidi na haina gharama kubwa sana, ni kutoka na panga mtu akakata miti akaenda akapika chakula chake.

Lakini kuna watu ambao wanakata miti kwa wingi sana. Kwa mfano tunakuta katika mabekari yetu ya mikate magari kwa magari mizigo ya kuni inapelekwa watu wanapika mikate. Haya ni mambo yetu ya asili ya kale, lakini tunaweza kwa njia ya kuelimisha watu wakaacha kutumia kuni kwa ajili ya kupika mikate badala yake wakatumia ma-*oven* ambayo hii itapunguza ukataji wa miti.

Lakini pia, tunaona katika maeneo yetu mengi kuna mahoteli kila pahala yamejaa, shamba kuna mahoteli, mjini kuna mahoteli, ama watatumia miti au watatumia makaa. Sasa hili ni suala zito sijui tutafanya njia gani kwa hao watu wenye mahoteli makubwa makubwa na yamejaa nchi nzima. Vipi tutadhibiti matumizi ya kuni katika maeneo hayo.

Ukenda huko Jeshini utakuta kila siku magari kwa magari yanapeleka kuni huko watu wakapikie vyakula. Ukienda katika vyuo vyetu vyote takriban Unguja na Pemba, magari ya Fidel Castro yanakwenda mashamba yanakata mikarafuu wanapelekewa kule kwa ajili ya matumizi ya kuni. Sasa hili ni suala zito na ni suala kubwa sana. Je, njia gani ama mbinu gani tutafanya ili kudhibiti suala hili lililokuwa kubwa zaidi.

Maana kuna mambo mengine ni *small scale* ya matumizi ya nyumbani, lakini hii *large scale* ya matumizi kama humo kwenye mabekari, mahoteli, maskulini na Jeshini mnahitaji udhibiti wa hali ya juu.

Zaidi ya hilo Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji kutumia teknolojia mpya ili kuweza kupata fedha. Fedha ni lazima zipatikane kwa kuweza kutoa msukumo katika mambo yetu yote. Ingawa Waswahili wanasema “Pesa sio msingi wa maendeleo” sijui vipi tafsiri yake hii, lakini naona bila ya fedha mambo mengi hayawezi kwenda.

Tuwaelimishe watu na tuwape maarifa mbali mbali. Tunahitaji kuwatoa watu katika hali ya umaskini kupunguza umaskini, hatuwezi tukauondosha moja kwa moja umaskini. Kwa hivyo, hapa sera hii ina kazi kubwa sana si kwa maneno tu, lakini pia na kwa vitendo ni lazima tupate fedha ya kutosha ili kupunguza huu umaskini.

Katika kuwatoa watu kule waliko hivi sasa na kuwapeleka katika hali nyengine mpya ni lazima tuondoshe tabia ambayo tayari tunayo *(habit formed).* Mtu kumuondosha tabia yake ni ngumu sana na ni nzito. Kwa hivyo, tuna kazi kubwa sana ya kuwaondosha watu waliko na kuwaleta kule. Sasa tunahitaji

fedha kuwaondosha kule waliko. Katika fedha hii inawezekana kwamba wizara wakati mwengine inaweza ikafumba macho ikawasaidia watu kuwapelekea umeme kule waliko. Wanaweza kuwapelekea umeme kwa njia ya *solar*, upepo au nyengine yoyote ya jua.

Lakini hata hivyo, sisi haja yetu tunataka wananchi waachane na tabia hii ambayo nimekwishaizungumza. Kwa kuwa matumizi haya ya mkaa pamoja na kuni sio tabia nzuri katika maendeleo ya nchi. Sasa, je, hili suala tutalipunguza kwa kiasi gani ili kuhakikisha. Lakini pia, tunaweza tukawafundisha watu wetu namna ya kujiingiza katika miradi na kuweka pesa za akiba ili kuweza kujisaidia wenyewe baadaye. Yaani hii iwe ni mkakati maalumu wa wananchi kuelimishwa na kuweza kuona kwamba kila mtu apate huu umeme.

Pesa taslim mtu atakuwa hana, lakini hivi sasa zinaweza kuzalishwa njia za kuweka pesa benki au kuweka katika mradi maalumu. Wajiingize katika njia za uwekezaji maalumu. Kwa mfano kuna taasisi ndogo ndogo za fedha wakaweka fedha zao au katika mabenki au njia zozote nyengine zitakazowasaidia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la kupanda kwa bei za umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bei hizi za umeme ni kubwa sana, hali ya watu wetu ni maskini sana na ni sisi tunataka kuwatoa kule katika hali hiyo wanayokwenda nayo sasa, mazingira wayaache vile vile, lakini tuwaweke katika matumizi ya umeme. Lakini sasa Unguja bado haijawa na uwezo wa kuzalisha umeme, umeme tunaotumia hapa ni kutoka Tanzania Bara, umeme unaotoka kule wao wana hiari zao kuuweka kwa bei wanayoitaka wao, sisi hatuna mamlaka nao kwa sababu si wetu. Laitani kama ni wetu tungeweza kuiweka nishati ile kwa bei rahisi ili tukawasaidia watu wetu.

Kwa hivyo, bei zinaweza kupanda kutokana na njia mbali mbali, vifaa vinavyopanda bei wanaweza kusema kwamba bei ya umeme ambayo sisi wakati mwengine tunashindwa. Sasa kama ikiwa suala ni hilo bei ni kubwa, inabidi sasa kwa kuwa Shirika la Umeme liko kule na sisi tuna Shirika letu hapa la Umeme la Zanzibar, mimi ningeshauri tu kwamba kwa masuala hayo ni lazima mashirika haya mawili yakae kitako pamoja na kuzingatia hili suala zima la bei hususan kwa nchi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, umeme ni suala ambalo tunalitegemea halijawa letu, ni umeme tegemezi, tunautegemea huu umeme kutoka Tanzania Bara. Lakini mimi naamini si muda mrefu tutakuwa na umeme wetu wenyewe. Lakini pia, si vibaya sisi siku za nyuma tulishauri tuwe na umeme mbadala ambao mimi naamini unaweza ukatusaidia pakubwa sana. Kuna njia chungu nzima za kuweza kupata umeme mbadala zaidi ya huo, kuna umeme wa jua, kuna

umeme wa upepo, kuna umeme wa njia ya nishati ambao tunaupata sasa *hydroelectric power*, lakini sisi bahati mbaya hatuna maji wenzetu ndio waliyonayo. Kwa hivyo, tunategemea umeme kutoka huko na bei kupanda ni wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba baina ya hizi nchi mbili ziweze kuwa na mazungumzo mazuri na makubaliano ambayo yataweza kuwasaidia watu wetu kwa kipindi hiki tulichonacho.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba hii Sera yetu ya Nishati ya Zanzibar haitaki kufanya kazi peke yake inaomba msaada. Lakini mimi nina wasi wasi, mara nyingi tunazungumza hapa ku-*share* mambo kwa pamoja kwamba tunafanya kitu *interdependent* yaani kwa kutegemeana. Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi haiwezi peke yake kulifanya suala hili, kila sekta katika masuala haya linahusika, lakini sasa jukumu linabakia katika wizara hii.

Sasa tusiwe kama ile tuliyosema ya kilimo ambapo sekta ya utalii imeingia kuipa nguvu sekta ya kilimo, tukasema zile ni *clusters*, nakumbuka tumezungumza nyuma mambo ya *clusters*. Sijui haya mambo ya *clusters* imetoa mwamko kiasi gani kuipa nguvu hii Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Nishati haiwezi kwenda peke yake, ni lazima sekta zote zishiriki. Mimi nafikiri labda tuandae kitu kama *job description* ya kila sekta kwamba wewe bwana unahusika maana mzigo wote unaelemea katika wizara moja. Hapa tunazungumza, lakini baadaye naamini hili suala lote litakuwa la Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi sekta zote zitakaa upande.

Lakini sijui tutafanya kwa kiasi gani kuweza kutoa mchango wetu kusukuma mambo haya kwa sababu hili si suala la sekta moja, ni suala la sekta zote. Kwa hivyo, ni jukumu la Sera ya Nishati kuimarisha kama kilimo inahitaji vile vile kwa sababu tunazalisha chakula. Sasa na yeye kwa upande wake ni lazima Sekta ya Kilimo, Sekta ya Biashara pamoja na Sekta ya Utalii zote hizi zitakuwa na majukumu katika kuisaidia Sera hii ya Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni kilimo tunajua na yeye vile vile ana dhima yake, lakini anahitaji kuzalisha vyakula vingi, huyu anahitaji kusafirisha vyakula, lazima yapatikane magari ya kupeleka chakula hiyo ni nishati vile vile, lazima watu watatumia mafuta kama si dizeli na petroli. Lakini pia, na yeye anahitaji suala la *irrigation*, anahitaji umeme, ana mambo chungu nzima anayoyahitaji. Kwa hivyo, nafikiri suala hili si suala peke yake la wizara hii,

lakini itakuwa ni wizara zote. Mhe. Mwenyekiti, naomba bidii iwepo ya kukuza uzalishaji, tukuze uchumi kwa dhamira ya kupunguza umaskini. Kila tukizalisha mahitaji bila shaka yanaongezeka, nishati pia inaongezeka. Mambo yote haya ni muhimu na tunahitaji kushirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri atajitahidi upande wake kuangalia kwamba kila anayehusika katika sekta hii kukabidhiwa jukumu lake, lakini *follow up* iwepo au tathmini ipatikane, sekta hii imekabidhiwa kitu kadhaa wa kadhaa wafanyiwe ufuatiliaji ili kuona hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwa ufupi kwamba watu wetu mazuri wanayataka, lakini namna ya kuwaondosha kule waliko na kuwaleta huku kidogo ni ngumu. Kwa hivyo, sijui mbinu gani tutatumia kwanza kunusuru mazingira na kuwanusuru watu wetu kutumia vitu visivyotakiwa. Kama ilivyozungumzwa matumizi ya kuni ni moshi, kuna athari nyingi katika maumbile ya kibinadamu kwa kutumia moshi. Tunaona athari ya binadamu kwa haya mambo yote yaliyopo kwa mfano ya *pollution*, athari ya kimazingira, hewa *carbondioxide* imekuwa nyingi, gari ikipita inatoa *carbondioxide* na mashine zote moshi mwingi.

Hivi sasa majenereta yaliyopo katika mji huu *carbonmonoxide*, kiasi gani hapo iliyopo, pale ipo na pale ipo. Sasa *carbonmonoxide* inaathiri katika afya ya binadamu. Kwa hivyo, mimi nafikiri tujitahidini kama inawezekana sasa hivi hali ni kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nishati ya viumbe ni katika nishati ambayo nafikiria mimi zaidi ya hii. Unajua tuna vyuo na kuna madakhalia mengi tu. Kwa hivyo, tunaweza kutumia badala ya yale mabaki ya *wasted* ya binadamu anayoitupa inatiwa katika shimo. Kwa nini katika chuo hatuweki *chamber* kubwa moja kile kinyesi chote kinachokwenda kule kikatiwa pahala chini kule tayari umeme upo pale, lazima tutumie umeme huo, tutapuuza kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba popote penye mkusanyiko wa watu mia au mia tano kile kinyesi cha pale chote kichimbiwe shimo huko chini kijengwe kwa matofali ili kinyesi kitakachopatikana tuta-*radiate* tutatumia taa na kila kitu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kupata nafasi hii kuchangia Sera ya Nishati ya Zanzibar hasa tukizingatia kwamba sera hii ni muhimu kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hii kwa kuhakikisha kwamba suala hili linasimamiwa vyema na linapata muelekeo na ufanisi kwa ajili ya hatima ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nishati ya umeme ni chanzo muhimu kwa mambo mbali mbali ya maendeleo katika nchi. Mimi tegemeo langu kwamba nishati hii ni kipaumbele kwa maslahi ya watu wetu na maendeleo ya maisha yao ya kila siku. Bila nishati hii kuwepo madhara, matatizo na mambo mbali mbali yatajitokeza hasa tukizingatia kwamba wananchi kwa asilimia mia moja wanategemea nishati hii kupata mahitaji yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nishati ya umeme licha ya kuwa ni mtaji wa wafanyabiashara mbali mbali, lakini pia, ni kipumziko cha binadamu kwa njia moja anayotumia alimradi mambo yake yatakwenda kama alivyojipangia pindi akiwa nayo. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Waziri, kwa kuhakikisha kwamba Sera ya Nishati ya Zanzibar imeletwa wakati mzuri hasa tukizingatia kwamba tuna matatizo ya historia katika nchi yetu yaliyojitokeza. Haya hailaumiki wizara wala serikali, bali ni mambo ya Mwenyezi Mungu, huna uwezo nayo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna vianzio vingi vya nishati hii ya umeme. Wenzangu wametangulia kusema mengi zaidi, lakini mimi nitakuja katika maelekezo mengine ambayo yatasaidia katika kukuza nishati hii na kuleta maendeleo kwa jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, taaluma ni jambo muhimu na ndio kitu muhimu kwa wananchi wetu na kwa walengwa wetu ambao wataendesha shughuli hii ili kuhakikisha kwamba wanajipanga vizuri, wanakwenda katika mafunzo mbali mbali ili kuhakikisha kwamba tunapata watendaji wazuri na nishati hii inaendelea vizuri katika mambo yake waliyojipangia kwa kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, taaluma ndio njia moja wapo ya kumpa mtu mwongozo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa sera hii imeletwa wakati mzuri na naamini matayarisho haya ndio mwanzo wa kuelekea huko tunakotaka kufikia, basi namuomba kwa heshima kabisa vijana wetu madhubuti Wazanzibari bila ya kutegemea mkopo kutoka kwa wenzetu. Nakusudia mkopo huu tusiazime watu kutoka nje ya hapa Zanzibar kwa muda huu, tuhakikishe kwamba tunawapata vijana wetu wazuri, wenye taaluma nzuri na wanakwenda kupata mafunzo haya kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba nishati ya umeme Zanzibar na mambo mengineyo tutaishughulikia sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba tuna vijana wetu wengi wazuri wataalam katika fani mbali mbali kama watawezeshwa na wataendelezwa basi tutakuwa

hatuna shida ya kufanya lolote. Kwa mfano tuazime mtu huyu tulete kwa ajili ya shughuli zetu. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana wizara kwa kuwa suala hili tunaliandaa, basi ni vyema kabla halijawa tayari vijana hao nao wakaandaliwa wakawa tayari kuwa *stand by* kwa lolote linalotokea ili kufanya kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, taaluma ni sehemu moja wapo ambayo nimesema inaleta kila kitu, lakini pia, katika sera hii nimeona kuna wizara nyingi ambazo zimejipanga kwa ajili ya kuingia katika mikakati mbali mbali ya kuhakikisha kwamba inakwenda sambamba na Wizara mama ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi au wizara inayohusika na nishati kama ilivyoeleza sera hii.

Mhe. Mwenyekiti, Tawala za Mikoa nayo imetajwa katika sera hii. Kwa hivyo, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa inawaeleza wazi wazi kwamba wao ni wahimili wa mwanzo kuhakikisha kwamba taaluma zinatolewa wilayani na mikoani kupitia Masheha kwa ajili ya kuwapa maelekezo watu wetu juu ya kutumia rasilimali ya nishati tulizokuwanazo katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulilokuwanalo hivi sasa mwananchi anaelewa nishati ni sehemu moja ya umeme au mafuta, kumbe nishati ni sehemu mbali mbali ambazo zimo kwa njia moja au nyengine. Kwa mfano ukitumia kuni ni nishati ya kuni, ukitumia takataka ni nishati ya takataka, ukitumia vinyesi ni nishati ya vinyesi. Lakini sisi tunaelezea zaidi kwamba kuni ni nishati kubwa sana inayotumika hapa kwetu Zanzibar hasa tukiangalia kwamba wananchi wetu wengi walioko mijini na asilimia kubwa walioko vijijini hawana njia nyengine mbadala wanayotumia isipokuwa kuni. Kwa hivyo, nishati hii ikiendelea itaathiri harakati za nchi yetu na mazingira pia yataharibika.

Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane tu kwamba nishati ni sehemu moja itolewe taaluma na Tawala za Mikoa ili kuhakikisha kwamba wanaohusika na shughuli mbali mbali za kila siku kuwapa taaluma wananchi wetu na kufikia pahala ambapo waelewe nikikata mti nipande miti. Kwa sababu ukikata mti ukipanda mti utachelewa, lakini ukikata mti mmoja panda kumi na moja au hamsini ili kunusuru ile sehemu ya nishati isipotee.

Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika pia Afya yaani Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni mhimili mmoja wapo wa kuhakikisha kwamba madhara mbali mbali yanayojitokeza katika nishati tunazotumia wawe tayari kuwaelezea wananchi wetu matumizi mabaya ya nishati pindi yakizidi athari yake inatokea kitu fulani.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, ukikata miti unapata athari ya kiafya kwa sababu joto au ukame utaongezeka. Kwa hivyo, maradhi ya aina mbali mbali yatakuja pale. Pahala palipokuwa hapana wastani wa miti basi pana maradhi

fulani yanajitokeza. Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara inayohusika kuhakikisha kwamba inatoa taaluma na matumizi mazuri ya nishati ili wananchi waelewe athari ya miti au mambo mengineyo kwa ajili ya afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Utawala Bora imeelezwa wazi wazi, naomba ninukuu. "Kushirikiana na Idara inayohusika na Nishati katika utayarishaji wa mikataba ya utafutaji na uwekezaji wa mafuta na gesi asilia na mikataba mingine inayohusiana na nishati".

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri suala hili ni zuri kwa sababu bila ya mikataba mizuri basi hatari inaweza kutokea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, pamoja na maelezo haya mazuri wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ikatafuta wataalam wa kutosha, wanasheria wazuri ili kuhakikisha kwamba mikataba inayowekwa inanufaisha wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuitaja nchi fulani, lakini ni marafiki zetu wa karibu sana. Wenzetu wana mambo mengi ya madini mpaka leo wana kiu, wanasema kwamba pamoja na rasilimali kubwa waliyonayo, lakini bado wako katika umasikini mkubwa. Kwa hivyo, mimi namuamini sana Mhe.Waziri na watendaji wake kwamba ikiwa watasimamia mikataba mizuri na ya uwazi ambayo haina mashaka, basi rasilimali hii kweli kwa asilimia mia moja itawanufaisha watu wetu na kuondokana na umasikini uliokuwa mkubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tukubali kwamba tuna bahati Wazanzibari, hivi sasa tunaingia katika milioni moja laki mbili na kidogo katika sensa iliyopita. Lakini Mwenyezi Mungu akitujaalia mafuta na gesi yakipatikana na *inshaallah* kwa uwezo wake *Allah* yatapatikana, naamini wazi kwa hali na mali tutanufaika Wazanzibari bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala si la utani ni zito. Mimi naamini kama Mwenyezi Mungu akitujaali likitokea, basi Wazanzibari waamini kwamba wamekomboka kwa asilimia 100 hawana wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo linahusiana na wizara inayoshughulikia maafa, wizara hii kwa hapa kwetu ni Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa sasa hivi, lakini kimuundo ndio itakavyokuwa hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba mafuta na gesi asilia na maafa mengineyo yanayotokana na nishati hii, tukubali kwamba kila penye kazi nzuri, pana hatari au kwenye kazi yako ya maisha pia pana hatari vile vile. Kwa hivyo, niseme tu kwamba wakati wa kuandaa mambo haya, basi kitengo chetu hiki kiwe karibu sana hatutarajii na tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe yasitokee maafa.

Lakini tunasema kwamba maafa ni sehemu moja Mwenyezi Mungu kayaweka kwa njia zake anazozijua yeye, tunamuomba Mwenyezi Mungu asituletee narudia tena.

Juzi wenzetu wa kisiwa cha Haiti karibu watu laki mbili wamekufa na hadi leo wanahangaika. Serikali juzi ilikuwa imeshafikia hatua ya mwisho kuwa isiendelee kutafuta watu waliokuwa hai, lakini kwa rehema zake Mwenyezi Mungu jana kaokolewa wa kijana na nimemuona mwenyewe kwenye televisheni anaokoka bado kadhofu, lakini anacheka anasema bado niko hai, ni kijana tu wa miaka kama 24. Kwa hivyo, serikali ikafuta usemi wake ikasema bado endeleeni kuwatafuta watu wanaimani kuwa bado wapo.

Kwa hivyo, haya Mhe. Mwenyekiti, hayazuiliki kwa sababu Mwenyezi Mungu analoliandika analijua yeye. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri, kitengo hiki ni muhimu sana na kuwepo wenyewe tunajua matatizo ya mafuta na ndio maana tunaambiwa kwamba hata wale watu wanaojenga *shell* huwa hawatakiwi kuwa na nyumba ndani ya *shell* au nyumba za karibuni pia ni hatari.

Wengine walikuwa wanapiga kelele kwenye Baraza hili *shell* imejengwa chini ya nyumba yake, mtu anakuambia hataki iondoshwe, lakini ndio wakati tena ukifika tena utatumia unavyotaka mwenyewe, lakini ni hatari kweli. Kwa hivyo, niipongeze wizara kwa kuliona hili.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo ambalo tunaendelea nalo, wadau ni walengwa wakubwa sana katika kufanikisha suala hili. Nampongeza Mhe. Waziri, kwa kuhakikisha wadau mbali mbali au wenzetu wa Norway asilimia kubwa wamejitolea ili kuhakikisha kwamba wanatusaidia kwa hali na mali ili rasilimali hii ya mafuta na gesi ya Zanzibar yanapatikana kwa faida ya Wazanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tuamini kwamba hakuna jambo la peke yako kwa wakati tuliokuwa nao. Asubuhi hapa katika Baraza hili niliuliza swali moja kwamba pamoja na umasikini wetu, lakini bado kuna nchi tajiri zinatutegemea na hizo nchi tajiri hazijitoshelezi wao bila nchi maskini ili kupata yao. Sisi vile vile, umasikini wetu hatuwezi kwenda nao moja kwa moja, lakini tutazitegemea nchi tajiri kwa kutupatia hayo tunayotegemea.

Kwa hivyo, hapa pana mambo mawili yana uwiano, lakini kubwa niseme tu kwamba wenzetu kwa mtazamo wa mara moja wako kwelini. Kwa kuwa wako kwelini, namuomba Mhe. Waziri na watendaji wao tuwaunge mkono, tushirikiane nao, twende nao na tuwasaidie kwa kila hali tuwape msaada. Ni vyema ile taarifa niliyokuwa nimeisema mwanzo tuwaelekeze wananchi wetu

katika maeneo mbali mbali ambapo maeneo yale ni muhimu wakifika hawa wapewe ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha kwamba wanaendelea kupata kila msaada katika utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, tukisimamia hayo kwa asilimia mia moja basi naweza kusema mafanikio yetu yatakuja haraka bila ya matarajio yetu. Mhe. Mwenyekiti, naamini katika utendaji wa kazi zetu, Mhe. Waziri ana watendaji wake mahodari sana, lakini katika uhodari huo wakubali kushauriana na wizara mbali mbali ambazo zimeelezwa humu, kwa ajili ya kupata msaada wa kila hali kwa pale wanapohitaji. Hakuna wizara inayojitegemea bila kupata msaada wa wizara nyengine.

Kwa mfano Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, atakuwa na nishati mbali mbali. Mfano maji na umeme na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, atakuwa na nishati mbali mbali. Mfano nishati ya miti na mengineyo na yeye huyu itabidi nishati yake itembee kule kwa wenzetu ili mahitaji yaje.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunaamini na tuko katika mbio za kuangalia harakati zetu za maisha za kila siku. Wananchi wengi wa Zanzibar hivi sasa wameamka kimaendeleo na harakati nyingi zimekuwa katika sehemu mbali mbali za maendeleo. Ndio nikasema kwamba serikali kwa juhudi zake, msimamo wake na shughuli zake, ndio maana nikasema kuwa hivi sasa inatafuta nishati ya mbadala kwa ajili ya Zanzibar na kwa ajili ya Wazanzibari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, “mtumainia cha ndugu hufa maskini” na mtumainia cha ndugu huyo huyo asitumainie kubebwa na mgongo wa ndugu yake tu. Mimi nimeridhika kwa asilimia mia moja, umefika wakati sasa hivi tuwe tayari ili kuhakikisha kuwa tunatafuta nishati mbadala ya Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya Wazanzibari kwa Unguja na Pemba. Ndio maana nikasema katika swali langu moja kuwa umeme wa Pemba unaotoka Tanga ambao uko mbioni kupelekwa Pemba.

Tunamuomba sana Mwenyezi Mungu atujaalie ukiwaka umeme ule kule Pemba, basi na wa hapa Unguja siku nyengine uwake siku moja ili kuondoa hii adha ambayo imetukuta au maafa ambayo Mwenyezi Mungu na kama ni historia, basi isitokee tena kwa upande mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo kule kuna vinu ambavyo vimekaa tayari vitakuwa vipo na Mhe. Waziri, kaeleza vizuri tu jana katika majibu yake ambayo alisema kwamba pale vilipo vitaendelezwa na vitahakikishwa kuwa vinawekwa vizuri kwa lolote linaloweza kutokea la dharura vikatumika. Kwa

hivyo, mimi niseme tu Mhe. Mwenyekiti, umeme wa Zanzibar hivi sasa umekuwa mkubwa sana ua matumizi yameongezeka mara mia zaidi. Kwa sababu ulipoletwa umeme wa mwanzo kutoka Rasikiromoni kuja hapa, tulikuwa watumiaji ni kidogo sana, lakini leo umeme ule ule ukiwapelekea wenye mahoteli peke yao wa Zanzibar, basi hauwatoshi. Kwa hivyo, nasema kwa sisi kuwa na jenereta la *kilowatts* 20 au 25, bado itakuwa halitutoshi kwa dharura. Tutafute angalau jenereta lenye *watts* 30 au 35, hapo tunaweza kupata mgao wa masaa 2 au 3.

Mhe. Mwenyekiti, kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu na kwa jitihada ya wizara inayohusika, hayo yatakuja na hasa kwa kuwa tuna mahusiano mazuri na wenzetu ambao wanatusaidia kwa hali na mali na wanatusikiliza na tunawaeleza. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, dharura ni jambo la muhimu na ni jambo ambalo linafaa kuhangaikiwa na kushughulikiwa kupata utekelezaji mzuri ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme wa kutosha kwa siku zote, pindi ukikosekana huu wa kutoka Bara basi hapa Zanzibar tuwenayo majenereta yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naamini katika harakati hizi tulizokuwanazo serikali kwa kupitia wizara inayohusika inajua fika kwamba hivi sasa katika maeneo mbali mbali, mimi ningetoa ushauri kama ufuatao. Mhe. Mwenyekiti, tuna mikoa yetu mitano hapa au tuna mikoa yetu mitatu hapa Unguja. Mkoa wa Kusini Unguja, Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa kuwa tuna maeneo mazuri ya kuweka huduma hii ya jenereta, kwa mfano Mkoa mmoja likiwashwa jenereta basi litasaidia Mkoa huo, basi si vibaya Mhe. Mwenyekiti, tusijilazimishe lazima liwekwe kwa nchi nzima liwashwe kwa wakati mmoja, hatuna uwezo huo kwa sasa.

Ushauri wangu namuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake. Kwa mfano Mkoa wa Kaskazini patafutwe katikati wapi, basi tunaweka jenereta la dharura kwa Mkoa mzima wa Kaskazini pindi ukikatika umeme wa kutoka KIDATU basi tunalitumia, halikadhalika kwa Mjini na Kusini Unguja. Mhe. Mwenyekiti, naamini na ninakuhakikishia mafanikio yatapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunawaona wananchi wetu kadhaa wana majenereta yao binafsi makubwa kidogo katika baadhi ya vijiji na maeneo mengi yanasaidia sana. Kwa hivyo, mimi naamini kama patakuwa na jenereta kubwa, basi tunaliweka kwa mkoa au wilaya fulani, basi litasaidia na matatizo mengi yanayojitokeza, basi yataondoka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie na ashauriane na watendaji wake kwa linalowezekana kuanzia majumbani, mahotelini pamoja na huduma

ya maji, kwa sababu kero letu kubwa na tunalopigia kelele ni huduma ya maji kwa wananchi ambayo inaleta msongamano mkubwa na tunajua ni kutokana na haya matatizo ambayo yametokea.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu katujaalia katika nchi yetu tuna mambo mengi ambayo yatatusaidia pindi tukifanikiwa kuyapata. Mhe. Waziri, katika jibu lake nililomuuliza jana, alituambia tu kwamba kuna umeme wa jua, upepo na mawimbi na ninaamini pia kuna umeme wa takataka.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya namuomba sana Mhe. Waziri, tuyape kipaumbele sana kwa makampuni ya nje mbali mbali kusaidia ili kuboresha huduma hii ya umeme kwa pale panapostahiki. Mimi nakubaliana na Mhe. Suleiman kwamba umeme Tanzania ni ghali na sisi Zanzibar tutaupata ghali zaidi kwa sababu tunanunua kutoka kwa wenzetu Tanzania Bara. Lakini umeme wa Tanzania unavyopigiwa kelele kuwa ni ghali kuliko nchi yoyote kwa Afrika ya Mashariki na Kati.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, kwa kuzingatia hili, makampuni yakijitokeza kwa umeme wa jua, upepo, mawimbi au takataka, basi wakijitokeza makampuni kwa umeme wa nishati kama hizo nilizozitaja, basi nina hakika kwamba matatizo ya huduma ya umeme yanaweza kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, nina imani umeme huo unaweza kushuka kutokana na ushindani wa kibiashara. Biashara Mhe. Mwenyekiti, inategemea inavyoelekezwa na pia inategemea jinsi utakavyoizalisha. Mimi nitataka niuze, lakini katika kuuza kwangu serikali ipate fungu lake na mimi mwenyewe nipate fungu langu la kujiendesha, basi ushindani huo ukiwepo na taasisi zikijitokeza, basi ziruhusiwe na ninaomba zijitokeze kwa wingi ili kuhakikisha kwamba ushindani wa kibiashara katika sekta hii ya umeme basi uweze kupata mwelekeo mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali isiogope wala isiwe na hofu kwamba zikija kampuni hizi, Shirika letu la Umeme litakosa fedha hapana. Shirika la Umeme litakuwa na mapato yake pale pale, kwa sababu wao ndio watakuwa nambari moja na watakuwa wanapata fedha zao kutokana na watakavyowakata hawa. Lakini katika makato yao ningewaomba tu pasijekuwa na makato makubwa kwa vile wananchi wetu wanategemea msaada mkubwa wa kupata nafuu ya bei hii kubwa ya umeme iliyokuwepo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tegemeo langu kubwa ninaloamini nishati ya kuni inaua mazingira na misitu. Misitu hii ndio kila kitu kwa wananchi wetu, kwa sababu kama nilivyotangulia kusema kuwa wananchi wetu wengi vijijini hawana kitu wanachokitumia isipokuwa kuni. Bado naiomba wizara yako Mhe. Waziri,

itowe taarifa kuwa hii nishati ya gesi ambayo inatumiwa katika majumba mbali mbali bado inasaidia sana. Kama mwananchi atapewa taaluma nzuri, basi itasaidia pia kupunguza hii rasilimali ambayo tunaitegemea kwenye misitu kwa kuleta kilimo na mengineyo, kwa sababu bila misitu mvua pia zinakimbia.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala zuri na linataka kupewa maelekezo wananchi wetu ili walifahamu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu na kuiweka vizuri nishati hii ambayo itatusaidia siku za mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nategemea kwamba Mhe. Waziri, haya niliyomueleza kwa nia njema atayafanyia kazi na hasa nikizingatia kuwa Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake ni watu ambao wanapenda kuhangaika na kupata mambo mbali mbali mpaka kwa wananchi, wajuwe nini kinahitajika na nini kifanyike ili mahitaji ya kila siku yapatikane kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, naikubali Sera hii ya Nishati ya Zanzibar ya tarehe 8 Disemba, 2009, japo haijatiwa saini, lakini ilipoletwa hapa. Naikubali kwa asilimia mia moja. Ninamuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake, isimamiwe vyema na kanuni zipangwe vizuri ili mahitaji yapatikane kwa ajili ya wananchi wetu wa Zanzibar ambao wanaisubiri kwa hamu. Kila siku walikuwa wanaisikiliza lini itatoka. Kwa hivyo, namshukuru Mwenyezi Mungu kuanzia juzi hadi leo tunaendeleo nayo na hatimaye Mwenyezi Mungu atajaalia itafikia tamati kwa ajili ya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono sera hii, ahsante nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hapa ndio tunafika mwisho kwa leo. Lakini kesho baada ya maswali tutatoa nafasi mbili Mhe. Said Ali Mbarouk na Mhe. Moh'd Ali Salim, halafu Mhe. Waziri, atafanya majumuisho. Kwa sababu kesho tutakuwa na ziara.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 26/01/2010 saa 3:00 za asubuhi)